# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## MSAMBWENI CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

## DIANI SECONDARY SCHOOL

ON

Monday, May 6, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MSAMBWENI CONSTITUENCY MONDAY, MAY 6, 2002, AT DIANI SECONDARY SCHOOL**

**Present:** Com. Nancy Baraza
Com. M. A. Swazuri
Com. Bernard Njoroge

**Secretariat Staff in Attendance:**

Peter Apamo – Programme Officer
Edgar Kagoni – Asst. Programme Officer
Jacquline Nyumoo – Verbatim Recorder

Meeting started at 9.30 a.m with Com. Swazuri in the Chair. Com. Swazuri welcomed participants.

**PRAYER:** in Arabic.

**Com. Swazuri:** Haya wazee, vijana ndugu zangu saalam aleikum. Tumekuja tena hapa kama tulivyoahidi kama mlivyosikia siku nyingi, kwamba Tume itakuja hapa kusikiliza maoni yenu. Leo ndio siku ambayo tuko Msambweni Constituency. Leo sisi tuko hapa watu watatu na wengine watatu wako Bomani kule Msambweni. Kwa hivyo nimekuja hapa na dada hapa anaitwa Nancy Baraza – huyo ni Commissioner; na huyu mzee wangu hapa anaitwa Bishop Bernard Njoroge hata huyu ni Commissioner; na mimi naitwa Mohammed Swazuri mwanijua ni Commissioner na mwana Tume. Kwa hivyo hapa kuna njia tatu za kutoa maoni.

Kwanza wale wanaotaka kutoa maoni ni lazima wajiandikishe pale, na sisi tutasoma majina na kulingana na ile ratiba inayotoka pale. Kuna wengine hawataki kutoa maoni wanataka kusikisa tu, pia ni sawa. Lakini wale ambao wanataka kusema lazima waandike kule maanake hii tutaenda naye Nairobi kuonyesha kwamba furani alizungumza na tuna record hapa yasipotee yale maneno. Na kuna watu wanaandika na sisi pia tuna andika. Kama kuna memorandum lakini hutaki kuisoma utakuja utatwambia utawapatia wale, kuna register pale. Hiyo ni njia moja ya kutoa maoni; umeandika mswaada wako lakini huna haja ya kusoma tutakwenda kusoma.

Pili, umekuja na memorandum au mswaada lakini unataka kupitia kidogo watu wajue umeandika nini, hatutaki usome kurasa

baada ya kurasa nene baada ya neno itachukua muda mrefu na tuko wengi sana kwa hivyo tunataka utupatie mapendekezo peke yake. Ukimaliza pia hiyo utakwenda pale tuaandikisha majina yako na kila kitu tunataka kujua wazee walikuwa wangapi, vijana walikuwa wangapi, wakulima walikuwa wangapi, wafanyi kazi wangapi tujue Katiba imechangiwa na akina nani.

La tatu, unataka kuzungumza hukuandika memorandum yoyote, tutakupatia dakika ngapi – tano. Na dakika tano ni nyingi sana kama wazungumza maneno ni nyingi sana. Dakika tano ili kila mtu apate nafasi ya kuzungumza. Sisi wote tuko hapa hata mkileta karabai hapa, hata kama ni saa tano ya usiku, lakini tusikilize maoni yenu. Na mtu akimaliza kuzungumza pia naye ataenda pale aandike mambo yake yote halafu ndiyo ampatie mtu mwingine nafasi. Tumeelewana hapo? Na kama mtu hawezi kuzungumza Kiswahili hata Kidigo, kama mtu hawezi kizungu hata kiswahili, kama mtu hawezi Kidigo hata Kiduruma ile lugha ambayo wafikiria ukisema utakuwa sawa sisi tutatafsiri hapo. Tumeelewana? Haya bismilahi.

Councillor wewe ndiye no.1 (inaudible) Councillor Mabavu.

**Con. Mabavu**: Basi Bw. Commissioners, Bi Commissioner Madam Nancy, wananchi wa Diani na shukuru kwanza kupata nafasi hii, ili kuweza kutekeleza haki ya jamhuri ya Kenya kupeana maoni yangu juu ya marekebisho ya Katiba. Jina langu naitwa Said Mabavu Mwamabavu.

Kwanza, nataka kuchukua nafasi hii kutoa maoni yangu ya kwanza. Maoni yangu kwanza nasema, serikali inayokuja iwe serikali ya majimbo ili katika jamhuri, kila jimbo liweze kujitawala na kila jimbo liweze kuwa na Governor wake ambaye ataweza kuchaguliwa pia na wananchi na makamu wake pia hivyo hivyo awe anaweza kuchaguliwa na wananchi. Na jimbo hilo liweze kuwa na katiba yake ambayo haiwezi kuingiliana na jimbo kwa mfano kutoka Western.

Kwa serikali hii kuwa Katiba tulionayo ya umoja, tayari tumeona ile hasara yake kwa mfano, tuchukulie wizara ya ardhi. Kila kitu hakimaliziki mpaka Nairobi. Kwa hivyo sababu moja ya kutaka serikali ya jimbo, ni kwamba maswala yote ya ardhi ianzie katika kata, yaani location, wilaya imezidi mwisho wake iwe mkoa. Safari hizi za Nairobi ziweze kupotea. Vile vile kiuchumi, kiuchumi kwa mfano sehemu tuliyo sasa ambayo ni Diani ni sehemu ambayo inaongoza kwa utalii. Kwa hivyo pia tunaomba katika maoni yangu aslimia ile ambayo inatokana na maswala ya utalii, sabini na tano iweze kubaki katika mkoa na ile ishirini na tano iliyosalia iende kwa serikali kuu.

Elimu. Ni maoni yangu pia kwamba aina ya elimu irudi kama zamani, kwanzia darasa la kwanza mpaka la nane na elimu iwe ya bure kwa primary level.

**Com. Swazuri:** Umesema iwe kama ya zamani mpaka darasa la nane?

**Con. Mabavu**: eeh zamani tulikuwa tunaenda mpaka …………. Vile vile katika maoni yangu kuhusu maswala haya ya Provincial Administration – maChifu, Ma PC, DC wawe wanaweza kuchaguliwa na wananchi wenyewe na yule Governor wa jimbo awe na mamlaka kamili ya ku-appoint ma-judge, kama kutakuwa na wale wa sector nyingine zote, iwe na uwezo wa yule ni governor – uwezo ambaye ni kwa wakati huu tunaupunguza kutoka kwa Rais wa wakati huu. Kwa maana nasema uwezo ule wa Rais upunguzwe upelekwe katika majimbo. Rais wa jamhuri awe atachaguliwa lakini asiwe anatoka kwa chama chochote, na kazi yake iwe ni Head of State na kuleta mawasiliano bora na mataifa mengine, iwe kazi ya Head of State. Vile vile tuweze ku-create katika Katiba -serikali inayokuja tuweze ku-create nafasi ya waziri mkuu. Pia katika maoni yangu ninapendekeza na ni maoni ya watu karibu elfu hamsini ya watu wa Diani, ni kwamba katika sector hii ya kutaka jimbo, na jua wengi huwa na wasi wasi, hasa sasa sisi watu wa Pwani tunataka majimbo lakini si majimbo yale watu wengine wanafikiria ni majimbo ya kawaida kama Ugerumani. Kwa hivyo ziko nchi ambazo imekuwa vigumu kukubali majimbo, lakini ilifika stage wakakubaliana, kwa mfano kama Canada iko sehemu ambayo hiyo nchi nzima, nchi nzima iko hivyo lakini hiyo sehemu imepewa jimbo lake. Kwa hivyo sisi watu wa sehemu hii tunasema, hata kama itatokea kwamba wenzetu hawataki majimbo sisi wa sehemu hii tunasema si vibaya kama tutapewa jimbo letu kama kile kijiji cha sehemu ya Spain. Hayo ndio maoni yangu. Mwisho kabisa ndio niondoke hizo seconds ambazo zimebaki, ni mahakama za Ki-islam. Tukiangalia vipengele katika kitabu cha sheria za Kenya, ni vipengele vichache tu –, kama hamukukubaliana hakuna ku-appeal. Uki-appeal tunaenda katika mahakama za serikali. Kwa hivyo tunahitaji katika mahakama yakishinda katika ngazi za chini, ile appeal uende katika mahakama za Kiislam, ili Muislamu aweze kuhukumiwa kisheria. Mwisho nasema Katiba inayokuja isiingiliane kabisa na sheria za ki-islam, na mwisho kabisa ma Kadhi wote wawe wanaweza kuchaguliwa na Waislam wenyewe katika jamhuri katika mpangilio ambaye utakuwa umeweza kukaa na kuona kwamba huyu anastahili kuchaguliwa na wale "mascholars" ambao ni wasomi. Kwa hayo mengi nasema nashukuru kwa kuwafungulia kwangu sehemu yangu kwa hivyo nyote karibuni na mutoe maoni bila wasi wasi wala shaka. Asanteni.

**Com. Baraza:** Con Mabavu, ninataka kukuliza swali moja hii ya the type of federalism … ya America iko derived different na Ugerumani from the Canadian one. Which one do you have in mind?

**Con. Mabavu:** Ile nivyo nayo katika kichwa changu ambayo pengine inaweza kuwa created from my mind ni ile ya kwamba kwa mfano, watu wa Pwani waweze wakati tumekubaliana kwamba kila watu waweze kutawala jimbo lao kwa hivyo tuweze sisi watu wa Pwani kwa mfano kuchagua Governor wetu katika hii sehemu yes.

**Com. Baraza:** Na wajua Ugerumani that's what………???

**Con Mabavu**: Yes. Sawa sawa.

**Chief**: Salaama aleykum. Asante. Kwanza na mushukuru Mungu ambaye ametuwezesha kukutana hapa siku ya leo, kwa kuangalia masilahi ya nchi yetu kwa sababu katiba ni masilahi ya nchi kwa hivyo twashukuru. Pili, tunashukuru serikali yenyewe tukufu kwa kubali kwa wananchi wachangie chombo chao wenyewe ili wapate chombo wanacho hitaji.

Kwa hivyo kwanza, ni kianza nasema mfumo wa elimu, urudi kama tulikuwa nayo kuwe na primary education, kuwe na secondary na tuende mpaka kidato cha sita ili tuweze kupata vijana ambao wakiingia shule watakuwa wamekomaa. Lakini kwa sasa hivi kwa vile vijana wanaenda wachanga sana, ndio utakuta kuna rabsha nyingi katika shule zetu, kuna rabsha katika vyuo vyetu vya kitaifa, kwa sababu vijana wanaingia katika vyuo wakiwa bando wachanga. Lakini katika ule utaratibu wakisawa sawa kijana ataingia chuo kikuu akiwa amesoma. Na akiingia hapo atajua kwa nini yuko hapo.

Swala lingine ni ugawanji wa rasilmali. Katika nchi nyingi za ulimwengu sasa kuna matatizo kwa sababu ya rasilmali zake. Kwamba sehemu nyingine rasilimali zake zinafaidisha wenye huko lakini kwengini rasilimali haziwasaidii wale wenyenji. Kwa hivyo kuwe na usawa wa kugawanya rasilmali zao, kila watu wepewe haki za kusimamia rasilimali zao. Zile za kitaifa ziangaliwe zipi za kitaifa, na zipi zinastahili Western, zipi za Eastern, zipi za Coast zifaidishe watu wa Coast, kitu kama hicho.

Chengine ni kuhusu mamlaka tunaona kwamba Kenya kwa sasa tuko na vurumai kubwa kwa sababu vyama vya kisiasa ni vingi sana. Vipunguzwe tuwe na vyama vitano, viatisha kwa sasa vyama ishirini ni vurungu tupu, na hii ni kwa sababu kila mmoja

anataka mamlaka kwa hivyo vyama vya kisiasa vipunguzwe.

**Com. Swazuri:** Na kuna ombi wale ambao wanavuta sigara, kuna watu wanafuta sigara na wanadhuru wengine hapa kwa hivyo kama mtu anafuta sigara tafadhari aende kando akamalize uraibu wake halafu arundi hapa.

**Chief:** Kawaida katika mamlaka ya kikazi kuna mara mbili, kuna mamlaka ambayo yainapitia kwa wananchi, ingine ni ya kisiasa. Na kwa nchi yoyote ni lazima kuwe na mamlaka ya wale watu wanaitwa wa Serikali, hiyo lazima iwe. Kama Chief yaani anastahili kuwa mtu wa serikali, serikali ichukue mahali pake pa kuchagua huyu mtu. Yule ambaye anastahili kuchaguliwa na wananchi basi apewe haki yake. Kwa sababu tukisema kila mmoja achaguliwe na mwananchi haijulikani mtu wa serikali ni yupi na mtu wa wananchi ni yupi. Kwa hivyo lazima kuwe na hiyo tofauti.

Na katika hali hiyo hiyo ndiyo tunasema kwamba mtu akipewe kuhudumia sehemu anayotoka anayohuduimia zaidi kuliko mimi ni toke saa hii nipelekwe Kisumu ?? nitafanya kazi kiuvivu vivu kwa sababu kuko si kwetu lakini kama mimi ni DC atoke katika ile sehemu aliyozaliwa atakuwa anaelewana vizuri mula ya wale watu atakua anajua tabia za wale watu, atakuwa anajua desturi za wale watu, lakini sasa hivi kumekuwa na sifa kwamba wengine ni wavivu wanakaa wangoje maembe yaanguke, na sijui huyo muembe ulipandwa na nani ndiyo saa hii uzae maembe.

Lakini kwa sababu mtu si kwake, hali ya anga pia inatofautiana. Kwa mfano sisi watu wa pwani tunaweza kuitwa wagii lakini si makusudi yetu. Hapa kwetu saa hii ikiwa wakati wa kiangazi tunapambana na jua kutoka saa kumi na mbili asubuhi mpaka kesho za kumi na mibili asubuhi. Maanake mpaka usiku ni joto tupu. Lakini katika sehemu nyingine jua linawaka mchana lakini ikifika usiku lazima ujifunike blanketi. Sasa mtu yule amejifunika blanketi ni kwamba amepata upepo mzuri asubhi akiamka na nguvu zake za kufanya kazi shamabai na sehemu nyinginezo lakini kwa sababu ya hali ya mazingira hiyo haijulikani labda wengine wavivu wengine ni hawafanyi kazi.

**Com. Swazuri:** Dakika moja umalize.

Kwa hivyo nasema kwamba ikiwa kuna njia ya kutumika, katika nchi zilizo endelea na si katika nchi zingine zilizoendelea

hatutaki kuchukua wakoloni kuwaleta tena wa Kenya, lakini hata nchi zingine za Africa tuangalie ni ipi ambayo ina maswala ambayo tunaweza nasi tukaiga kama wakenya na tukawa sawa sawa nao. Kwa mfano Nigeria, ni serikali ambayo nafikiria ni ya majimbo, sasa hata jambo furani hata kuwa watu wapigana wengine kule wanaendelea na shughuli zao. Wengine kule wanazozana wengine kule wanaendelea na shughuli zao, sasa haiwi swala la kitaifa inakuwa ni swara la jimbo linarekebisha makosa yao, wengine wanaendelea na shughuli zao. Kwa hivyo nafikiri mfumo mzuri kwa Kenya pia kwa vizazi vizazi kulinda haki za Kenya kwa vizazi vijazo ninaona serikali inayostahili hapa kwetu, ni ya kugawanya majimbo. Asante.

**Com. Swazuri**: Asante sana. Jiandikishe pale Bw. Mohammed Juma.

**Juma**: Sallam aleykum wabalakati. Nawashukuru sana Macommissioners wetu ambao mmekuja hapa kutaka kusikia maoni yetu. Mimi sina mengi zaidi. Yangu ni mawili. Kitu cha kwanza, nataka majimbo Pwani .

**Com. Baraza:** Tupe jina lako kwanza.

**Juma**: Jina langu ni Mohammed Juma Nzunga. Kitu cha kwanza nataka majimbo. Pili, nataka katiba ile ya majimbo ilitengenezwa Lancaster House 1963 ije ifanye kazi .

**Com. Swazuri:** Mfano wako. Kwa nini wasema hivyo?

**Juma**: Nasema hivyo kwa sababu ile ilikuwa imeondoa wasi wasi wa watu. Serikali ya umoja imeleta vurumari kubwa sana katika Kenya. Katika uajiri wa watu kila jimbo linatakikana 75% ya watu wa hapo jimboni. Na kuhusu mashamba wale vijana ambao hawana mashamba wapewe mashamba kuliko sisi ambayo mtu atakuwa na watoto karibu watano na unategemea shamba moja. Hao vijana lazima waangaliwe sana. Nafikiri hapo mimi sitaki kuendelea zaidi hapo panatosha.

**Com. Swazuri:** Andikisha majina yako pale. Sasa tutamsikiza Amari Matano Keya.

**Matano:** Mimi kwa jina naitwa Amri Matano Keya. Na shukuru kamati ya mageuzi ya katiba na watu wa Diani salaam aleykum. Mimi maoni yangu, nasema katika serikali ijayo nataka serikali ya majimbo. Nataka kila mkoa ujitegemee wenyewe

katika uwajiri wa kazi tunataka asilimia sabini na tano wawe ni wenyeji wa kutoka mahali kunaajiriwa watu, asilimia ishirini na tano iwe ni ya watu wa kutoka nje. Katika upande wa usalama tunataka, walinda usalama wawe ni vijana kutoka mahali walipo, kama ni mkoa wa Pwani wawe ni vijana kutoka Pwani. Katika upande wa jeshi, tunataka kama wanachukua watu mia tano, wahakikishe watagawa wale mia tano kwa mikoa minane. Natunataka katika serikali ijayo elimu, irudishwe kama zamani, iwe elimu ya bure sio kuwa mtu anataka kuenda shule alipiwe admission fee and whatever, hiyo hatuitaki. Tunataka pesa zetu za council zichukuliwe asilimia sabini na tano ziwe zitagharamia mambo ya hapa Pwani mashule, mahospitali and whatever.

**Com. Baraza:** What per cent?

**Matano:** Seventy Five. Na ninataka katika ofisi za ardhi, tunataka wawe ni watu wa kutoka hapa kwetu mkoani sio watu wa kutoka sehemu nyingine, sababu wao ndio wanajua maswala ya watu kutoka hapa kwetu wanajua ni nani anastahili kupewa mahala fulani na ni nani anastahili kupewa mahala fulani. Hatutaki watu wakutoka nje ya jimbo letu.

**Com. Baraza:** Na mkiletewa wazee wa jiji wenyewe si hiyo itakuwa mzuri kuliko huko mambo ya mashamba.

**Matano**: Mambo ya mashamba tunataka wale Macommissioner katika ofisi za serikali wawe ni watu wa kutoka hapa halafu..

**Com. Baraza**: Na tukitoa kwa Macommissioners tuletee wazee wenyewe si hiyo itakuwa mzuri?

**Matano**: Hiyo itakuwa mzuri sana. Lingine, nataka serikali ijayo Rais asipewe uwezo kama vile katiba ya safari hii inasema. Rais apunguziwe uwezo. Na tunataka Bunge lipewe uwezo wa kuvunja vikao vyake vya Bunge. Na tunataka Councillor, Mbunge asiyende kutoa maoni yake tu kwa kichwani tunataka aje achukuwe maoni ya watu wale walimchagua wakampeleka Bunge.

**Com. Baraza**: Kwa hivi sasa hawachukui maoni yenu?

**Matano**: Hawachukui wanaenda tu wenyewe kusema watu wa pwani hawana neno. Na tunataka serikali ijayo kuanzishwe mahakama za Ki-islam. Waislam ama watu wa Pwani wawe wanaenda kwa sheria za Ki-islam sio mahakama za kisasa. Waislam wahukumiwe na kitabu cha mwenyezi Mungu si katika sheria za Kenya.

**Com. Swazuri:** Una dakika moja.

**Matano**: Na tunataka chief – Ma chief wawe ni watu wanaochaguliwa na wananchi wala si ku-appointiwa na Rais. Wala salaam aleykum.

**Com. Swazuri**: Bwana Jefa Martini, Bakari Nasoro awe tayari.

**Martin**: Kwa majina naitwa Martin Jefa Fisi. Asante. Ma-commissioners na Wazee waliofika kusikiza maoni. Mwanzo kabisa ningeomba Katiba inayotayarishwa wakati huu iweze kuwa Katiba ya kimajimbo ili kuwe na ugawaji sawa wa rasilimali. Kwenye Katiba hiyo iwe na mwanzo ambaye unatambua watu wenyewe pamoja na Mungu.

Watu wajiliwe mtu moja kwa kazi moja, sio mtu moja awe na nafasi tatu za kazi. Watu wote waweze kuwa chini ya Katiba hiyo, kusiwe kuna mwingine juu ya Katiba hiyo. Pia kuwe na tume ya kikatiba ya kuchunguza Katiba. Kuwe na tume ya ufisadi na wafisadi waweze kuadhibiwa.

Elimu ya msingi iweze kuwa ya bure. Secondary pamoja na universities ziwe na gharama ndogo. Matibabu yaweze kuwa ya gharama ndogo na mahospitali ziweze kusambazwa mashambani kule watu wanakaa kwa wingi. Kuwe na utaratibu wa kuchunguza bei za vitu (control of price) si kwamba mtu akitengeneza vitu zake anaweza kuweka ile bei anataka, kuwe na control of prices.

Halafu viwanda viweze kufufuliwa. Kwa mfano kama za korosho, meat commission, KCC, ili watu waweze kuajiriwa na wapate kazi. Pia uwajiri uweze kulingana na elimu ya mtu, si kwamba kwa sababu kuna mkumbwa fulani mtu fulani anawekwa pale ofisi. Uwajiri uweze kuangaliwa kulingana na elimu ya mtu yule anaye ajiriwa. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana, andika jina lako pale. Bwana Bakari Nasoro.

**Bakari**: Arabic greetings. Jina kamili naitwa Bakari Nasoro Mguta. Ningetaka serikali ijayo iwe ya majimbo. Na jimbo hilo

liwe na uwezo kama vile ulivyokuwa mwaka wa sitini na tatu. Kwa upande wa ardhi lazima jimbo liwe linaachiwa mamlaka yote ya ardhi yake. Mamlaka ya Rais yawe yatapunguzwa kidogo na nchi hii iwe na waziri mkuu. Na nyumba za kutunga sheria ziwe nyumba tatu.

Hapa kwenye jimbo kuwe na Regional Assembly, kuwe na bunge la sasa hilo, halafu kuwe na nyumba moja ambayo ni ya juu zaidi, iwe ni ya wazee kutafutwa kila constituency kama hii msambweni pengine iwe na mtu wake mmoja, au ichanganywe na kinango na awe si mgeni wa kuja. Mtu huyu anatakiwa wa kabila ya hapo. Kwa mfano Kinango na Msabweni inajulikana wao ni makabila wawili, ikiwa kunatakikana mtu mmoja watu wawili hao wanaweza kusimamishwa wakapiga kura atakapochaguliwa ndiyo aende kule upper house.

Cheo cha chief Kadhi, awe ni mwenye kuchaguliwa na wasomi wa Ki-islam, si achaguliwe na serikali, hapana. Achaguliwe na wasomi wa Ki-islam. Na chief Kadhi huyu awe na mamlaka sawa na Judge, sio Hakimu – Judge hao wadogo zake huko mikoani ndiyo watakuwa kama mahakimu yaani Muislam akipeleka kesi yake ikishindwa kwa hakimu atapelekwa kwa judge, ikiwa hakuna judge atapelekwa wapi?

Kazi, kiwanda kikianzishwa hapa kiwe watu wa Pwani watapata asilimia sabini na tano na watu wakutoka nje ishirini na tano. Lakini sabini na tano hawa wasiwe ni watu wa kuja wawe ni wenyenji wa hapo mahala pa kuwekwa kiwanda hicho. Hata ikiwa kwa mfano mimi nimeondoka hapa nimekwenda Murang’a huko, niishi miaka kumi, lakini wenyewe wanataka kuweka kampuni nyingine huko, siwezi uwe sheria hainiruhusu kupigania nafasi. Ikiwa nataka nje hapa kwetu nipambanie hiyo ishirini na tano lakini hii sabini na tano, niwachie wenyewe wa Murang’a.

Polisi. Polisi wakimekwa, kwa mfano kituo chetu kama Diani hivi kusiwe na watu kutoka nje. Lazima ma-officer hao watakakuwa hapo wawe ni watu wa Coast.

**Com. Baraza:** Kwa nini?

**Bakari:** Sababu wale watu kutoka nj, wakija wanafanya masilaha ya watu hawa na wafanyi masilaha ya kazi.

**Com. Njoroge**: Kwa hivyo hii kuajiliwa tunasema watu wakae katika jimbo lao?

**Bakari:** Ukiajiriwa huko ukija hapa utafanya kazi bila wasi wasi, lakini si hiyo nafasi ya hawa wapokonywe tena na wewe uingie sasa, itakuwa huko ishirini na tano ishaa chukuliwa na hapa ushawanyang'anya haki yao.

**Com. Njoroge**: Kwa hivyo unasema kama ni mwenyenji na amekaa hata kama miaka kumi hana haki ya kuajiriwa kazi. Kwa hivyo unasema hawa watu ni lazima waondoke waende wakaajiliwe kazi katika jimbo lao?

**Bakari:** Hao waliokwisha ajiriwa watakaa mpaka wata retire. Mimi vile unaniona nimefanya kazi nanime retire. Nishakuja sasa ile nafasi kampuni ina haki ya kumrundisha mwenyewe wa hapo, lakini sio kusema hivyo na unapeleka mtoto wangu unapeleka mtoto wa shangazi na zote tumefanya kuja hapa hiyo ni kuwazuia hao wenyeji.

**Com. Baraza:** Wacha nikulize swali hii mambo ya uwajili, mkiwa na industry yenu hapa halafu labda experts (unajua experts) nikisema experts – watalaamu. Ikiwa mtalaamu hatujatoa wetu hapa Msambweni kwa sababu hakuna mtaalamu wa hiyo industry, sasa tutafanya aje hapo? Tukitoa mtaalamu kutoka Western aje watengeneze vizuri mpate pesa 75% ibakie hapa hiyo itakuwa vibaya? Sisemi kwamba watu wa Msambweni sio wataalamu, tunaweza kuwa na hiyo sugar unajua hiyo Mumias Sugar, Western wanatoa Wataalamu kwingine hata watu wa Coast wako huko nani wataalamu na wanatufanyia sukari yetu tunauza, mapato inapatikana kwa hivyo itakuwa na shinda gani?

**Bakari**: Mtu mmoja hakuzuia ile ishirini na tano itaingia nafasi ya wale ishirini na tano.

**Com. Baraza:** Mutaalamu atakuwa kwa sukari na huyu wa kuweka miwa awe wa hapa Okey sawa.

**Com. Swazuri**: Asante sana mzee. (the rest is inaudible)

**Mohammed**: Arabic greetings. Namshukuru Mwenyezi Mungu (Arabic). Kwanza ambaye ndiye alituumba sisi zote tulio hapa na vile vile akawapa vyeo baadhi yetu. Wengine ni wakubwa wengine ni wadogo. Akawafadhilisha wengine juu ya elimu wakawa na elimu kubwa wengine ndogo. Kwa hivyo na mshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake huo, na pia na shukuru hao aliowapa elimu hiyo waliotujia mbele yetu hapa, kuchukua maoni yetu kuhusu nchi yetu hii. Pia mimi mwenyewe kwamba

ni Asmani Mohammed Higa namshukuru kupata nafasi hii ya kutoa maoni yangu hata kama ni machache. Na pia nawaomba wakubwa, na raia wenzangu kunisamehe nitakaposema neno la kosa.

**(interjection:Com. Zwazuri**: Sema maoni yako, kila mtu yuko huru kusema bora usitukane)

Mohammed: Maoni yangu kwanza naomba serikali inayokuja iwe ni serikali ya majimbo. Pili, nataka serikali inayokuja iwape waislam uhuru wa ndini yao. Tatu, nataka serikali inayo kuja iwape waislam mahakama zao, za mwanzo mpaka Mwisho, ziwe kesi za wailama zinamalizwa na waislam wenyewe. Pia nataaka serikali inayokuja, itoe elimu za bule kwa raia wake wote na katika elimu hizo hizo, ikiwa ni skuli iwe na elimu za ki-islam vile vile. Waislam wapate nafasi ya kusomesha watoto wao katika ndini mbili humo humo na katika skuli moja.

Upande wa uchumi, nataka serikali inayokuja, kila jimbo liwe na uwezo wa kujisimamia mambo yake yote. Pia, nataka serikali inayokuja, katika jimbo hilo la mkoa wa Pwani iwe na university zake. Pia katika serikali inayokuja, ikiwa universities ziko pia skuli za watalii ziwe ziko Pwani vile vile. Kwa upande wa kitambulisho, naomba pia serikali linayokuja iwe kila jimbo linaweza kuandikisha watu wake kumalizia mambo yake yote pale sababu hii wakati huu tunapata shida kupewa lakini kuna wengine kupata jina na kubadilisha jina ni shida kubwa, itamaliza karibu miaka tatu hujabadilishiwa. Pia, ningeomba kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho ni Koran takatifu wondolewe katika mahakama ambazo si Ki-islam.

**Com. Baraza**: Ifanye nini?

**Mohammed**: Iyondolewe katika mahakama.

**Com. Swazuri**: watu wasiapishwe kutumia Koran?

**Com. Baraza**: Na wasiapishwe na nini? (inaudible)

**Mohammed**: Na neno. Mimi sitakuwa na maneno marefu sana ndugu zangu Waislam kwa hayo na shukuru lakini nataka serikali ya majimbo.

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Choka**: Asante sana, Macommissioners wa Katiba asante sana. Kwa jina langu naitwa Osmani Omari Choka. Mufumo wangu wa serikali inayo kuju, naomba serikali iwe ni ya kimajimbo. Elimu. Elimu yetu kuanzia std. One mpaka std 7 or 8 iwe inakuja bure kama vile awali ilivyo anza.

Ulinzi: ulinzi umekuwa si ulinzi wa maana ni ulinzi wa kula hongo tunaomba ulinzi kama huu serikali ijayo iwe sio hivyo.

Utalii. Utalii wote katika nchi ya Kenya, wote wao katika Coast Province. Nataka mamlaka ya utalii yote mamlaka yawe katika jimbo la Pwani.

**Choka**: Tuondoe hongo na tuondoe pesa. Asilimia yetu sabini iwe Coast.

**Com. Baraza**: Au upite mlango wa mbele ununue dawa.

**Choka**: Upitie mlango wa mbele ununue dawa, hayo ni mambo mengine.

**Com. Baraza**: Ni nini umesema?

**Choka**: Mimi nasema hivi serikali inayokuja dawa ziwe mahospitalini ziwe nyingi na ziwe zinahudumia wananchi bure.
Ulinzi: Ulinzi Kenya hauko imara tunaomba ulinzi katika Coast Province, katika hii jimbo letu. Commissioner awe mtu wa Coast. Wakubwa wote katika hii serikali ya majimbo wawe wenyewe wanajiendleza wenyewe. Upande wa ….. yamekwisha hayo. Asante sana.

Com. Swazuri: (inaudible)

**Osman:** Saalama aleykum. Kwa jina naitwa Osman Riziki Kassim. Na shukuru kukutana na Tume ya Katiba na maoni yangu nikianza na swala la kilimo, kwa sababu sana tunaambiwa watu wa Pwani especially Kwale ni wavivu. Na ule uvivu hatu uoni. Ni hivi kitu cha kwanza ningeomba Tume ya Katiba - Title deed zilizoko zote ni-fake sifutiliwe mbali. Serikali hiyo inayokuja jimbo letu tunalolitaka sasa litatengeneza title deeds mpya kufanyiwe upimaji tena mwingine wa ardhi. Swala lingine kwamba kuhusu upande wa kilimo kuna mikopo mingi sana huja kutoka nchi za nje, lakini watu wa Coast hawapati za pelekwa kule

mbara tunapata ma-tractor yako kule hapa hatuna hata tractor moja hivi sasa katika Kwale hakuna tractor hatamoja ya serikali na tukienda Rift Valley tunapata ma-tractor yako kule kama zile combined harvesters zinafanya kazi kule, hapa hatuna hata ile ndogo, ile hamna.

Kwa hivyo sisi tunataka serikali ile inakuja ya majimbo, tujitawale wenyewe tupange maswala kama yale. Na kuhusu lile swala la kiafya, kama alivyosema mwenzangu. Mambo ya mlango wa nyuma hatutaki, tunataka mkuu wa afya katika Pwani awe mwana Pwani , kama ilivyo sasa Coast General Hospital yule mama aliye pale. Tunataka tupate zaidi ya yule. Mambo ya back door yatapotea.

Waislam tumerudishwa tumewekwa nyuma tunaonekana sisi hatuna maana na hatuna maana kubwa sana. Leo hii unapata siku ya jumapili na jumamosi ikifungua radio kutgoka asubuhi mpaka saa atano za usiku jina la Bwana, jina la Bwana huwezi kusikia tumepewa vipindi vidogo siku ya ijumaa ya Waislam. Kwa hivyo tunataka kama ni ile siku ya ijumaa kwanzia saa nne za asubuhi mpaka usiku wote Waislam wapatiwe nafasi na hayo maswala yao yasikike kwenye ma-radio na mateleviseni.

**Com. Baraza**: Na tukitoa jina la Bwana liwe haisikiki kama Waislam sasa tuwe sawa si hiyo itakuwa muhimu?

**Osman:** Haja yetu twataka dini iende mbele, ndini yetu iende mbele isikike sasa tukiondoa hiyo sasa tutaishi kipagani. Swala lingine ni kwamba ma-Kadhi wetu sio Chief Kadhi peke yake Makadhi wetu wapewe, kipao mbele wawe na heshima kama vile ma-Judge wengine. Swala lingine ni kuhusu mambo ya kazi kama walivyosema wenzangu waliotangulia wanataka 75% iwe hivyo, iwe hivyo ukweli na tuangalie sisi tuna vijana wengi ambao wana ujuzi kama walivyosema mama mwanzo ya kwamba kama twaweza letewa mtalaamu. Tunao wataalam hapa lakini saa watalaam wale imekuwa utalaamu wao hauna maana, umefichwa tunaletewa mtu kutoka kule tunaambia ni mtaalamu tukija naye hapa nikiwekwa mimi na yeye pamoja ile kazi yake inakuwa wasi wasi ile yangu inakuwa nzuri lakini nimedharauliwa kwa vile nimetoka wapi – Coast especially Kwale. Tunaambiwa sisi kazi yetu kuwangalia Wajerumani.

Swala lingine, ni kuhusu mambo ya ulinzi. Vijana wananyanyaswa ufuoni hapa ma saa yananzia Chale mpaka Tiwi hakuna Polisi yoyote ana mu-harass lakini kijana wa kidigo ama wa Kigiriama ama wa Kiduruma akitembea kule ufuoni hawezi enda mita mia

mbili atapelekwa  Kwale.  Akifika pale shilingi elfu moja (**clapping**) huo ni unyanyasaji.

Swala lingine ni kuhusu mitihani tunayoifanya kila wakati, kila mwaka watoto wa Pwani  especially Keale wame-fail, wame-fail na tukiangalia  hawa watoto na tukiwafanyia mitihani yetu manyumbani ni wazuri tena wengine ni ma-genious.  Lakini sisi tumeshangaa wame-fail vipi kwa hivyo tunataka pia pale pale pawe na watu wa Pwani ambao kama vile tutapata Bw. Mohammed, muwe pale muangalie yale maswala Bwana, tunanyanyashwa watoto ….. (interjection).

**Com. Swazuri**:  Bw. Juma ni mkubwa wa mitihani  (inaudible)

**Osman**:  ah……. Amezungukwa akawekwa kwapani eh, watoto wanapita wakishapita jina linageuzwa anapewa mtu kutoka Turkana kule.  Mimi nimefika Turkana na Mturkana mpaka apewe sukari aende skuli sisi tunaenda wenyewe kwa hiari yetu, kwa nini tuna fail?  Kwa hivyo hayo ni maswala sisi tunataka tuangalie hayo.  Halafu kitu kingine, ni kwamba tangu serikali hii ilipoaza mpaka leo, Rift Valley province kuna vyuo vitatu sasa vya elimu.  Kuna university tatu, Nairobi, lakini Coast angalia Mombasa polytechnic ukienda pale kijana wa Coast haipati ngoo!  Mimi nimejaribu pia ku-apply Mombasa polytechnic mpaka mwisho nika surrender, sipati.

**Com. Baraza:**  Walikwambia aje?

**Osman:**  Na takikana nitoe kitu kidogo na sina.  Nitafanya nini.  Mimi sijapata nitatoa wapi?

**Com. Swazuri:** Asante sana kwa maoni yako nzuri.  Huyo alikuwa ni Osman sasa tuko na mzee Ali.

**Ali:**  Arabic greeting.  Nashukuru sana wakubwa wetu walio kuja hapa kuchangia Katiba yetu na kusikia maoni yetu. Tunashukuru sana  kwa watu wetu kuja hapa maoni ya wananchi hapa kila mtu atoe maoni yake sawa sawa.  Mimi nataka serikali ijayo iwe ya majimbo. Tujitawale wenyewe, tujifanyie mambo yetu sisi wenyewe – ninavyotaka namna hiyo.  Na katika Pwani yetu isiwekwe maboya watu kukatazwa  kwenda kuvua, tuwe na uhuru wa kuvua kila kitu wenyewe tutavua. (interjection: inadible) Nataka tujifanyie  wenyewe kazi zetu sawa sawa tusinyanyaswe hapa Pwani.  Mimi sina zaidi. Nimemaliza.

**Com. Njoroge:** Asante sana uende pale mzee uandike majina yako. Adam, unafuatana na Mohammed (inaudible – tape has low sound)

**Adam**: Mimi nitasoma memorandam ya UDC kwa kusimama kwa haraka haraka UDC ni Ukuka Development Committee. (interjection: inaudible) Kwa kutambulisha ni nini UDC, ni kamati ya maendeleo ya kata ndogo iliyoko kata ya Diani wirayani Kwale. Kamati hii pia ni sauti inayo hamasisha wakaazi wa kata ndogo ya Ukunda, ama Diani, katika nyanja mbali za maendeleo kama ukulima, elimu afya, na hata kufahamisha jamii juu ya haki zao katika nchi hii ya Kenya. Kuhusu marekebisho ya katiba, UDC umelazimika kwa niamba yajamii nzima kwa jumla kuchangia mabadiliko ya Katiba kwa sababu katiba iliyoko sasa, inetuadhiri sana sisi wakaazi wa mambao wa Pwani kwa jumla. Kwa nini tunataka Katiba ibadilishwe? UDC inakubaliwa na Wakenya wengi wenye fikira kwamba Katiba iliyoko sasa ambayo imerekebishwa mara thelathini na nane ni mbaya.

**Com. Njoroge**: Kwa nini huwezi kutupatia mapendekezo….

**Com. Swazuri**: Kupatie mapendekezo uliona ni mbaya sasa tufanye nini hiyo ndiyo tunataka tunaenda kusoma hiyo ingine.

**Adam**: Mapendekezo yetu ni hali za matatizo nyeti yanayotukumba kama elimu mambo ya ardhi, uchumi utawala wa mikoa na usalama. Kwa hivyo mapendekezo yetu ya Katiba tuitakayo UDC kwa niamba ya wengine wote nataka Katiba ibadirishwe ili iwe na uwezo wa kuamua kwamba sera za serikali zirudishwe kwa wananchi kuliko kubaki kwa watawala ambao ni watumishi wa uma.

Katiba tuitakayo ni Katiba ambayo italeta utawala au serikali ya majimbo, ili kila jimbo liweze kuamua na kusimamia maendeleo yake. Kila jimbo liweze kutabua matatizo ya jimbo lingine. Neema za kila jimbo ziweze kuwa neemesha jamii ya jimbo hilo kwanza na Kenya kwa jumla.

Haki na rasilmali za kila mtu aliyechagua kuishi katika jimbo lolote ziweze kulindwa. Dini, mila na desturi ziweze kulindwa kisheria katika majimbo yanayo husika. Memorandum hii imetayarishwa na ku-signiwa kwa niamba ya Ukunda Development Committee na wafuato. Zaidi Edward – Chairman; Juma Mboga- Organizer na mimi mwenyewe kama Secretary.

**Com. Swazuri**: Asante sana kwa hiyo memorandum tuatenda tusome neno baada ya neno.

**Mohammed**: Salaam aleykum. Na shukuru sana waheshimiwa kwa kupata nafasi hii. Mimi nina mambo manane. Jambo la mwanzo, serikali itakayokuja, twataka ile parliamentary system. Rais awe Mbunge akiwakilisha jimbo lake. Rais awe anachagua waziri mkuu. Rais awe mkuu wa nchi. Rais awe anaiunda serikali na iwapo serikali itakuwa haina msimamo mzuri aivunje. Rais ashughulikie sherehe za kimataifa. Waziri mkuu aunde baraza la mawaziri na kuendesha shughuli za kiserikali.

Majimbo. Mfumo ni ule ule wa Lancaster House tuwe na mabaraza mawili lower house na upper house. Jimbo liwe na uwezo kamili kwa kujimiliki. Katiba. Katiba ni ile ile ya vyama vingi kama uliyokuwa KANU, KADU na vyama vingenvyo katika majimbo.

**Com. Swazuri**: Ni ngapi ………….. (inaudible) number yake?

**Mohammed**: ah ah Mwambao wa Pwani tuupate sisi wenyewe wa Pwani, kama tulivyo upata wakati wa ukoloni na Muarabu walipokubaliana kutoka wenyewe.

Ardhi: Mtu aliyepata ardhi kutoka kwa babu na mababu zake halafu kuja mtu mwengine kumondoa katika ardhi hiyo, hiyo ni dhuluma na mbinu za ukabila.

Com. Swazuri: Sasa tufanye je?

**Mohammed**: Tumwachie yule, yule aliyepata mapato kutoka kwa warithi wake, kwa sababu kuna watu wengine huja wakitokea wakisema hii ni ardhi ilikuwa ya mtu wangu huo ni ukabila na ubepari. Neno kupewa ardhi, kupewa ardhi, neno kupewa ardhi, aliyepewa ardhi halafu kupata kibali, kibali hicho kifutwe kwani si cha halali. Nitafafanua hapo. Kuna ardhi zimechukuliwa kutoka kwa wanyonge na kupewa wakumbwa. Halafu mkumba yule tayari amepewa kibali hiyo ni dhuluma. Kibali hicho kifutwe. Kununua: Nikisema kununua ni kununua ardhi. Kuna watu wanauziwa ardhi kimakosa ananyang'anywa mtu halafu haraka inauziwa. Tayari yule mtu anapewa kibali, huo ni unyang'anyi na ndiyo maana hapa Diani location, vita vikubwa ni mashamba kwa namna hiyo.

**Com. Njoroge**: Ule ambaye imeuzwa ka ajili ya kupokonya mtu haki yake unasema ifanywe nini au ikae hivyo hivyo?

**Mohammed**: Ile ifutiliwe mbali. Arudishiwe yule yule mwenywe. Tunaenda kwa ajira. Ajira zetu hapa Pwani, hasa Kwale ajira za Kwale zina matusi makumbwa sana. Kuna wake zetu waliosoma. Punde anaposikia kuna nafasi kwa kiwanda fulani mtu yule ama bibi yule hawezi kuajiriwa, ama msichana yule hawezi kuajiriwa mpaka aonane na boss aonane kimwili. Baada ya kuonana kimwili ndiyo hapo sasa anaajiriwa kazi. Hiyo si sheria hiyo si sheria.

Utawala. Utawala ukumbusho wetu tunaotaka ni ule wa mwambao wa Pwani kwenye makataba ulivyo tekeleshwa kama uliyo kuwa hapo awali. Sera ya utawala ni ile ile iliyo leta uhuru kutoka Lancaster. Mwisho twataka majimbo Mwambao wa Pwani tupate. Na shukuru.

**Com. Swazuri:** inaudible.

**Rashid (Kidigo vernacular using an interpreter):** (Kidigo greetings) Eh swali langu Katiba. (**Interjection: Com. Baraza**: Mzee sema jina lako hapo.) Jina langu naitwa Iddi Rashid Mwavumbai kutoka Galuikinoi? Jambo lingine nasema hivi nchi hii mtawala ni Kubo aliye pigana na Mbaruk akamuondoa akapelekwa Gogo la Mboto akachukuliwa na Mgerumani akapekekwa huko, hapa tukatwala wenyewe. Halafu akaitwa Said Mbaragash kutoka Zanzibar akapewa maili kumi akae kule baharini amuangalie adui yoyote ajae. Aje atoe report kwa mzee Kubo. Kutawala kwake ataka jimbo lake hakutawalwa, alikuwa na bendera yake na kitambaa chake cha red (**clapping)** munaiona bendera hii basi nitaivaa.

Iliondolewa na Kenyatta, uliondolewa na Kenyatta, alipokuja hapa alisema watu washirikiane wawe Africa moja. Tuliposhirikiana tuliangushana na Mbaniani, halafu mwenzetu akageuka kule akawa mau mau, halafu akashikwa akafungwa Lodwar. Halafu watu wakaenda Cairo, wakaambiwa waunde Serikali, KANU akakataa. KADU ikaunda, serikali ikaenda kufungua Kenyatta. Alipokuja nyumbani akauliza, je, mimi nimefunguliwa na KADU niingie chama gani? AkaaMbiwa aingie KANU ndiyo chama chetu. Aliyesema hivyo ambaye ni Gichuru. Ndiyo chama changu ni KANU. **(interjection: in vernacular).**

Mimi nataka na majimbo neno lingine ni ardhi, haiuzwi. Ambaye amenunua ardhi aondoke aende nayo kule anakotaka lakini hakuna ardhi ya kuuzwa, ardhi hufanya kukodishwa akimaliza miaka yake aondoke. Ndiyo sababu kitambulisho twataka ya Mijikenda sio cha Kenya. Kenya ni huko mpaka Mtito Ndei (**clapping)** ndiyo mpaka wetu. Ukiutia Kenya ukileta na huku ndiyo wamgandamiza mzee haiwezekani. La. Swali langu, Mijikenda mfungwa mzee Kenyatta kumleta hapa kwa jina la Africa, na Africa hakuna sasa ni wazungu watupu. Wa-africa wako wapi sasa hebu niambieni? Mimi nataka Waafrika warudi hapa. Bunge la hapa kuwe, Kidigo ya kusizitisa ...

**Com:** (inadible)

**Edward:** Majina yangu kamili naitwa Said Edward Zaro. Mimi ni mzaliwa wa Pwani na ni mwanabiashara na pia ni chairman wa kamati ya maendeleo ya hapa Ukunda sub-location. Huu ni utangulizi na mapendekezo yetu wa Pwani tunataka majimbo, majimbo hasa yale yaliyopatikana mwanzo wa uhuru. Katiba ya majimbo ni Katiba ya haki na Katiba hii ya sasa ni Katiba iliyotungwa tu na watu wachache. Kwa hivyo tuna shukuru hii commission, sasa tunataka kutengeneza hiyo katiba na ni Katiba tunaiyounda ya majimbo. Kwa hiyo commission ichukulie jambo la muhimu kuwa watu wa Pwani wanataka majimbo. Yote haya yameletwa kwa sababu ya matatizo mengi yanayotukumba hapa.

Kwanza tunaingilia swala la ardhi. Sababu nyingi tunataka mageuzo haya ya katiba ni sababu ya ardhi, na mengineyo ambayo nitataja lakini kila kifungu nitaeleza kabla sijaingina kingine. Swala la ardhi lina tupeleka sana kwanza tutasema ndiyo lana ya kwanza katika hapa mkoa wa Pwani. Na sisemi majimbo haya ni ya kufukuzana, la. Kwa sababu tuna pokuwa wengi ndipo hapo tunapeana mawazo tukajenga nchi.

**Com. Swazuri:** Sasa ardhi unatakaje, tupaties mapendekezo.

Ardhi: Mashamba iliyonyakuliwa yarudishwe kwa wenyewe. (interjection Com. Swazuri: inaudible) Kilichonunuliwa ni haki, kilicho nyakuliwa kilegezwe kwa wenyewe. Halafu mashamba yaliyokodishwa kama vile kiwanda cha sukari cha Ramisi pia kiregeshwe kwa wenyewe kama vile Tiwi na nyinginezo zina jilikana. Na ugawaji wa mashamba na utoaji wa haki za kumiliki

mashamba ziachiwe serikali ya mashinani. Haya na sehemu nyingine tofauti, takatifu ziachiwe jamii yenyewe wazihifadhi nakuzilinda. Yule alieyena haki ya kumiliki mashamba awe atamiliki rasilimali zote zilizoko kwenye shamba hilo pamoja na madini ama mafuta yake.

Ukulima: Ukulima tunapenda tuachiwe kama serikali yetu tumepata majimbo, tuachiwe tuamue wenyewe na tutafute masoko wenyewe kuliko mazao yetu yatafutiwe huko baraama na serikali iliyoko sasa. Na pia tukipata majimbo itakuwa rahisi kuregesha ama kufufua miradi yetu yote iliyo achwa kiholela ili tuzoroteke hapa Pwani.

Kuhusu elimu, mkoa wa Pwani ndiyo wa kwanza kuelemika. Mkoloni alipokuja hapa alipitia huku Pwani, na mpaka sasa tukitazama upande wa elimu umezoroteka na si kwa sababu hakuna wasomi. Wasomi wako chungu nzima lakini huwa tatizo tu, wame-pass, utasikia Kenya waliofanya mtihani kidato cha secondary. Ni watu kama elfu mbili na wanataka kuenda university. Hao watu elfu mbili baada ya wiki mbili utakuta wamechujiwa mpaka wa Pwani ndiyo wanachwa kupata hizo nafasi. Wana qualification za kuenda university lakini waachwa kwa sababu wanapopata hizo nyathifa, wataendeleza Pwani yao. Kwa hivyo ningependekeza tupate university zetu huku ili tunapohusisha watoto wetu watachaguliwa huku hatutakataza wengine, lakini wengi watatoka huku huku.

Serikali ya mikoa: Serikali ya mikoa iliyoko sasa haitufai, kwa sababu tunapendelea ma DC, PC, DO, ma-Chief wachaguliwe na wananchi wenyewe, na wawe wanatoka sehemu zao kwa sababu tunashukuru mpaka sasa kama tungepata aina ya machief tulionao sasa wote wanatoka hapa hapa. Na sub-chief anatoka hapa hapa, na ma-chairman wetu wote wanatoka hapa hapa. Maendeleo yake kweli ni mazuri kuliko yale ya DO, ya DC, ya PC na yote inaletwa kwa sababu si mzalendo halisi wa hapa, na kama angekuwa mzalendo wa hapa, basi naona pia tungendelea. Kwa hiyo tunapenda serikali za mikoa tuachiwe wenyewe tuamue na tuchaguwe wenyewe.

Kwa kumalizia nitasema katiba tunayotaka ni Majimbo. Tena tunataka majimbo ya kisawa sawa. Majimbo ambayo tutafanya tuwe na Katiba yetu na Katiba hiyo iwe italinda masilahi yote kama vile dini halafu na mila zetu ziwe zitalindwa. Sina mengi asanteni na tunaomba ya chukuliwe maanani na mwenyezi Mungu atubariki tupate majimbo yetu. Asanteni (**clapping**).

**Com. Swazuri:** Asante sasa atafuatwa na Rajid Matoyo, ako tayari?

**Sheikh**: Arabic greetings. Mimi na shukuru kwanza kwa kupata hii nafasi.

**Com. Swazuri**: Sema jina lako.

**Sheikh**: Sheikh Saidi Mwanyota. Mimi kile nataka kwanza kwa memorandum ni majimbo. Sababu inayotaka nipende majimbo ni kwamba katika huku kwetu tumezoroteshwa sana kimaendeleo, na pia tunanyanyashwa. Kwa sababu katika hali ya maendeleo ya ukulima tunanyanyashwa. Mtu atakuwa ameanzisha ardhi miaka nenda ama ameirithi kutoka kwa mabubu zake, lakini hapo hapo katikati patakuja paingie kipengele kwamba mpaka uwe una title deed na huyu anayekwambia hivyo ni mtu kutoka nyanda za juu na ikiwa utakosa hiyo title deed niyeye atamiliki hiyo ardhi na haijui mwanzo wake ulianzia wapi wala ulimalizikia wapi.

Kwa hivyo hilo neno kwanza nalipigania liwe litaondolewa. Halafu pili ni kwamba nataka majimbo kwa sababu tumezoloteshwa kimaendeleo. Sisi huku Pwani mazao yetu ni nazi, korosho, maembe na tulikuwa tunayo mtambo wa koroso hivi sasa hakuna umefungwa. Kwa hivyo imekuwa mazao yetu hata tunapoipata hayana dhamani yoyote

Tatu, minazi ni mazao yetu makubwa lakini utakuta meli imeoagizwa ya mafuta ya nazi kutoka ng'ambo yaletwa hapa yawe yatasambazwa kwenye maduka. Hali ya kuwa nazi zimejazana mpaka utakuta sasa hazina dhamani yoyote, na hali ya kuwa ndiyo mazao makuu ya kutegemewa katika mkoa huu wetu. Halafu ni maembe hali kadhalika, lakini ukiangalia nyanda za juu kumbe ikiwa zao lao kubwa ni kahawa liko na themani mpaka ng'ambo. Majani chai hivyo hivyo. Na mapalreto hivyo hivyo, sasa inaonekana hii serikali tulionayo hivi sasa haipendelei mkoa wa Pwani, bali wapendelea nyanda za juu (**clapping)** kwa hivyo tunataka tuwe tunajitegemea kwa njia kama hiyo.

Jambo jengine ni kuhusiana na elimu kama walivyozungumza wenzangu, kuanzia darasa la kwanza mpka la nane tunataka hii elimu iwe ya bure. Pia tupate vyuo vyetu vikuu hapa hapa mkoa wa Pwani ili nasi tujivunie. Ikiwa watoto wetu watakuwa wemepita katika masecondary watakuwa wanaenda hapa hapa kuliko kuwa mpaka waende Kaimosi huko na hali ya nauli itakuwa hakuna ya kumpeleka huko. Kwa hivyo hilo ni jambo jengine muhimu na pia nataka litiliwe mkazo lipatikane katika hapa mkoa wa Pwani. Nimemaliza. Asanteni.

**Com. Swazuri**: Rajab atajuatwa na Mohammed Bakari.

**Rajab:** Mimi jina langu ni Rajab Mwazoyo. Maoni yangu mimi nazungumzia kuhusu ardhi, kwamba hali ya ardhi hapa imekuwa na utatanishi wa hali ya juu sana. Ardhi inauzwa au zinauzwa bila mapatano na wenye kusimamia ununuzi ama wauzaji hawaangalii sababu ya kuuza, nyuma ana nani na nani, wala anauza kwa shida gani. Kwa hali hiyo naona hiyo hali hairidhishi.

Lingine ni kuhusu upande wa elimu ya kidini. Mfumo uliokuwako mbeleni tuliweza kupata mfumo kwamba dini ulikuwa imependekezwa ipate uzaidizi wa hali zote kimisaada kama elimu zengine. Ajabu ni kwamba mpaka sasa wazo hilo lilikanyangwa. Hii dini yetu inategemea sisi wenyewe kuendelezwa watoto wetu kiasi ya kwamba sisi uwezo hatuna heli ya kuwa misaada ilikuwa imepitishwa kwamba lazima dini hii isimamiwe na ipate misaada kama dini zingine.

Lingine na msahafu kuweko kwenye kijukwa pale katika hali ya kuapishwa. Hali ile hairidhishi kwa sababu si wote wajuao usafi wa msahafu kushikwa.

Lingine ni kusudia koti wakati mtu ameingia pale, hilo jambo lina matatizo, anaye sujudiwa ni Mwenyezi Mungu. Itakuwa vigumu kwamba ukiiruka ama ukiingia mpaka usujudu.

Jambo jengine ni kuhusu ni afya. Hali ya kutibiwa watu wanapata dhiki sana vyombo viko vya kutumiwa lakini lazima ukiwa na magonjwa unatatizwa kwamba ni lazima ununue kitu kile unanunua unaelezwa tu mahali kuna kibanda cha mchungwa unaambiwa uende ununue ‘pipe’ ya shindano. Kama serikali ina shindwa kuweka, kile kibanda kinawezaje aje kuweka kitu kama hicho. Hilo ni jambo unatatiza sana. Lazima tupate matibabu yalio vyombo vinpatikana katika hospitali, sio kwama tukanunue nje tena utoe damu na mpaka uinunue.

Tena hali ya muhuduma. Unapoku wa na mgonjwa pale ni lazima uende uambiwe umsimamie kiasi ya kwamba kuna watu wameajiliwa kufanya kazi hiyo na uende ulale chini mgonjwa akikojoa ni wewe na mengineo. Yule aliyeajiriwa kazi yake ni nani alipwa na mimi silipwi. Hilo ni tatizo moja ambalo lina tukumba. Kwa hali hiyo tunataka serikali ibadilishe sherikali itakayo kuja

mambo kamahayo.

Na mwambao tunautaka na majimbo pamoja. Majimbo yaliyo na uwezo wa kumiliki mambo yote ki vita, ki nini. Swala la nchi majimbo haya ya simame pamoja kuletwa. Lakini mengineo jimbo liwe lina simamia. Kwa hayo machache asanteni (**clapping** ).

**Com.** (not audible)

**Mzee**: Salaam aleykum.**(This is an interpreted Digo vernacular)** Mimi tatizo langu mwaka arubaini na saba walichangisha shilingi moja moja kutoka Ngombeni mpaka Vanga, wahipauliza pesa hizo, waliambiwa ni za serikali yenu ya wananchi na serikali hiyo ilikuwa County Council. Je nauliza hivi sasa huyo manager yuko hapo County Council ni mtoto wa Kidigo nani? Mbona haifai kitu ikiwa Mishi waraka ndiye yuko hapo? Nataka ajulikane kabisa iwe Manager ni Mdigo, mtoto wetu, na hiyo hiyo County Council sio kutenga viwanda vyao. Kama hapa walitenga hapa wenyewe lakini wakitanabai wawetu wakakuta pahali hapo pamegawanywa vipande vipande, pameuzwa na matajiri, wakiuliza hawa julikani na hiyo hiyo county council inatutia hasara. Twataka mtu wa kisawa sawa. Nina maneno mengi lakini nataka majimbo. Shukurani.

**Com. Swazuri**: Bw. Abdala Mboga, atafuatiliwa na Rasid Kando awe tayari.

**Abdala**: Salaam aleikum. Nashukuru. Nafaa sana kukutana na Tume la uchaguzi ambalo tumengoja siku nyingi sana. Kwa ufupi kabla sijaendelea na memorandum yangu, hii nchi Mungu alipanga kimajimbo. Tangu hapo zama za Adam mpaka sasa Kenya ipate uhuru hii nchi ilikuwa hivyo kimajimbo. Wa Mijikenda walikuwa na sehemu zao, wengine walikuwa na sehemu zao, watu wote walikuwa na sehemu zao. Hata huyu Mwarabu alipokuja alitukuta kila mtu na sehemu yake. Hata Mzungu alipokuja alikuta watu sehemu zao. Sijui ni kifungu gani cha Katiba kilinganisha hizi nchi kuwa Kenya moja. Kwa hivyo naendelea kumbu kumbu ya Tume katika marekebisho ya Katiba kutoka kamati ya wazee wa Diani, yaani katika Wilaya ya Kwale, Kamati hii inapendekeza mambo yafuatayo.

Mabibi wanaolewa katika ndoa za kienyenji wapate haki za kudhibitisha ndoa zao na serikali katika ofisi za machifu, na

waweze kupata haki za urithi za mali za bwana, wakati bwana wanapofariki, kwa sababu hii, akina mama wanaketi kwa kimila miaka mingi mahali, bwana anapokufa mwanamke huyu hana haki, anafukuzwa ana kwenda kwao na watoto. Kwa hivyo Katiba lazima imlinde mtu kama huyu sababu kosa ni la bwana mwenyewe.

Kifungu nambari thelathini usajisi wa ardhi cha sheria ya Kenya kurekebisha au kufutiliwa mbali kwani inahimiza wizi wa ardhi, kwa mfano haki kama ile ya kupata ardhi furani halafu haiwezi kuponyoka tena na pia anakuwa …. (interjection)

**Com. Swazuri**: (inadible).

**Abdala:** (Cap 300 under acquisition act) okey pia anakuwa na haki ya kufanya ardhi ile atakayvo. Mfano mkumbwa ardhi katika misitu mingi, kama vile wao, Diani, Kinondo, Tiwi, Ukunda, Chale na ule Msikiti wa Congo. Hicho kifungu ni lazima kitazamwe, kina hatari, Cap 300. Kifungu cha sheria cha usalisaji wa ardhi – land registration act cap 300 na kile cha ufadhili wa vitu vya kale, artiquity and monument act chapt 215 zitangamanishwe kwa sababu hivi sasa hazijulikani ni ipi ilivyo na nguvu kushinda nyingine, kususa sheria hizi inapo kushughulikia misitu ya kaa inasajiliwa na serikali kama kifadhi za kitaifa ya kupitia serikali ya makararati (interjection).

**Com. Swazuri**: ……. (inaudible) mapendekezo .

**Abdala:** Mapendekezo yangu Kaa ni lazima ipate kibali Okey?(interjection: inadible) Cha kumiliki ardhi hiyo kuwe na serikali ya majimbo kila jimbo liweze kujisimamia na pia kusimamia rasilmali zake na Wakenya na jamii bali bali wanaokwenda kufanya kazi katika jimbo ambayo sio wanakotoka watozwe kodi. Kwa mfano mimi sio mkazi wa huku lazima nitozwe kodi katika jimbo hilo. Kiasi fulani cha kodi ambayo itakwenda katika mfuko wa maendeleo ya jimbo analofanyia kazi. Sawa sawa? Kiasi furani cha kodi kutozwe kutokana na ushuru unaopatikana katika bandari. Wajua bandari ina pesa nyingi sana, kwa hivyo pesa zilikuwa tangu 1963 wenyewe walikuwa wakichukua pesa wakija nazo huku. Sasa serikali dralimu imechukua hizo pesa na Pwani wamekosa. Kwa hivyo hizo pesa kwanza tunazidai tangu 1963 mpaka 2002 zitoke central government hiyo serikali kuu ziletwe jimbo la Pwani sababu hiyo ni mali yetu **(clapping**).

**Com. Swazuri**: Baada ya hapo? Yale malipo yale ………… (inaudible) na central govt.

**Abdala**: Hao ni wezi watupatie pesa zetu kwanza baadaye mazungumzo okey? (**clapping**). Sheria za kukataza mwananchi kuzuru maeneo ya viwanja vya ndege, reli na mifuo za bahari zilizo mkaba na hoteli ya kitalii ziondolewe mbali. Mwananchi awe ni huru kwama mwanaPwani aweze kuogelea huru huko hakuna trespass ama nini ile public trespass hakuna kitu kama hicho iyondolewe. Sheria ya kunyonga. Hii sheria iyondolewe mbali kabisa kwa vile tuko uhuru afadhali huyu mfungwa afungwa maisha ama apate adhabu. Lakini kunyongwa kuondolewe kwa sababu ni mtu wa Mungu huyo.

Serikali iweze kutengea wananchi maduka ya matajiri sababu kuna hata anapata elfu tatu, kuna mtu anakula million mbili anakula duka hilo hilo kwa hivyo maskini wategemee maduka yao na matajiri maduka yao. Kwa sababu vitu ni vile vile (clapping). Hata elimu maskini wapate shule zao za maskini, na matajiri shule zao. Kama ile Starehe Boys ilikuwa ya maskini sasa imekuwa ya matajiri. Kwa hivyo hiyo ni lazima ishughulikiwe.

**Com. Swazuri**: Mitihani itakuja ya matajiri ama?

**Abdala**: ah hii system lazima ipangwe maskini wapewe mitihani yao, na matajiri yao, maanake mitihani mingine ina-leak. Inanunuliwa. Mila na desturi za kila jimbo zihusishwe na sana inapopatikana na pia inapowezekana katika usimamizi wa rasilmali, mazingira na uamuzi wa kesi za kinyumbani. Pia kuwe na koti za kienyeji badala ya kuenda kule kusema kizungu mzee hajui, lazima aje katika koti yake ya kienyeji apambane na lugha asikizane na wenkake. Ok? Kamati za wazee zipewe uwezo wa katiba ya kusimamia kila shughuli za misitu ya Kenya ambayo sasa hivi iko chini ya makarati ya kitaifa, na uwezo wa kusimamia ardhi. Watumishi wa vidogo wa serikali na hata pia mabani wenyenye walio bemba kusimamia ya kuholela ardhi kihorela ifutiliwe mbali.

**Com.** (not audible)

**Juma:** Salaam aleykum. Sisi watu wa Pwani tunaomba majimbo. Kwa jina naitwa Rashid Juma Chikandu. Kitu cha pili nataka Maendeleo ya utalii, kama unavyoona kwetu sisi kuna utalii, lakini hakuna college hata moja. Nimeeleweka?

Kitu cha tatu ni mashamba, kama tunavyoona mashamba yetu tuko nayo lakini hatuko nayo kwa sababu utaona uko na shamba

yako umekaa hapo kwa muda mrefu kama walivyotangulia hapa wengine kusema, baadaye utaona unaambiwa hiyo shamba imeuzwa kutokea juu, juu kule hatujui ni wapi. (**clapping**) Sasa hiyo tunataka marekebisho.

Halafu katika mambo ya kazi katika serikali ijayo tunataka kila kampuni itakayoundwa kila chief katika location apeleke watu wake katika hiyo kampuni hiyo kabla wa watu wa bara kuingia hapo ndani.

Kitu chingine ni mazao. Mazao kama munavyojua tuna minazi, Mikorosho, Miembe na Mihogo. Lakini tukichunguza sana vitu hizi hazichukuliwi maanani kama vile vinachukuliwa juu kama kahawa na whatever. Kwa hayo ningeomba serikali ichukuwe hilo jukumu la kuchukua hizi bidhaa ziwe zinatafutiwa soko nchi za nje kama zile zinginezo.

Elimu: Katika elimu, Kenya hii, utaona wale wanapata elimu yajuu ni wale matajiri, maskini wanakuwa chini kabisa. Sasa tutaona wale wa chini wanaendelea kuwa chini zaidi na wale wa juu wanakuwa wa juu zaidi. Kwa hivyo tunataka serikali ijayo iwe inaweza kurekebishe mambo hayo. **(interjection: inaudible)** Hii elimu iwe bure.

Chingine ni kuhusu show beach kule baharini. Upande wa biashara kule beach kama mwenzangu alitangulia kusema utaona kwamba wakamba wanauza masanamu kule hwapelekwi kokote wakati wa msako lakini utaona ya kwamba vijana wa hapa wakati wa msako ndio wanashikwa. Hata ukiongea nini unaambiwa hakuna hiyo mpaka kule ndiyo tutajua mambo yako. Sasa hiyo ni kitu ingine ambayo si mzuri. Nataka irekebishwe.

Kitu kingine ni upande wa security. Askari wetu hawa wa utawala wa Kenya Police wanaturunyanyasa sana. Utaona kwamba wakati ninatembea na mtu ambaye ni wa kabila lingine, police wakiwashika, mkienda pale ndani, Onyango anatoka Omari anabaki. Sasa tunataka katika serikali ya majimbo, utawala uwe ni wa wenyewe huku kwa sababu mwenye mji ndiye anajua matatizo ya mji. Kwa hivyo tunaomba iwe hivyo.

**Com. Swazuri**: Andika jina lako hapo.

**Rashid:** Salaam aleikum. Kwa majina yangu ni Rashid Mbogo Zengeza. Mimi hapa nawakilisha the Coast Kaya Elders

Advisory Council kama coordinator wa Coast Province. Kwanza, wazee wa Makaya maoni yao wanasema hizi Kaya zote ziwe chini ya wazee wenyewe wa Makaya na wapewe title deed zao. Sio zimilikiwe na serikali ama mtu wowote mwingine.

Pili, utalii tukijua kwamba utalii 60% wa watalii wanalala hapa Pwani, kwa nini pato linapatikana hapa lakini headquaters ziko bara. Kwa hivyo ile utalii college uregeshwe hapa (**clapping).** Kisha kunjengwe tourism industry itakayo fundisha kazi za ki-talii hapa kwa sababu sisi ndiyo tuna miliki mambo ya kitalii katika hapa (clapping).

Mashamba ama ardhi swala nyeti. Ardhi ni swala ambalo limewatatanyisha watu wengi sana, wazee wa makaya wanasema wanataka katiba mpya ihakikishe kwamba zile shamba walizokuwa wakiziita leased lands, owners lands, reserved lands, zote ziwe revoked ama ziondolewa mbali (**clapping**). Kisha wakasitiza na wakatoa mifano kwamba kuna mashama ambayo pengine ni kuzungumza hivyo wengine hawajui ni yapi. Kama vile Lancaster Farm, liko hapa Diani, Complex iko hapa Diani, kuna Msambweni Development iko hapa, mashamba kama hayo yaregeshwe wenyewe , waridhi halisi. Kwa sababu kuna sheria kwa hii ardhi kwamba eti kitu kikigundulika fui tatu chini ni mali ya serikali hiyo sheria hiyo ifutiliwe bali. Kifungu kingine cha kuhuzu ardhi nasema kwamba mali itakayogunduliwa ndani ya ardhi sio ya mwananchi aliyeko pale, ni mali ya serikali hiyo iyondolewe bali na mali ni mwananchi mwenyewe serikali ipewe kodi tu (clapping).

Shinda si utawala kama wanavyosema wazee, shinda ni hii Katiba ifutiliwe mbali na Katiba nzuri iwakilishe. Hii na-refer point imezungumzwa na wazee wengine hapa. Kwamba wanasema oh si sio shinda ile.

Swala la haki za kimisingi. Usalama na afya bora. Afya mwanzo ikiwa bora iwe bure. Halafu maji safi kwa mwananchi yoyote si ubaguzi kwamba kwa akina fulani kule wana uwezo wanaweza kununua maji safi sisi hatuna. Hiyo iyondolewe na maji iwe safi kwa kila mtu sote tufurahie uhuru wetu.

Elimu iwe bure kwa kila mwananchi kutoka nursery mpaka secondary school that is “O” level. Halafu ile elimu ya higher level, iwe affordable ama inawezekana kulipwa na mtu yoyote. Ajira, iweko, kazi ziweko, si mwingine analala nyumba ya gorofa, mwingine nyumba yake hata udogo miguu unaonekana. Chakula iwe bure mtu anaweza kula three meals a day.

**Com. Swazuri**: Nani atatoa ……………… (inadible)

**Rashid**: Sasa Katiba ikiwa mzuri tuna imani kwamba mashama yatanawiri kwa sababu tutapata maji ya kunyunyiza mashama yetu na tutaweza kuruna matunda na kuuza, tutauza kwa hivyo kila mtu atajipatia chakula chake 3 meals a day **(clapping**). Nikija ya mwisho kabisa kabla sijaondoka hapa ni wazee wa Makaya wanasitiza ya kwamba haki zote za kibinadamu zi heshimiwe zikiweko za watoto, za wanawake zote ziheshimiwe. Na kama zile harassment katika section fulani za police act ziondolewe na kusiwe mtu yeyote juu ya sheria ya Katiba hii mpya. Watu wote wawe sawa waweza kushtakiwa kulingana na serikali iliyoko. Kisha natoa kama ombi ama nalalamika hapa chini. Kwetu mimi ni Lunga Lunga. Sisi watu wa Lunga Lunga, Mwereni, Vanga, Kikoneni, Location tano Zombo, sote tumenyimwa maoni haya kuja kutoa. Walioelezwa mambo haya ni watu wa Msambweni na Diani, ambao wako jirani. Lakini kule Lunga Lunga mpakani mwisho, hukukupelekwa commission yoyote sasa kutakuwa kule hakuna watu wa kutoa maoni. Kwani mimi nimegharamika kutoka Lunga Lunga mpaka hapa, kwa hivyo kama maoni, Wakenya wawakilishwe wote. (**clapping).**

**Com. Swazuri**:……….. wakati ambapo kame moja itaenda hapo uhusiani baina ya Msambweni na Lunga Lunga lakini ………….. (inaudible)

**Rashid**: Thank you very much. Kwa hayo mengi ama machache lakini hapa Bw. Swazuri tunaweza kumbuka sisi hii memorandum yetu tuliandika kitambo na tukawatumia na tuna shukuru kwamba mulitujimbu vizuri wazee wa makaya, na hii ni barua yenu mulitwambia tutengeneze diskette, kwa hivyo tume watengenezea diskette yetu hapa nataka ni wa handover ni wapatie. Thank you very much for that.

**Com. Swazuri**: Mwingine ni Kassim Mwashiki.

**Kassim**: Salaam aleykum. Kwa jina mimi naitwa Kassim Said Mwashiki. Mimi ni mkufunzi katika Moi Teachers College, Baringo. Nimekuja hapa kuwakilisha vijana kabisa, ikiwa mimi mwenyewe ni mmoja wa wale vijana. Kidogo nitaongea kwa ufupi. Kwanza kuakilisha vijana ningesema vijana wa hapa kwanza hawana kazi. Na watu wengi wanasema watu wa Pwani hawana elimu lakini kuna kazi simple kuna kazi ya Shamba Boy, utaona ukifika pale Manager anakuuliza kwanza wewe unakaa wapi? Na kama kwa bahati mbaya yeye ni Mkamba atakwambia, ah hiyo sijui, kwa hivyo tunaomba ya kwamba hii kuwa

watu wa hapa Diani vyama wengi hawana kazi na ndio na changisha kuwa kuna uvutaji mwingi wa Unga. Kwa hivyo, ningeomba tafadhali kuletwe mtu ambaye ni mkaazi wa hapa, ama yule ambaye yuko hapa awe ana zingatia sana matakwa ya wenyewe hapa. Ni hii inawezekana tu wakati ambapo pengine tungekuwa na Manager wetu pale. Kitu kingine ninachoongea ni (interjection)

**Com. Swazuri**: Manager wenu kutoka wapi?

katika mkoa wa Pwani tafadhari kwa hivyo tunataka tuwe na Manager wetu ndiposa ajira zitakuwa rahisi, kwa sababu yule ambaye yuko hapo anazingatia ukabila.

**Com.Swazuri**: Manager wa wa wa kule hotelini ama manager wa wapi?

**Kassim**: Manager wa hotelini. Tunataka awe mtu wa hapa kwa sababu wale ambao si wakaazi wa hapa ukifika pale malengo yao hao wanachukua kiubaguzi na hiyo imechangisha kuwa kuna ufutaji mwingi wa bhangi, unga n.k. Point yangu ya pili ni kuhusiana na intake katika institutions, colleges, kwa hakika ni kitu kinacho nisikitisha sana, kuona ya kwamba training institutions kama Chanzu. Almost 70% ya ile intake ya pale si wakaazi wa kutoka mkoa wa Pwani, wengi wao hata ukienda leo utaona ya kwamba wengi ni watu kutoka kule sijui ni kitu kilipangwa ama vipi. Halafu pia mimi nikiwa na some kule Baringo hii second intake ya waalimu unakuta inahusu tu inatoka tu within Baringo District. Ni kitu cha ajabu kwa sababu wengi wao ni watu ambao tunaongea nao. Kwa hivyo utaona wengi wanatoka pale pale tu ili hali hapa kwetu ni kitu cha kusitisha kabisa.

**Com. Swazuri**: Sasa ungependa tufanye nini tu solve hiyo problem?

**Kassim:** Ningependa tafadhali wakati wanafanya intake iwe evenly distributed tafadhali. Halafu kitu chingine mwenzangu ameongea, hapa Kenya tunategemea utalii na utalii kususa uko katika sehemu ya Pwani. Ajabu ni kwamba utalii college iko huko ili hali utalii ambao ni uti wa mgongo uko hapa Pwani. Sasa mtu anatoka hapa anaenda kule na ukienda huko mamabo ni yale yale ambayo nimeyasema. 80% utakuta si watu wakutoka hii sehemu ambayo utalii nitegemeo.

**Com. Swazuri**: Una habari kwamba serikali umesema itojenga chuo cha Utalii kule kijipwa (inaudible)? Unazo habari hizo?

**Kassim:** Kama ziko ni maoni mazuri sana kwa hivyo ni naomba serikali kama ina mawazo mazuri hivyo basi iyendelee kufanya hivyo.

**Com. Swazuri**: …………. Kiwanda imesha weka pesa tayari land ishapatikana watajenga kijipwa.

**Kassim**: Sawa Sawa kabisa Utalii college itarudi hapa kwa hivyo muwe tayari ili twendeni kazini. Mwisho hii Kenya vile ninavyoona hii Kenya imegawanyika kimajimbo viongozi wote tumechaguliwa sijui kina, Raila – amewakilisha nani huyo? Halafu huyu wetu hapa nyote mwawajua viongozi wote mkiwangalia hivi ina picha ya kuwa haya ni majimbo. Na kwa sababu ya haya ubaguzi, ubaguzi wa intake ya watoto wanachaguliwa ki-ubaguzi, ni kwa sababu hamna mtu wenu na hiyo ni kutaka majimbo kwa sababu kama hawataki, wanataka majimbo. Kule wenyewe wanachukuana kwa sababu mimi niko kule. Huyo intake ya colleges wanachukua pale pale ni nini? Wanataka kuelimishana wenyewe kwa wenyewe ili kukija majimbo wao wawe mbali. Kwa hivyo mimi naomba majimbo.(**clapping**).

**Com. Swazuri:** Ali Kweli.

**Omari:** Asante sana ndugu wa Commission hii mimi kwa kusema kweli

**Com. Swazuri:** Jina lako kwanza. Ali omari Kweli kutoka hapa hapa Diani. Mimi nimekuja hapa nawakilisha welfare ambayo inaitwa tushauriane ambayo inawakirisha wananchi kutoka Ukunda sub-location na Gombato sub-location. Mimi langu hasa nitaanza na ku-comment, kuhusu Katiba ninayotaka mimi na wale wenzangu ambao tuko pamoja. Huu mgogoro wote umeingia kuichafua ile Katiba ambayo ilitoka Lancaster House kuifanyia mabadiliko thelathini na manane ndio imeleta mgongoro ( **clapping**). Na hii ni nia ya Wakenya wenyewe, watu weusi. Waliotupa Katiba muda ule waliichunguza na kuikubali walikuwa watu weupe tunaowaiita wakoloni na wengine Waarabu. Lakini wamekuwa na nia nzuri kutupatia Katiba ambayo ingetufaa, ambayo haingeleta mgogoro. Lakini uchafuzi umeanza kwa sababu ya nia ya watu weusi wenyewe Kenya wale ambao wengi walisema wao ndio wapiganiaji uhuru ndio walio badilisha Katiba kama hii mpaka ikalieta mgongoro sasa wakenya hawapatani.

Kwa hivyo pendekezo la moja kwa moja, Katiba ile iliyoleta uhuru hapa ilikuwa ya majimbo; ilikuwa ya vyama vingi na ilikuwa

na mabunge mawili na ikiwa na waziri mkuu, pamoja iwe na Rais. Halafu majimbo ilikuwa na uwezo wake kila kitu kilipangwa sawa sawa. Lakini kwa ulafi wale wengine waliokuwa mstari wa mbele waliona haiwezekani, afadhali wavuruge Katiba ili walete serikali moja nchi moja kwa manufaa yao, si manufaa ya watu wa Kenya. Kwa hivyo moja kwa moja ombi langu mimi nasema, kwanza kabisa Katiba ile ile irudishwe moja kwa moja bila kuondolewa hata kipengele kimoja (**clapping**). Ni Katiba ambayo ita tufaa sisi kwa sababu ilikuwa imepangika sawa sawa na kila kitu walifanya hayo walikuwa na nia ya Wakenya waishi pamoja wawe ndugu na wapendane, lakini wenzetu walioanza kuwa msitari wa mbele ndio waliokuwa na nia mbovu na mpaka sasa ndiyo imeleta haya matatizo. Kwa hivyo ombi nikusema, katiba ile urudishwe bila kuondoa hata kipengele kimoja.

Jambo la pili na sema, ni ajabu moja ambayo sisi wapwani tukija hapa Pwani wale wenzetu wanatumikiwa tu na Katiba moja, haidhuru imechanganywa changanywa ikaleta adhari lakini wale wa bara wote wanatumikiwa na Katiba moja tu hiyo hiyo ya nchi ya Kenya lakini wananufaika. Sisi ambao saa hizi tungetumikiwa na katiba mbili wa Pwani kwa sababu tungetumikiwa na Katiba ya nchi ya Kenya na pia mkataba wa Mwambao ambao Wakenya walipotaka uhuru walikubali mia kwa mia mkataba wa Mwambao wa wakauchukulia dhamani kuwa lazima watu wa mwambao wawekwe hivi.

Tukaahidiwa kuonekana kuwa maneneo ya mwambao ambayo yalikuwa yamejaa waislam ma DO, Ma-DC, Ma-chief, ma-Inspector Police, ikiwa kuna Ma OCS na OCPD wote watakuwa Waislam ili waweze kuchunguza hali zao (clapping). Lakini ni kusema mipangilio hiyo yote hakuna hata mmoja uliotendeka hata saa hizi ilikuwa ni watu tu kuondoa ile katiba na kutegema serikali za mikoa ili makusidi wafanye order, kila kitu ni ku-order tu. Ikifanywa order kule ardhi ichukuliwe basi, hakuna majibu. Na lazima aliye pewa order akachukue majeshi akapige watu awatoe ardhi iyende. Sasa kulingana na hiyo hali, inaonekana moja kwa moja sisi kama watu wa Pwani tuna test tu hivi sasa hii ni kitest kutaka majimbo ikiwa wenzetu watakubali. Na ikiwa hawakubali sisi wapwani kupitia yule aliyechukuwa utawala kwanza amekubali kuwa Pwani ni kipande kilichoko peke yake.

Kwa hivyo ikiwa watu wa bara hawataki kukubaliana undugu wa kuwa na majimbo ni kila mmoja afaidike, ni lazima sisi tutegemee mkatamba wa Mwambao na tutake Pwani yetu ili jimbo lijitenge. Hilo ni jambo la wazi ambalo halitaweza kufanyiwa woga (**clapping**) Kwa hivyo moja kwa moja sisi twasema tunafanya test ikiwa mwataka ndugu wenzetu mlioko huko hizi

habari pengine zita wafikia vizuri. Wakipataa undugu basi, wapwani wajitokeze sasa kwa sababu ilikuwa hatujapigania uhuru wale wenzetu walipigania uhuru ndiyo sababu wakaharibu Katiba ya umoja, sasa ni sisi tutakuwa tujitokeze tupiganie tuhakikishe Pwani imejitenga. Kwa hayo machache mimi nitabakia hapo basi sitaendelea mbele **(clapping**) **(noise)**

**Com. Swazuri:** Andika jina lako pale. Bakari Swaleh

**Swaleh:** Arabic greetings. Jina langu kamili ni Bakari Swaleh Mwakumanya ama ukipenda ukiniita Moya ni sawa. Maoni yangu moja kwa moja ingawaje yamepitiwa na mimi pia ni majimbo. Tunapenda serikali ya majimbo na si vihonja maanake ilikuwa imependekezwa kutoka hapo kutoka Lanchaster House. Halafu ikafurugwa karibu mara thelathini na mbili. Kwa hivyo tunaomba iregeshwe na kama alivyosema mwenzangu ikiwa wenzetu hawaipendelei majimbo wanaona wanapokonywa pokonywa sisi tupewe majimbo inshallah kwa sababu hilo ndio lengo letu na tuone sisi tutafaidika ki vipi?

Tunaomba serikali hizo za majimbo ikiwa kutakuwa na Rais, asiwe juu ya sheria, apokonywe uwezo apunguzwe uwezo. Uwezo uwe watoka kwa wananchi wenyewe (**clapping**) Kwani kuwa juu ya sheria ni kujitweka laana. Mwenye kwa juu ya sheria ni Mungu peke yake kama watu hawajui wajue leo. Tunapenda serikali ya kuzingatia haki. Kitu chingine tunaomba mahakama ya Chief Kadhi iwe na uwezo na iwe na koti ya appeal ili Muislam akistakiwa ikiwa hakuridhika ataweza appeal kwenye koti ya ki-islam vile vile. Isiwe huku asikiswe mara anaambiwa hii kesi itasikiswa kule hii itakuwa ni dhuhima kabisa na ni kukosa kujua haki za mwenyezi Mungu.

Kitu chingine tunaomba ma-bar yaondolewe katika sehemu za Waislam kwani yamevuruga kabisa vichwa za watu (**clapping**). Kitu chingine ambacho tunaomba serikali ijayo iweze kutoa mwongozo wa wanawake wavae kiheshima vasi lenye heshima si kuvaa tupu tupu. Hii Kenya imeondoa baraka kama watu hawajui kwani Mwenyezi Mungu anataka mwanamke asionekane hata nywele lakini tunaona ajabu mwanamke anavaa nguo hata huwezi kumwangalia.

Kitu chingine ambacho tunafuatia tunataka kitabu cha Mwenyezi Mungu katika koti kiondolewe kisiwe kinaapisha watu ile ni sheria ya kuwaambia watu si kuapisha watu kwenye koti. Tunataka heshima ya kumuinamia Judge iyondolewe kutoka ama kuingia heshima ni kunyamaza kwenye koti wala si kuinamia. Hiyo ni heshima ya Mwenyezi Mungu haifai kwa mwanadamu.

Kitu kinachofuatia ni tatizo sugu la ardhi. Vita vyote vimeletwa na ardhi. Wakati wa kugawanya ardhi kulikuwa na vifungu vinne. Kwanza mwananchi ambaye analima pale apate ardhi. Wa pili, ni mwananchi wa pale ambaye halimi lakini heshima akahama apate ardhi. Tatu, mwananchi yoyote ambaye ni wa sehemu hiyo apate ardhi. Nne, kama kuna nafasi basi ndipo Mkenya, mwingine lakini serikali imechukua hiyo hatua ya nne kuwa mwananchi wowote apate ardhi. Tuna ardhi zetu tulizonyang'anwa na ambazo ziliuzwa bila halali. Mtu amelima miaka nenda miaka rudi, lakini watahamaki mtu anakuja kikaratasi anasema hiyo ardhi ni yangu. Imeisha, masitikiko ni kwamba ardhi yangu pia imekatakatwa. (interjection not audible) imekatakatwa na imelimwa (interjection not audible) na hiyo serikali kwamba imewahi karibu mara mbili, imewahi mkondo wa kwanza, wa pili tukakosa ile ardhi hajui number yako ni ipi. Kwa hivyo inapenda haki ya dhiluma hizo zote ziondoke.

**Com. Swazuri**: (inaudible)

**Hassan:** Salaam aleykum ndugu Waislam na wasio kuwa waislam pia na pia Tume ya maombi. Mimi jina langu ni Hassan Saidi Mwamnyambo kutoka hapa Ukunda Magutu. Kwa maoni yangu mengi nitakayozungumza (tape stopped side A tape 2)

Pili nataka hapa Diani beach kwa mfano, katika sector ya Utalii inaongoza kabisa lakini ukienda kule walioajiriwa 75% ni watu wa bara, na ukiuliza munaambiwa nyinyi hamukusoma lakini hebu tuambie, wewe Bwana Swazuri wewe mwenyewe ni kutoka hapa Pwani kama hujasoma ungekuwa kwa Katiba hii? Kwa hivyo hii ni kitu kimoja wapo kwa sababu vyuo vya utalii havikunjengwa hapa Pwani. Ikiwa hapa ndiyo kuna watalii wengi kwa nini vyuo vya Utalii viwe kule bara? Umezungumza tayari umesema chuo kitanjengwa kule kijipwa lakini kimechelewa. Kwa hivyo nasema ikiwezekana vyuo vya utalii wiwe hapa na watu wafanye mafundisho wengi wao wachukuliwe kutoka hapa mko huu ama kutoka sehemu ya district hii.

Kitu chingine ni kwamba, mambo ya vyuo vikuu viwe viko hapa Pwani kwa sababu watoto wanaoipita hapa, wanaambiwa hawakupita kwa sababu nafasi za chuo hawana. Kwa sababu angalia nchi zingine zote zingine zina utalawa wa wakubwa wakubwa huko kumejegwa vyuo karibu mara tatu kama Moi, kuna Egerton kuna wapi n.k. Hapa Pwani ni pa kubwa na hakuna chuo kikuu chochote hata kimoja. Kwa hivyo tunaomba katika Katiba ijayo viwe vyuo vinajengwa viwe kama vile

maskuli.

Kitu cha tatu ni mashamba. Tunaomba Katiba ijayo iwe na serikali ya watu kila mmoja awe na maji katika kwake shamba ya kunyunyushia mashamba na pia mazao yako hapa Pwani nafikiri ishaelezwa kitambo haya. Mazao ya hapa, watu wale wanasema tunangonja maembe yaanguke wacha iyanguke kwa maana haina thamani. Ikiwa maembe yako hapa na hatulimi yamepandwa na nani hayo? Tunataka matunda ya hapa kama Korosho, nazi badala ya Kinyanjui akauze nazi zetu sisi tukauze wenyewe huko ulaya **(clapping**).

Na pia kitu chingine cha kumalizia, katika mashamba hapa kama Bw. Bakari alivyo kwambia kwamba mashamba katika serikali hii tuliyo nayo yalikuwa yanagawanywa ofisini kwa machifu na maDC na wambunge wetu wana ambiwa fanya hivi, ukikataa ni vile vile wewe umelima hapa mahali umefyeka msitu una minazi na wewe unaambiwa hiyo shamba sio yako hii shamba ni ya muhindi ama ni ya Njenga unakuja kuonyeshwa na watu kutoka ofisini. Tunaomba sheria ijayo, ama sasa kabla hii Katiba ijafanywe yale mashamba yetu tupewe. Pia katika mashamba ya beach, ambayo yana dhuluma hapa beach, hapa Pwani mashamba yote yalienda kuliundwa Gema. Gema ilimaliza watu wa Pwani kisiasa na ki mashamba kwa sababu mashamba hayo yalikuwa yapeanwa number kule Nairobi, wewe una ambiwa mzee uanuza shamba yako wewe, ndiyo twende Kwale unahesabiwa note ya tano tano na kumi kumi unataka elfu ngapi? Zingine zinaongezwa huko mbele. Unaambiwa shamba hiyo umeuza kwa mia tatu na wewe ulitaja elfu thelethini hizi ni dhuluma nyingi sana.

**Com. Baraza**: Hawa kuruhusu wewe ku-count hiyo pesa?

**Hassan:** Sasa kama saa ingine kila watu wako na akili zao mtu mwingine anachukua mtoto wake amesoma mwingine haja soma anakwenda yeye mwenyewe tu kwa sababu amefuatwa na car. Kwa hivyo hizo vitu lazima muangalie mashamba yaliyoenda kama ya beach. Tukiangalia Wadigo wenye mashamba beach hakuna mtu hata mmoja hata Mbunge wa hapa ana hoteli huko, na amekaa kwa miaka 35 (**clapping**). Matiba ametoka kwao amekuja kujenga nyumba hapa ukitaka akuajiri ukiongea, anasema jengeni yenu muajiri watu wenu. Je hii ni sheria kweli? Utakuwa na uhuru kweli hapa Pwani? Sisi bwana – Pwani hatujapata uhuru kwa hivyo kwaherini nasema …… (**clapping**)

**Fatuma:** Greetings in Arabic. wataala wa balakati. Mimi mzaliwa wa Diani, Gombato sub-location, Mwaroni Village kwa jina

naitwa Fatuma Abdala Mwanyuchi. Chama ni Maendeleo ya Wanawake Msambweni Division, mfanyi kazi wa huduma za jamii. Kwa niaba ya akina mama, wa Msambweni, kwa niaba ya watu wa Kwale, kwa niamba ya watu wa Pwani, Kwa niamba ya watu wa Msambweni Location wamenituma, tunataka majimbo **(clapping**). Tunataka majimbo kwa sababu tume choka kutoka 1963 haadi sasa hatujui maana ya uhuru ni nini (**clapping)** kwa sababu mahitaji yetu hayajatekelezwa na serikali iliyo pita.

Serikali hii ijayo tunataka iwe ya majimbo kwa sababu ya kurahisisa usafiri hata kitambulicho ukitaka kinakaa miaka tatu kabla hujapata ukipoteza. Rasilmali zetu ambazo tunazo hapa Pwani ni za maana sana na hasa hiyo serikali iliyoko inategema rasilimali za Pwani, utalii – ambayo ni bahari na Port. Chochote kinacho ingia kutoka nje kama kina usafiri wa bahari kinatelemshwa popote halafu kina ruka kinaenda mbala inagawanya yake hatuyajui wala hatuyathamini kwa sababu hatuyaoni. Majimbo ni manane ama province ni nane labda hizo saba ndizo zinasaidia rasilmali zetu ama mapato ya hapa Pwani, kwa hivyo majimbo ( **clapping).**

Jingine ni usalama. Usalama kwa hakika ni mbaya sana hasa hata hapa kwetu Pwani, kwa sababu upande wa madereva. Madereva hawachugunzwi vilivyo kwa sabasbu kuna huyo ulagai wa bara barani. Dereva akienda akifika kituo anaangusha mia moja anenda. Yeye mwenyewe si dereva timamu, yeye mwenyewe miaka yake haimuruhusu kuwa na driving licence alikuwa tu manamba hapo Ferry ama alikuwa manamba Kinango baada ya muda ashapewa licence anapeleka gari. Tumepoteza watu wengi sana bara barani.

Ufisadi huu wa kuweka shilingi mia moja chini ya bara bara na kwenda haukaguwi gari wala haukaguwi dereva. Ombi langu Katiba ijayo, dereva aanzie miaka thelathini asianze miaka ishirini ama kumi na tano huyu hajakuwa timamu wa kupeleka ngari, la si hivyo kuwe na uchunguzi wa hali ya juu, asiwe tu dereva, manamba wakutoka pale Ferry jana alikuwa anaitisha pesa, leo wamuona dereva hata anasahau anapiga gari huku anapiga kule mbele paa! Anaona bado ni manamba (**clapping**).

Jingine haraka haraka ni kwamba naomba usalama huu umetushangaza kama tungekuwa na serikali yetu ya majimbo Commissioner wa Police yule aliyoko kule Nairobi angekuwa Commissisioner wa majimbo hapa Mombasa akajue vile tuna sukwa sukwa na wezi usiku. Siku hizi hata saa moja unapate simu unaambiwa inuka enda nyumbani ukatoe vyombo. Sasa

ombi langu; mtukufu Rais aliyenda safari akapelekewa simu kwa sababu hiki kikosi cha Mungiki kilicho fanya maafa alipokuja akachafuka, akazungumza ukali mpaka akasema hicho kikundi hakitaki. Basi Commissioner wa Polisi kule Nairobi akachukuwa uzito wa kuwa sungu sungu wote Kenya wasiweko. Eh hebu na asafiri aje hapa Mombasa, Kwale, Diani ambako tunajukumu la kuchukua mataifa wote wa dunia nzima. Hapo kwa sababu ya utalii, sisi tumekaliwa na kabila zote na dini zote hapa. Sasa na wezi wale wote ambao hawana pahali pa kuiba wanateremshwa na gari lile ya jicho moja wanakuja na ndege.

**Com. Swazuri**: Tupatie resolution yako. Ombi langu Commissioner wa Police atufungulie sungu sungu zote ziyendelee kwa ulinzi hasa hapa Diani location.

Dakika yangu ingawaje imeisha sitakosa la kusindikiza. Dini, naomba tu kidogo kama wengine wataomba, wataomba; naomba Waislam siku kuu ile ya Ramadhani ina julikana Public Holiday hata hii siku kuu ya mfunga tatu ambayo ni kama pasaka pia izingatiwe Katiba ijayo tupewe holiday (clapping) hiyo siku kuu ya Hirja tukienda swali tukae ma nyumbani tujisikie hata sisi tuko siku kuu kama wale waenda pasaka.

Pia naomba wafanyi kazi waserikali na wengineo wa Waislam siku ya ijumaa wafanye nusu siku ikifika saa tano waende wa kaswali vizuri bila jasho na waende nyumbani wa kapumzike wakijua ni siku ya sala ya ijumaa (**clapping**). Mwisho ama mwanzo siasa. Serikali iliyoko ilituahidi kwamba hii Msambweni Division itagawanywa division mbili na ikiwa Msambweni ni sub-district sasa uchoyo wa kuandika wafanyi kazi wa serikali mpaka sasa haijakuweko. Ombi langu naomba kabla hii Katiba haija endelea kumalizwa mukiwa mwazungumza mambo ya elections twa taka hata ikiwe haija tabulikana hayo ya kugawanya division. Lakini mjumbe mmoja hatoshi location kumi na moja (**clapping**) twaomba katiba ijayo ipitishe wajumbe wawili Msambweni Division maanake tuko na location kumi na moja ngumu.

**Com. Swazuri**: inadible

Mwisho nasema, vitambulisho viwekwe kwenye malocation vile picha kila kitu ili isiwe msongamano wa vetting hii kuandisha kikadi cha kura hiki na wengi hawana vitambulisho mambo yanachelewa. Na pia wale ambao wataandikisha vitambulisho badala ya miaka kumi na nane iwe ishirini kwa sababu atakuwa kijana mzuri na msichana mzuri mwenye akili timamu. Asanteni (

**clapping**) mengine mtasoma humo yamo mengi sana.

**Com. Swazuri**: Robert Mwangi na mzee Omari Mazuri awe tayari.

**Mwangi:** Salama aleykum. Mimi naitwa Robert Mwangi mwenyeji hapa nikitaka kusema maana mahali ukiishi miaka zaidi ya thelathini, wewe ni mwenyeji. Mimi ombi langu naomba Katiba (interjection inaudible) ombi langu ni tufungilwe minyororo. Hatuko uhuru kabisa **(clapping**). Sisi nikisema hatuna huru Katiba inayelinda mufanyi kazi ni kama mnyororo uliofungwa mwananchi wakawaida. Kama kwamba tumeshaona na makampuni hapa katika nchi yetu hasa parastatals (yaani serikali ina shares ndani yake) zinafilisika na zikifilisika mfanyi kazi wa kawaida mwananchi wa kawaida inasemakana hawezi kulipwa kwa sababu rasilmali ya kampuni iliyouzwa pesa mpaka zilipwe bank, na zilipwe serikali ichukue rasilimali yake. Wewe mwananchi wa kawaida hakuna mtu anayekutambua wakati ule na wakati mwingine ulifanya kazi pahali pale zaidi ya miaka thelathini. Sasa ni Katiba inayoelekea kuundwa iundwe katiba yakusimamia mwananchi wa kawaida. Tuwe sawa sote hakuna mtu ambaye si muajiriwa hata Rais ameajiriwa hata na mawaziri na nani kila mtu ni muajiriwa. Hii katiba iwache kuchagua, kumbagua wafanyi kazi wa chini na wafanyi kazi hali ya juu. Tungetaka Katiba hii ibadilishwe na iwe sawa kwa watu wote.

Nafikiri mengi yamesemwa na sitaki kuchangia mengi zaidi ya hapo kuna wengine wanangonja kuzungumza yao hilo kama ni la mhimu basi lifuatiliwe. Asante.

**Com. Baraza**: ……….. (inadible)

**Mwangi:** Mimi siko kwenye siasa niko kwenye kutetea haki za wananchi.

**Com. Swazuri:** Omari Mazuri, hayuko?

**Omari:** Salaam aleikum. Jina Omari H. Mazuri nikiwa mkaaji wa sub-location ya Ukunda. Kwanza kabla sijatoa maoni ningetaka kufahamisha tume kwamba nia yangu na madhumuni yangu ni kutaka majimbo. Na sababu ya kutaka majimbo kwanza ni ardhi. Ardhi ni kitu ambacho hapa Pwani ama hapa tulipo tumekuwa sugu kiasi ya kuwa mwananchi halali wa hapa hana raha hata kidogo. Zile ambazo zinaitwa settlement scheme kwa kusema ukweli zimegawiwa kimakosa. Kwa sababu kama natoa mfano wa Diani settlement scheme ina plot kama mia nne na arobaine na sita za hekari tano tano lakini wenyeji

halisi, walipata kama mia moja hamsini zilizo mbaki zote zimeenda. Na kama zimeenda basi, ndiyo sababu nasema tuwe na majimbo na Katiba ibandilishwe hizi settlement schemes ziwe – nullified na sikiwezekana zigawie wenyewe wanao husika, sababu kulikuwa na watu wameishi hapo kabla ya mkoloni wala Mwarabu kuja.

Pili, kinacho fanya mimi niseme nataka majimbo ni elimu. Elimu kwa kusema ukweli ilianza hapa pwani muda wa miaka elfu moja ishirini na tatu lakini ajabu ni kwamba mpaka sasa tunapozungumza kugeuza Katiba hakuna hata chuo kimoja kikuu ambacho pengine kingeweza kuwanufaisha watu wa Pwani. Je, itatuchukua vipi elimu kwa muda unaokuja ikiwa hali itakuwa hii.

Tatu, nataka Katiba igeuzwe kwa sababu hali ya uchumi imetuzorotesha kupita kiasi. Kwa sababu inaonekana robo tatu ya uchumi wa Pwani inakwenda mahali nisikojua. Na utaona kwamba watu wamedhoafika kwa sababu wana minazi, mikolosho, miembe na miti tofauti tofauti ambayo ni ya pesa, lakini hakuna hata kidogo kinacho wafaidisha. Hakuna bei hakuna chochote kinachotafutwa ama kiwanda cha kuweza kuwasaidia hawa wananchi pengine waweze kubadilika ki uchumi hivyo basi wanazidi kudidimia. Uchumi ulivyo ni kwamba mkoa wa Pwani unachangia robo tatu ya uchumi.

Utalii utakuta kwamba uko sehemu hii ya Pwani lakini mapato yake na mazao yake haya julikani yanako kwenda. Tuna Kilindini pale ambapo ndipo tunaweza sema ni jicho la East Africa ama la Africa pia sehemu lakini hatufaidiki na chochote. Masitikiko ni Kwamba kila kitu kina kwenda. Usimamizi wa kila aina uko mahali ambapo hatujui tufanye nini.

Kwa hivyo kwa sababu wenzangu wamesema nataka kumalizia kwamba pia tunataka majimbo au Katiba ibadilishwe iwe ya majimbo na ziwe sheria za kimajimbo ni kwamba hata Uislam umepigwa vita kiasi cha kuwa haujulikani wala hauna nafasi ya kupumua. Mpaka sasa umekuwa Muislam sasa akiwa na imani ile kali anaitwa terrorist. Kwa hivyo ni vitu ambavyo tunataka majimbo yapatikane usimamisi wa hali kama hizo ziweze kusimamiwa na watu wenyewe na waone wataweza kuendesha namna gani. Kwa hivyo sitaki kuchukua muda mrefu tume, nataka kuwapatia nafasi wenzangu na hayo mengine yatasemwa na wenzangu. Asanteni. **(clapping**)

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Salim**: Kwa jina naitwa Said Salim Mwawimo, Chairman wa Busara Men & Women Group. Maoni yetu kwa jumla tunataka majimbo. Kulingana na katiba mpya tunayoitaka Rais wa zamani alitoka katika mkoa wa central province baada ya kifo chake Urais ulienda Rift Valley na kwa dakika hii ya Katiba tunayoitaka tunataka watu wa Pwani wapate Urais safari hii ( **clapping**).

**Com. Swazuri:** ……… Mwapatiwa Urais au una-rotate kila province?

**Salim:** U-rotate kila province kwa sababu wasiwe na tamaa tena Wakikuyu watapata au Wakalenjin watapata. (**clapping**). Tunahitaji jimbo letu la Pwani liwe peke yake, kwa sababu lile jimbo la Pwani lilikuwa ni Kenya Protectorate na lile la mbala lilikuwa ni Kenya Colony ambalo liliungana tarehe tano mwezi wa kumi na moja mwaka wa 1964. Wengi wa viongozi wa Pwani hawakuweko wakati huo. Na kile chama cha KADU kiliweza kuvunjwa tarehe kumi mwesi wa kumi na moja 1964 na kuwa chama kimoja na KANU chini ya uwenye kiti wa Urais wa Kenyatta. Na ndipo watu wa Pwani wakazidi kudidimizwa baada ya chama chao cha Pwani kuunganishwa pamoja na Kenya.

**Com. Baraza:** Wabunge wenu walikuwa huko? Walifanya nini huko?

**Salim**: Walindanganywa. Tulizidi kundanganywa na ile Katiba yetu ya majimbo ikaondolewa na diposa hayati Kenyatta akajiweka madaraka mengi katika uwezo wake. Kulingana na Katiba ya majimbo tunayotaka tunahitaji asilimia sabini na tano ya watu wa mkoa wa Pwani wawe wameajiriwa kazi, waliosoma, na wale ambao hawajasoma. (**clapping)**.

Pili, tunataka mkuu wa mkoa achaguliwe na wananchi wenyewe kutoka sehemu hiyo tunayotoka. DO na DC wote wachaguliwe na wananchi wenyewe na mpaka machief tuwapigie kura sisi wenyewe. Katika sector ya utalii asilimia sabini na tano itumike katika mkoa wa Pwani kwa ukarabati wa zahanati pamoja na kununua madawa kwa sababu uongozi ulio sasa umefunja pesa nyingi sana. Maskini haweze kujitekeleza katika kwenda hospitali na iwapo utampeleka huko Msambweni ni kama anaenda kupata kifo kwa sababu hana chochote ambacho anaweza kujisaidia. **(clapping**)

**Com. Swazuri:** Kwa hivyo iwe bure?

**Salim**: Iwe bure. Tukipita kwa upande wa sector ya bara bara twasitikika sana kwamba katika sector hii ya utalii katika sehemu hii yetu ya Kwale imetupatia pesa nyingi sana lakini tukiangalia bara bara zetu zimekuwa mbovu hali ya kwamba serikali hatujui inafanya kazi gani. Kwa hivyo tunahitaji serikali ya majimbo kwa sababu iweze kutengeneza bara bara zetu kutoka Shimba hills, Kikoneni, Shimoni na mpaka sehemu nyingine ambazo ukarabati wake wa bara bara umekuwa mbovu kabisa.

Masilahi ya wanyonge. Serikali ya Uingereza ilikuwa ikitoa ushuru kwa watu masikini na wale ambao hawana kazi na walemavu. Tunataka katika Katiba mpya ijayo watu kama hawa waweze kupata ushuru (**clapping**). Tunataka katika Katiba mpya tuwe na bunge la mseto na Bunge la Mkoa wa Pwani ambapo katika kila mkoa uwe na Governor na uwe na Masilahi yake.

Kuwe na Katiba ya kijamii, kuna Katiba ya Mijikenda, kuna katiba ya Wandigo na mambo ya kale ambayo yalikuwa yakifanywa na mababu zetu kama kulinda makaya, misitu na utamaduni. Tunataka mambo haya yarudishwe kwa wenyewe wananchi. Tunataka Kiswahili kihalalishwe katika Bunge letu lijao kiweze kuzungumzwa Bunge na mtu aweze kuwasilisha hoja lake bungeni kwa Kiswahili. Katika utumishi wa uma usiwe chini ya Rais na Judge mkuu achaguliwe na Wabunge na asiwe katika chama chote cha kisiasa. Na ikiwa Katiba hii itapitishwa itaweza kumshtaki kiongozi yoyote kutoka Rais mpaka Wabunge wanoenda kinyume na Katiba ya wananchi (**clapping**).

Na ile tume ya uchaguzi ichaguliwe kutkoa kwa Maimam, Mapadri na wasomi. Na zile sheria za kizamani za kibepari, kujilimbulukia madaraka mengi ziondolewe, ile sheria ya kuweka mtu kizwizwi kwa kiongozi wa taifa kwa sababu ya manufaa yake hatuitaki. Manufaa ya vyama vyote via kisiasa yaweze kupatina wakati wanafanya mikutano yao wasiweze kusumbuliwa.

Katika utumishi wa uma – polisi anaweza akushike akuandikie mashtaka ya uongo na pia awe amekupiga katika cell, kama wewe huwezi kujitetea na kufanya kumshtaki sababu ya kujaribu kukugandamiza. Kwa hivyo tunakata katika katiba mpya inayokuja Polisi kama huyu aweze kuchukuliwa hatua kwa kufanya mambo kama hayo. Asante sana.

**Com. Swazuri**: Mohammed Yusuf? Omari Edward utafuatiwa na Ramadhani Mwasira.

**Omar:** Salaam aleikum. Majina yangu kamili ni Omar Edward Zaro Mwanza. Mimi ni mzaliwa wa hapa kijiji hiki cha Magutu na maoni yangu kamili, sisi tunataka majimbo. Majimbo yatatusimamisha kwenye msururu wa kupigania haki zetu na pia kujiendeleza kimaendeleo na hata na kwa kazi za mahoteli. Kwani sisi hapa tumetegemea kazi za mahoteli kama watu wa Pwani. Kusema ukweli watu wa bara huja hapa kutoka mahoteli iyaanze na hawaja fundishwa kazi na vyuo vya utalii. Tunawafundisha kazi sisi wenyewe baadaya miezi mbili tatu wakijua kazi sisi tuna simamishwa na hatuna haki ya kusema lolote. Kwa hivyo tunaomba Katiba ijayo ama hii Katiba tunayopigania sasa tuwe na haki zetu za kuajiriwa kazi hotelini kulingana na ujuzi zetu tulionao.

Na mengi yamesemwa na wenzetu. Kitu mhimu zaidi ni kuona akina mama wanakaa kama wafungwa hasa wanapofiliwa na bwana zao. Kwani utaona mashemeji zao wanawapokonya mali walizotafuta na mabwana zao kwa sababu hakuna sheria zinazo fuatwa hata ukiangalia watasumbuka na watoto kama ambao hawana wazazi ama vipi.

Kitu cha pili tunachotaka ni kusimamia mambo ya mashamba vijana nasi tuwe na mashamba. Kwa sababu mababu zetu na baba zetu wamepata shamba moja moja na kuna ardhi ambazo zimetengwa na zinagawanywa nasi pia tupate vipande vya mashamba ili nasi pia tukiwa wazazi, tujue watoto wetu watamiliki nini. Na kuongezea zaidi wenzangu wakiendelea lakini majimbo tunaitaka. Majimbo, majimbo. Asanteni.

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Ramadhani**: Arabic greeting. Kwa jina ni Ramadhani Bakari Mwasina. Yangu mimi ni kindogo sana sio mengi. Kitu mimi nataka nikimoja. Tuifuate Katiba ya mwaka wa sitini na tatu, hiyo Katiba haikufanya kazi hata kigogo. Hali ya umoja imetushinda sisi wa Kenya wote kwa jumla. Kwa sababu ukiangalia vile mambo ilivyo, umoja huu umetusenyeta sana nguvu hatuna kila kitu wambeba wakapeleka Nairobi. Pipeline Headquater Nairobi, Port Headquater Nairobi, Oil Refinery Headquater Nairobi, Title deed za ardhi zote Headquater Nairobi huu ni unyonyaji. Hivyo vitu vyote vinastahili kurundishwa Coast Province pale mahali vimetoka **(clapping)**.

Jambo lingine nasema ya kwamba mjue ya kwamba serikali ya umoja imetunyanyasa vibaya sana. Ikiwa itaundwa Katiba munayounda sasa na ikiwa watu kule watakataa kuunda ardhi ya majimbo hii Coast Province itatoka Kenya. Na maana yake ya kutoka Kenya ni haya: Sisi watu wa Coast Province tumetawaliwa karibu mara tatu. Kwanza, tumetawaliwa na Wareno, watu Wakenya walikuwa hawapo waliotawaliwa ni Coast Province pekee yake. Pili, tumetawaliwa na Warabu, watu wa Kenya walikuwa hawako hapo waliotawaliwa ni Coast Province pekee yake.

Tatu, alipokuja Muingereza bendera yake ikawa juu naya Mwarabu ikawa chini ina maanisha tumetawaliwa mara ngapi? Mara nne kwa hivyo inamaanisha hii Coast Province sio Kenya. Hii Coast Province ni mwita Mombasa (**clapping**). Naeleza kweli kweli kabisa hii Coast Province ni mwita Mombasa sio Kenya. Na ikiwa mutakataa kutengeneza hali ya majimbo tutainyakua Coast Province. Kwa hayo machache asante sana**. (clapping**).

**Com. Swazuri**: inaudible

**Musa:** Salaam aleykum. Mimi majina yangu kamili naitwa Musa Sundieya. Na niko hapa kuwakilisha kikundi cha Professional Group ya South Coast na tuna memorandum yetu hapa. Mwisho kwa sababu mambo mengi hapa yamezungumzwa hawa professionals Kwale Professional Forum nao pia wanasema wanataka majimbo **(clapping).** Nataka kuumunga mzee aliyetoka hapa sasa hivi kwamba Kenya tumetawaliwa hasa hapa Coast tumetawaliwa. Nataka kumuongezea hatukutawaliwa tu mara hizo alizozitaja bali mpaka sasa tunatawaliwa. **(clapping**). Kwa sababu ma PC, Ma DC wote sio watu wetu na kwa hivyo tumendelea kutawaliwa ambacho Coast hatujapata Uhuru **(clapping**).

Maswala ambayo yamezungumzwa ni yale yale kila mtu anazungumza. Kwa ufupi, maswara ya ardhi yametanjwa na watu wa Kwale Professionals wameitaja. Hii memorandum iko mtasoma wenyewe. Tunasema ile sheria ya kwamba mtu anamiliki ardhi tu hapa juu, chini si kwake hiyo ni sheria ya unyanyasaji na Kwale Professional Forum wanataka mtu anaye kuwa na ardhi anamiliki ardhi yote mpaka chini **(clapping**).

Tunataka pia hiyo halali kwamba title deeds zinatolewa huko kwa Commissioner of Lands imetunyanyasa na tumekosa ardhi zetu nyingi. Kwa hivyo tunataka maswala ya ardhi yangaliwe hapa hapa katika sehemu zetu.

Utalii ambayo ni chumbo kubwa sana kwa hii serikali tumeona wazee wengi wamesema course ziko kule za Kenya Utalii College, sisi hapa kwetu tumeambulia yale maafa ya maradhi ya ukimwi n.k. uchumi wote unaenda. Tunasema tunataka majimbo kwa sababu tunataka hali hizi tuzimiliki wenyewe uchumi unapatikana katika utalii asilimia kubwa ifaidi watu wa coast. (**clapping**).

Tunasema pia elimu ni chombo mhimu sana ambacho kina leta manufaa katika nchi. Kama alivyosema Prof. Ali Mazrui, Coast are the people who went to school but the last to graduate. Watu wa Pwani ndiyo wa kwanza kuenda shule lakini ndiyo wa Mwisho kufaulu. Na tunasema hivi kwa sababu serikali hii haina haya mpaka sasa Coast Province haina chuo kikuu hata kimoja. Hiyo ni kwa sababu ya kuondeleza unyanyasaji na kwa hivyo sisi tunataka majimbo kwa sababu tunataka kuendeleza mambo haya nasi pia tuyapate. Kwa sababu yaliyosemwa ni mengi, Polisi force imetajwa corruption na ni kwa sababu hatuna uwezo wa kuwachagua wale wakuu wa polisi. Tunasema Katiba hii ya sasa ambayo tunaitayarisha sisi wale Police Chiefs tuwe tuna uwezo wa kuwachagua **(clapping**).

Kwa sababu mambo haya yote yamezungumzwa tunataka kusoma tu conclusion ya hawa Kwale Professional yale yote ambayo yametajwa ni mambo muhimu na sisi tumechoka kiasi kusubuliwa na kunyanyaswa na serikali hii ya Central Government. Tunasema twataka majimbo haraka iwezekanvyo. Asanteni. (clapping)

**Com. Swazuri**: inaudible

**Salim**: Arabic greeting. Kwa kweli meni yamezungumzwa kwa majina kamili naitwa Rama Salim Jasho. Ni mwenyeji wa hapa hapa Diani. Mengi yamezungumzwa lakini kulingana na hali Kenya ilipata uhuru katika Katiba ya majimbo kwa hiyo tunasema tunataka majimbo. Majimbo ni lazima kwa kila Mkenya.

Pili, nasema kama watu wa mikoa hiyo minane wata kataa kutoa kushirikiana na sisi kwenye katiba ya majimbo, tunataka mwambao wetu wa Pwani. Mwambao wa Pwani umetuifadhi sana, umeifadhi sheria zote za ki-islam mpaka mambo ya ardhi na nini na nini. Kwa hiyo tunasema mwambao wa Pwani uwe unatufanyia kazi. Kwa upande wa mawala ya elimu hapa kwetu

Coast Province hakuna hata shule moja ya kitaifa licha ya kuwa na vyuo vikuu, hakuna hata shule moja ya kitaifa. Kwa hivyo tunataka tupate shule za kitaifa hapa na vyuo vikuu katika hapa Pwani.

Tukiangalia mambo ya ardhi –ardhi zimegawanywa sana sana mpaka kiasi ya kwamba zile za lease na nini, watu wa Pwani wananyanyaswa nazo hawapati, hawapati. Kwa hivyo tunataka jimbo liwe litatushughulikia kwa mambo ya ardhi tu. Na upande wa elimu tunataka kuanzia class one mpaka class ya nane iwe ni bure na pia secondary school mpaka form four iwe ni bure. Kwa sababu wazazi wengi hawawezi kulipa pesa nyingi, wengi wao wamekuwa ni masikini hawana pesa za kutosha. Kwa hivyo inatakikana elimu iwe ya bure, mahospitali pia yawe ni ya bure kuhudumia wananchi kwa sababu mtu ataenda hospitali kulipa pesa na hana pesa itabidi, anaumia. Kwa hayo mengi ninasema tunataka majimbo na mwambao wa Pwani tuupate. Asante.

**Speaker:** Salaam aleykum. Wana Commissioners, wananchi salaam aleykum. Kwanza ninalofuata hapa. Serikali ya majimbo halafu katika hiyo hiyo majimbo tuwe kila jimbo linauwezo wa kufanya mambo yake. Kwa upande wa serikali, iwe ya parliamentary. Serikali hiyo iwe na nyumba mbili upper house na lower house. Halafu katika hiyo hiyo serikali iwe na Rais ambaye atachagua Prime Minister. Na huyu Rais ni kama ceremonial, President I mean lakini anapeana mambo yote kwa Prime Minister ndiye anaongoza serikali.

Kwa upande ya mahakama. Mahakama ziwe mikononi mwa kila jimbo, iwe na mahakama yake na kila dini iwe na mahakama yake sio mambo ya kuchanganyana na vile vile kama walivyosema wenzangu, kitabu cha Koran katika hizo mahakama kitolewe kabisa kwa sababu hicho ni kitabu kitakatifu kwa hivyo hakifai kwenye hizo mahakama. Kwa kuongezea pia katika hiyo mahakama hizo sheria za kuinamia huyo Bwana, ama huyo Judge pia zitolewe

**Speaker**: Hata mimi kwenye elimu nataka elimu ya bure kuanzia std one ama kuanzia nursery mpaka std 7 ama 8. Na pia nataka ile system ya zamani sio hii ya 8-4-4 hiyo hatusaidii chochote. Kwa sababu hiyo 8-4-4 imefanywa na hakuna chochote. Katika hizo skuli hakuna instrument za 8-4-4 sasa imekuwa ni mchezo tu. Kwa hivyo hatuitaki twataka ile ya zamani.

Ardhi. Ardhi kama iliyvosemakana imekuwa tatizo sugu, tunataka mambo yote yaje kwa province mambo yote tufanyie hapa

kuanzia Chairman wa village mpaka kufikia hapo. Mambo ya title deeds pia kuna haja watu baada ya serikali ijayo zifutiliwe mbali tuwe na nyingine maanake hizo zote ni fake. Watu wengine wote wamechukuwa za fake si haki zao (**clapping).**

Kazi. Kazi zimekuwa sugu hapa watu wamesoma na hiyo swali ya kuwa watu wa Pwani wasomi ni uongo kabisa. Mimi nafanya kazi huko na mimi na train watu wametoka huko. Ametoka utalii na namsomesha mimi, sikuenda utalii lakini na - msomesha mimi. Kwa hivyo huku kusoma ati mpaka utalii ni uongo. Hata hawa ambao hawakusoma wanafanya hizo kazi za utalii. Na anazungumza hiyo hiyo lugha ya kizungu na naelewana na muzungu na hakusoma. Kwa hivyo mambo ya kusoma hiyo sioni kuwa hiyo ndiyo tatizo. Hakuna tatizo mtu yeyote aliye na akili timamu anajua kufanya kazi. Kwa hivyo lazima kazi tukipata, majimbo tutakuwa 75% lazima itoke hapa kwa sababu 75% nina hakika wale wamesoma, hawakusoma watapata kazi. Hivi vyeo vya Ma-manager, Personnel na vinginevyo vingekuwa ni zetu saa hii. Lakini kwa sababu ya ubwenyenye mambo yote hayo yameleta chuki. Kwa hivyo majimbo that's the solution majimbo. Sina mengi (**clapping**). Serikali ya majimbo ndiyo itatoa matatizo yote Kenya hii.

**Com Swazuri:** Mohammed Chandugu, na ….. Omari awe tayari

**Mohammed:** Arabic greeting. (interjection inaudible) Mohammed Omari Chandugu. Kitu cha kwanza nataka kuuliza je hii Tume hii haya mambo tunayoulizwa ni ya usawa? Nasema hivi hii tume ambayo imekuja hapa kutuhoji ya maoni ni ya ukweli yale tunazungumza kwa yanakiliwa kweli au ni (Com. Swazuri responds inaudible) Sasa mpaka ni ulize kwa sababu inaweza kuwa tunalopoka halafu hii mambo inafutiliwa mbali (noise)

**Com.Swazuri**: Tumeingia hapa kusikiliza maoni ya wananchi tumetoka Nairobi kuja hapa…. Baada ya hapa …… Mimi nataka kuhakisha tu kwamba ameuliza hili swali kwa sababu ana wasi wasi kweli au aiuliza tu for the sake. Kwa sababu tumeeleza mara nyingi sana tunaendelea kuwa elezea hapa. Serikali na Bunge zimetumia muda mrefu sana kwa sababu watu wame ilawa sababu ya jambo hili. Watu wengi hawako sasa. Katiba tunaandika lakini wale walianza fujo ili pia hawako wako makaburini. Kwa hivyo si neno la mchezo. Tumekuja hapa kufanya neno la muhimu sana. Tulieleza wakati wa vile vikao za mwanzo ya kwamba baada ya sisi kukusanya maoni hapa tutaenda kuandika ile report na tutarudi tena hapa kwa miezi miwili kila mtu apewe nakala yake angaliwe kama aliosema yame andikwa la. Hiyo ni sheria ambayo imetuleta hapa. Kwa hivyo mtu

asiseme kwamba labda haya tunayosema wanatuhilibu wale wanaandika halafu yataenda yaishe. Hapana. Sheria ambayo tumewasomea tuliwambia baada ya hapa tutakuja na ile mswaada ambao tumeandika mukae nayo miezi miwili kila mtu aandike vile amesema pana hii section wamesema makosa hii hatukusema hivi na hivi na tutakuja tukae na nyinyi. Kwa hivyo mtu akija hapa ajue kwamba hili ni neno linaendelea Kenya nzima. Sawa? Haya.

**Mohammed:** Kwa hivyo ndugu msinielewe vibaya kwa sababu sijajua nataka uhakika (noise from crowd) endelea bwana. Haya kitu cha kwanza ni hivi mimi nataka majimbo kwa sababu majimbo ndiyo yataleta usawa wa kila mtu. Hivi tunavyotembea hatuna uhuru kama mimi kutoka nilipozaliwa mpaka sasa sijui maana ya uhuru ni nini. Mimi najua watu kuishi tu. Kwa hivyo, hiyo majimbo nafikiri naenda nikajijua iko wapi na iko vipi na inaish vipi.

Nyingine ni kuhuzu ajira. Ajira tuna enda kule mahotelini kutafuta makazi ukifika pale kitu cha kwanza unaulizwa wewe ni kabila gani? Ukisema mimi ni Mndigo unaambiwa hwa ni watu wa kayambogo unakosa kazi, lakini ukienda mtu mwingine ambaye si Mndigo mkiwa naye akiwa mble yako au nyuma wako yeye atachulikuwa kazi wewe utarudi. Ukija nyumbani baada ya siku fulani unasikwa unapelekwa kotini na unafungwa. Wewe sio mfutaji utashikwa. Ukiwa mvutaji au usiwe mvutaji, utashikwa. Nafikiri sina zaidi ya hapo. (**clapping**)

**Com. Swazuri:** inaudible Hadi Mwanguo

**Mwanguo**: Mimi kwa jina ni Hadi Saalim Mwanguo, na mimi ni politician. Mimi kwanza kabla sijaeleza chochote nina omba nyinyi Macommissioner ma Officer mumekuja, mimi ninataka majimbo, kwa sababu hii. Sisi kama waKenya na kama ananchi wa sehemu hii tuna mambo mengi sana ambayo wenzangu wamezungumza kwa wingi sana lakini mumeyapata. Na ukwweli ni kwamba sisi twataka kama ni ukweli, serikali yataka mabadiliko iwe ni ukweli kwamba majimbo ni lazima ya patikane (**clapping**). Isiwe tu ni propaganda. Propaganda hiyo imetuchokeza kwa miaka thelathini kama na minane. Na hiyo sisi twaumia na kumbe ni maneno tu.

Kwa hivyo langu la kwanza ambayo nataka serikali hii ya majimbo ikipatikana sisi upande wetu twataka hizi kazi kuhusu mahotelini kuhusu kazi zile kubwa serikali irekebishe. Kwa sababu watu wengi kama sisi Wadigo tumesoma kama vile vile

wenzetu na kama ni upande wa ma-DO, Ma-DC wakubwa wa walimu wako vijana wamesoma vizuri sana. Lakini ajabu ni kwamba, kuna watu wengi sana ambao ni kitoa mfano kama hapo Post Office yuko mzee mwingine amesoma mpaka form 6 na sasa afanya kazi ya mataai hapo sasa amechaakaa pale pale. Elimu hiyo imekwisha wako vijana wamesoma mpaka form 6, form 4 elimu hiyo imekwisha. Kwa hivyo ninaomba serikali kwamba, maswala kama hayo ya kikazi kama zile za husika kama vile ma-DO na mengineo, yarekebishwe.

Upande wa Urais, lazima upande huo wa rais kama serikali ya majimbo tutapatiwa ama twataka, lazima madaraka fulani katika upande wa urais upunguzwe upatiwe wengine ambao pia wana uwezo wa elimu kama hizo.

**Com. Baraza**: Upewe nani?

**Mwanguo:** Upatiwe kama vile waziri mkuu na Ma-Governor ……….ama Waziri mkuu. Kwa sababu nisije nikakosea au Bunge eh. Na kuhusu tatizo la upande wa ardhi kama vile watu wengi hapa wamezungumzia kwamba ardhi hapa ni tatizo sugu. Lakini sisi tutasema kwamba kama plot zile zinagawanywa ama pahali panagawanywa mimi ninaomba serikali hiyo ya majimbo kwanza kuwe kuna wazee kule shina waangalie ni nani anaweze kupata plot pale. Je, ni mtu pale amelima, amendumisha vitu kama vile minazi, mikorosho, miembe apatiwe yeye kwanza. Si ardhi hiyo mtu amelima miaka ishirini amekuwa na mvi pale mtu akitoka huko na karatasi asema hii plot mimi ni yangu. Sitakabadhi kama hizo ndizo ambazo zatatiza wananchi wote hawa. Na plot nyingi zimechukuliwa kwa sababu ya kutoangalia kimakini hilo tatizo. Kwa hiyo unakuta plot kama hizo zinagawanya mara tatu na hapana jibu.

Jingine ambalo tunaliomba kama serikali ya majimbo itapatikana ninaomba kuhusu mambo ya baharini kule kwa mfano kama vile vijana wanatembea kule wale ambao ni makamu, ukienda pale chini tu ukizunguka zunguka washikwe; unaambiwa wafanya nini hapa? Lakini utakuta kabila nyingine pale bila kufichana kabila hiyo hiyo inaendelea pale ama akishikwa akipelekwa polisi utakuta kwamba hakuna lolote lakini Mdigo anasajiliwa kwamba yeye ni mwizi ama ni mvutaji bhangi, ama ni mvutaji unga, swala kama hilo ni lazima tuliangalie.

Swala lingine, upande wa dini ya Kislam mambo ya achiliwe Waislam wapange mambo yao wenyewe. Nasema Waislam mambo ya Waislam wachiliwe wao wenyewe wapange vile wanataka. Kama ni sheria wapange wao wenyewe vile ambavyo

wataka. Si leo ni mwezi ishirini na tisa lakini wambiwe siku kuu ni tarehe moja ambapo haiendi hivyo. Mwezi mara ingine watoka tarehe ishirini na tisa watoka thelathini au mwesi mara nyingine itakuwa ni jumatatu lakini mnaambiwa lazima muswali jumannee. Swala kama hilo serikali iaachie Waislam wenyewe ndiyo wataangalia kuhusu hiyo mambo.

Kuhusu mambo ya uchaguz. Sisi twaomba serikali ile ya majimbo kama itakuja tunaomba kama mambo ya kura katika vituo, kama kituo kimesajili watu ishirini na tisa, ama thelethini au arobaine iwe ni hiyo hiyo watu wakipiga kula wale watu thelathini na tisa zihesabiwe pale pale na zinjulikane ni hizo thelathini na tisa si mandebe nyengine yaje hapo. Twaiomba serikali ya majimbo ilekebishe swala kama hilo kwa sababu linatatiza viongozi. Mtu ameanguka lakini anaambiwa huyu ameshinda kwa hivyo swala kama hilo liondoke kabisa. Swala jingine…

**Com. Swazuri**: nakupatia dakika moja tu.

na rudia upande wa mikahawa hapo chini. Uandishi wa kikazi lazima ulekebishwe na uwe sawa na vile ambavyo wananchi pale wako. Kwa mfano sabini na tano iweko na ishirini na tano sisemi ule ukabila uweko, la. Lakini wenyenji wa pale wawe ni sabini na tano kwa ishirini na tano hili swala liangaliwe. Kwa hayo machache nawashukuru niko na mengi lakini ……….Niulize mama.

**Com. Baraza**: Unasema kwamba beach boys watoto wa Kidigo wakienda huko wanafukuzwa?

**Mwanguo**: Wanfukuzwa ama wanashikwa.

**Com. Baraza**: Wanakutafuta wewe ni Mdigo wanakuto?

**Crowd**: Ni hivyo.

**Com. Baraza:** Kweli munaniambia maneno ya ukweli?

**Crowd**: Ni kweli kabisa

**Mwanguo:** It’s a 100% na hii ni swala ambalo la tuumiza.

**Com. Baraza:** Kama ni Mluhia ana achwa hapo

**Crowd:** Kabisa

**Mwanguo:** Huna uhuru (noise) na hilo ni swala ambalo ni wazi. Uliza wananchi wenyewe hao. (noise from the crowd)

**Com. Swazuri:** Asante Sana.

**Fatuma:** Salaam aleikum. Mimi kwa jina naitwa Fatma Salim Kizumu, mzaliwa wa hapa Diani Gombato Sub-location. Mimi nataka majimbo. Majimbo yenyewe tunayotaka natoa mfano kidogo sana. Iwe ile 80% ikienda kwa wenyewe, wenyeji wa hapo jimbo 20% iwe ya serikali. Halafu maoni mengine ni kama haya kuna sehemu za kikazi hutoka kama za polisi hivi kuchukuliwa Kwale. Naomba iwe wenyeji wa hapo hapo Kwale wachukuliwe kwenye jimbo lao yaani mfano kila watu wachukuliwe kwenye jimbo lao. Halafu kuna mfano hivi ngereza na youth. Naona hizo sio kazi ngumu sana za kuchukuliwa watu kutoka jimbo lingine, watu wenyewe wa jimbo hapo hapo wawe wana miliki mambo yao youth wasimamie wenyewe na ngereza wasimamie wenyewe. Hiyo mifano kidogo kuhusu jimbo.

Halafu kuna hii mambo ya kidini, tumeachwa nyuma dini ya kiislam. Pia kuna haki zetu zingine kuhusu mambo ya Kiislam. Tukifelewa na mabwana zetu kuna msiba ambao huitwa heda. Lakini vile ilivyo ndini ya ki-islam imeachwa nyuma mama huyo atalazimika avae mijilemba yake hivyo hivyo aende kazini. Sisi twaomba Katiba ya Ki-islama wapewe hizo off kukaa nyumbani vile miezi mine na siku kumi na serikali imlipe ikiwa ni mfanyanji kazi vile vile kama maternity leave, ambavyo mtu hulipwa. Halafu lingine, tuna vasi letu la Ki-islam kama bui bui na hijabu. Tusilazimishwe kuvua buibui na nijabu kazini. Mtu avue akitaka mwenyewe lakini isiwe lazima. (**clapping**)

Point nyingine ninasema kuna zihinati na mahospitali yaletwe vijijini karibu na wananchi na madawa yawe ya bure na madaktari wawe qualified. Halafu jingine kuhusu elimu. Twataka elimu ya bure kwa sababu twataka watoto wasome lakini wengine hawana uwezo. Elimu hiyo ya bule yaanzie kutoka primary mpaka university. Hiyo jambo liangaliwe na serikali**.** **(clapping**) Halafu lingine nasema MPs na Wabunge watawale wakianza miaka thelathini na tano eeh MPs na Councillors, sorry, wawe na miaka thelathini na tano ndiyo waongoze. Na kuongoza kwa hivi ambavyo twa wapigia kura miaka mitano. Miaka mitano

huyo Councillor na Mbunge huyo ikiwa hakutekeleza yale ali promise wananchi, ikiwa haija fika miaka mitano afanyiwe kura ya kutokuwa na imani (interjection inaudible) eh, ikiwa hakufanya vile alivyogana na wananchi amefanya tu miaka miwili mwaka wake moja ameona eh ni yeye tu, tumpigie kura ya kutokuwa na imani naye (**clapping**).

Halafu twataka machief wachaguliwe na wananchi wenyewe, na chief atawale akiwa na miaka thelathini na tano. Chief huyo akiwa hakuridhisha vile ambavyo mwenendo wake waenda na wananchi kuwe na committee ambayo itaungana iyangalie mizozo ile. Ikiwa hawezi pia na yeye atolewe sio amilika pale kama nyumba yake na wawanyanyasa wananchi (clapping). Jingine twataka viti ya bunge na council (nominated) vitengewe akina mama. Jingine Kadhi court twataka Kadhi ambaye ameilimika ki masomo ya ……

**Com Baraza**:……. (inadible) mama nominated na nani?

**Fatuma:** Mama, twataka ile nominated Councillor iwe mama na MPs wawe akina mama nominated na vile vile.

**Com. Baraza:** Percentage gani?

**Fatuma**: All. Wawe watachukua zile zingine sisi ni nominated.

**Com. Baraza**: Hizo ni kidogo tu. They are very few.

**Fatuma:** eh basi haya tuaangalia twaweza kuongeza twaenda Lunga Lunga twaweza ongea vingine tukaongeze huko.

**Com. Baraza**: (inaudible) peopla are murmuring.

**Fatuma**: eh, sawa lakini twataka hizo ndiyo tumeonelea hizo nominated mbili za tufaa sisi wanawake. (**laughter**) Kadhi court twataka yule amesoma dini yake na amesoma kizungu na Kadhi awe amechaguliwa na Waislam wenyewe, yule Kadhi **(clapping**). Halafu kuna hawa watoto wa kiume na wa kike. Mtoto wa kiume anaporinga mtoto wa kike alazimishwe family ile ya yule mtoto alieringa mwenzakie amfundishe yule na akizaa mtoto amulee mpaka miaka kumi na nane. Alazimizwe hiyo ni lazima mtoto wa kiume akiringa mwenzake si aachiliwe tu hivi hivi. Halafu twataka hizi university na vyuo vikuu vije pia Pwani kama Utalii. Utalii wote naona uko Pwani sasa ikiwe Pwani kwenyewe kuko na Utalii hakuna chuo, chuo si tuletewe university

hapa na utalii. Sina mengi shukurani (**clapping**).

**Com Swazuri**: Fatuma Hussein, atafuatiwa na Hamed Mwaluda, Mohammed Juma.

**Juma**: Arabic greeting. Bw. Commissioners kwa bahati mbya yangu mimi nilikuwa nimeandika kwa lugha ya Kiingereza lakini nimeifanya kwa ufupi kwa lugha ya Kiswahili. Nitakwenda haraka haraka. Jina langu ni Mohammed Juma na mimi ni Secretary Majili Isilamia, na pia ni mzaliwa wa Kwale District, Wasini Island. Kwanza ningeeleza masitikiko yangu sana kuona kwamba katika location yangu. Kilimo kwanza location, mpaka kufikia Msambweni hapa ukienda Vanga mpaka Majoreni most of the people are not aware of this exercise.

**Com. Swazuri:** (inadible)

**Juma:** Hiyo ni habari na kupa bwana. Si kwamba mimi nasema ni vipi mimi ni habari na kupa kwamba hakuja tokea education huko. Kwa hivyo watu ku-participate ni vingumu. Mimi ni bahati nzuri tu ni mtu wa kuishi huku nimeyajua haya. Kwanza ningependa kusema kwamba kubadilisha ama kurekebisha Katiba ni haki ya kila mwananchi. Maelezo katika Katiba ambayo tunayo hivi sasa imekuwa kidogo ni vingumu kwa sabau wengi wetu hatukupata nafasi ya kujua Katiba inasema nini. Lakini wengine ambao wamewahi kujua basi wao watafanya kwa niamba yetu.

Jambo la kwanza ningeeleza kwamba ardhi za zamani wakati wa ukoloni, kama miaka mi mbili au tatu iliyopita utaona kwamba karatasi za kumiliki ardhi wakati ule ilikuwa ni vigumu kwa Mafrika au Mkenya wowote wakati ule kujua kwamba hiyo ardhi ina maana gani. Wale waliotutawala wakati ule waliwahi kujua kwamba ardhi ni nini, kwa hivyo wakati huo walichukua hiyo nafasi kwa ule ujinga wetu na wakawweza kuandika ardhi kwa ma miles. Yaani mtu amepata ardhi ya mamiles kama tano au sita na wenzake wako hapo wakiishi katika ardhi hiyo ambayo yeye hajui maskini hiyo ardhi ni yake. Basi imekaa hali hiyo ni yake mpaka sisi tuakapata uhuru 1963.

Haya sasa '63 sisi tumepata uhuru karatasi ile ile ambayo ameiandika wakati huo imekuwa ina dhamani ina weza kutumika wakati huu kunyang'anya ardhi yako wewe ambaye ulikaa pale miaka mia mbili. Mimi ningeona maoni yangu ni kwamba, yule

aliyefanya tu wakati huo na sasa leo tuna uhuru, karatasi zile zote zingekuwa hazifai. Ardhi yote iwe nullified na iaanze kupimwa upia na kila mwananchi na right ya kuwa na ardhi kipande kile kikiwa chake wakati ule babu zake waliishi miaka mia tatu. Hiyo ni lazima izingatiwe kwa katiba hii inabandilishwa sasa, kwamba ardhi zile zote zilizomilikiwa na watu wengine awe Mwarabu, awe Mzungu, awe Muhindi awe Government, hata iwe Government alright Government land, mimi nimeishi hapa miaka mia tatu baba yangu, baba nani kila mtu ameishi hapa leo ardhi hii sasa baado itakuwa karatasi ni zile zile mimi nafanya nini katika ardhi hii utafanyaje. Question of squatters haitaisha ni the Coast province and everywhere in the nation. Haishi mpaka ardhi zote ziwe nullified, halafu zipimwe tena na kila mtu apate haki ikiwa mimi ni mzaliwa hapa nini haki kupata hata kama ni acre tano. Pia iwe ni rule kwamba kila mwananchi aweanaweza kumiliki ardhi.

Ya pili ni security. Kumetokea kesi nyingi sana za mapolisi kushika watu na kuwatia ndani wakabaki siku mbili au tatu unatolewa na unaenda unaambiwa basi enda tumesha chunguza huna neno na huwezi kustaki popote kwa sababu act yenyewe imempa polisi nafasi hiyo ya kufanya hiyo. Kwamba anaweza kusikia mtu amuweke wiki moja akichunguza halafu kwa hivyo kanuni kama hizo zingeondolewa mwananchi yoyote ambaye anafaa kuchunguzwa basi iwe kwa masaa labda au siku nzima jioni anaachwa lakini wanatiwa ndani pengine ni monevu na kutolewa kwako lazima upeane pesa, kitu kidogo halafu ndiyo unatoka. Mambo kama haya yangeangaliwa.

National identification imetokea tabu kubwa sana kwa wananchi kupata kitambulisho au kupata karatasi ya kuzaliwa au kupata passport maswali ni mengi sana. Na ofisi ambazo unafaa kuenda ni nyingi sana. Unaenda mara kumi tano mpaka unachoka wewe mwenyewe njiani. Kama mwaka nzima unangoja ID card hujapata au Birth Certificate hupati au passport nayo pengine yatokee maswali madogo madogo unaambiwa wewe hufai kupata. Sasa maswali kama hayo yanawapa nafasi watu wengine kama Ma-officers katika ofisi za identity card ofisi za ma passport ofisi za birth certificate watu kupata njia ya kupata pesa. Kwa hivyo lazima serikali ingeangalia mambo kama haya yaondoke kabisa kusiwe na masharti mengi sana ni kuwe na uhakikisha tu wa kujua huyu ni mwananchi amezaliwa hapa imetosha na watu wakuweza kutosha hayo wako. Wako waalimu wa area hiyo, ma Kadhi, wako ma Chief na wengineo. Mambo kama haya madongo madogo basi lakini sasa unatabishwa mwaka.

Judiciary services: katika makoti yetu tulionayo tumeona pia vile vile kuna njia nyingi sana ambazo zinatumika baina ya Polisi

na ma Koti halafu watu wengi wanakosa haki zao hawazipati haki kama una ukweli kisawa sawa kwa vile huna pesa za kuhonga hapo basi unakosa.

Pia tungependa kusema ju ya ibaada. Ibaada ni lazima kwa sisi wote kwa wale wasio kuwa Waislam na sisi Waislam. Lakini sisi Waislam tunalia kwamba, somo letu la dini limewekwe katika syllabus ya kusomeshwa mashule. Kutoka Primary, secondary mpaka university lakini halikupanuuwa baada ya syllabus kutolewa basi vitabu havitungwi kabisa hakuna kitabu chochote cha kuweza kusomesha dini katika madarasa kutoka std one hadi std 8 halafu wakifika form 4 kuna vitabu viwili au vitatu. Kwa hivyo ule mwanafunzi yoyote hakuweza kuenda Madras labda akitumaini tu atasoma ma shule haitoshi. Kwa hivyo somo hilo tungesema Ministry of Education iyangalie sana.

Basi la Mwisho ningesema kwa vile naona ni muhimu sana nasema elections. Elections ziwe namna hii. Kwanza iyanze civics wachaguliwe Macouncillors kwanza halafu ndiyo waje Wabunge halafu baadaye President. Haidhuru hata kama ni mwezi lakini tujue kwamba ni tofauti kwa sababu tukiweka pamoja fujo linakuwa jingi na hali ya kuhongana inazidi sana Asante**.(clapping**)

**Hamisi:** Kwanza wananchi salaam aleikum. Mimi jina langu naitwa Hamisi Mwalimu Mombagizo former Councillor Kiundo location, na nimejifanya nisiwe nyuma kwenye haya marekebisho ya Katiba. Na malengo hasa ambayo kama mkeleketwa wa Pwani ningeomba serikali yetu ikubalie mkataba wa majimbo. Majimbo yawe ya utawala, majimbo yawe ya uchumi. Tujitawale na tujue kwamba chumi zote ambazo ziko hapa kwetu tunazipata.

Pia jambo jingine ambalo pia nimeliwaza usiku kutwa, nimeona ya kwamba majimbo hayo tuwe na Rais na Waziri mkuu katika jimbo. Na qualities ambazo nilifikiria za Rais ambaye nataka awe kwenye serikali hii , yetu ambayo tuna .. tunatamanisha hii jambo la majimbo, awe na sifa zifuatazo: Rais awe mzalendo, awe mwenye sifa nzuri, umri miaka thelathini na tano na zaidi, elimu yake iwe ni mtu wa darasa la form 4 na zaidi. Mwenye degree ya utawala na uchumi na mambo ya economy. Mwenye uwezo ya mali. Tusichague mtu ambaye yeye mwenyewe ni maskini ndio munona saa hii mali zitu pesa zinaletwa za IMF, pesa zinamalizwa kwa sababu ni mtu ambaye hakutosheka. (**clapping**).

Jambo jingine ambalo pia limewaza awe mwanachama wa chama ambacho kimeandikishwa ma kimesajiliwa. Pia asiwe ni

mbunge huyo ambaye mimi nataka mimi. Asiwe ni Mbunge. Asiwe juu ya sheria wala mamlaka zaidi awe ana uwezo wa kushtakiwa **(clapping**). Pia jambo jingine ambalo nimewaza, tunaomba serikali yetu ambayo tunataka tudumishwe kwa Katiba iwe serikali ya demokrasia kwa sababu saa hii hatujui kama hii serikali yetu inaongozwa na demokrasia au ni dictatorship (clapping). Hatujui maanake tunapelekwa tu. Maanake unaweza kusikia mtu sinjui amefanywa nini huko, na hiyo likifanyika hakuna chochote kinafanyika. Kwa hivyo, ningependelea serikali yetu iwe ya demokrasia ambayo mwananchi atakuwa na uwezo zaidi.

Jambo liningi ambalo mimi napigania U-councillor na kuna mwingine anapigania Ubunge. Kitu ambacho ningpenda, mbunge achaguliwe kwa miaka mitano lakini kuwe na kifungu cha sheria ambacho wale waliomchagua wanaweza kumkataa ikiwa uongozi wake sio mzuri (**clapping).** Na hiyo inaingiliana kwa wabunge na wale ambao wanachaguliwa ktiaka mabaraza ya wilaya.

**Com. Swazuri**: Na rais?

**Hamisi:** Rais ndio nimtanja awe ni mtu ambaye qualification yake nimetaja hapo. Na uweso wake pia kiboko yake ni mwananchi. Jambo lingine ambalo limtajwa ni wasemaji wengi ni habari ya mambo ya ma-squatter. Ni dhambi mpaka sasa tunasema tuko huru na wengi tuko squatter. Maanake ikiwa wewe ni President utakwenda ulizwa ulikaa aje kwenye serikali yako? Sasa ikiwa watu wengine wanalia wanasema ni squatter na kutoka 1963 tulipopata uhuru mapaka leo wengine wanalia. Mtu hajui title deed ni nini, anasikia tu, mpaka uwe na title deed wengine wanashangaa wakifika kwenye court wanaambiwa dhamini kama uko na title deed wanashangaa. What is the title deed?

**Com. Baraza**: How many of you are squatters?

**Hamisi:** Majority of them. Everybody.

**Com. Baraza:** Hamna title?

**Hamisi:** Hatuna title (noise). Jambo lingine ambalo pia nilifikiria, uchumi watu uregezwe kwa kufufuliwa viwanda vyetu ambavyo zimezikwa. Viwanda mfano, tunaambiwa ardhi yetu ya Pwani ya Ramishi haifai. Nani alienda kwa Mungu

akazungumza na Mungu akapata haya maneno? **(clapping**) Kwa hivyo, hivyo tayari mtu atakwenda ulizwa kwa nini uliwandanganya watu wa Pwani ya kwamba ardhi yao haifai. Sasa tuna korosho tukiangalia sasa hii tukitembea huko kwenye miembe huko twaona maembe mainzi. Na sababu ni kuwa hakuna viwanda. Kwa hivyo tunapenda majimbo na viwanda viwe ni vingi njugu. Tunashukuru ardhi yetu kila kitu tunachopanda kinamea. Kwa hivyo vitu vyote tunapenda, hata juzi nilisikia ile Bamburi pia wanataka kuhamisha wapeleke bara (**clapping**). (Interjection inaudible) Sasa ikiwa wamehamisha sisi tutakuwa tunamaana gani? Hatuna maana afadhali haya mambo yaje majimbo ndio kiboko yao.

Mheshimiwa bado moja. Namaliza hili moja mwenga na hili ndilo hasa utu wetu wa Pwani. Bahari yetu isiwe na mpaka ( **clapping**). Kuna watu wengine wanasema tunataka tuweke marine park. Mungu mbona hakuweka marine park. Hawa samaki Mungu ameleta tutumie kama chakula sio fashion ya watalii (**clapping**) Smaki tunataka wake wakubwa nasi tuwavue, tule, tujisike kama ni watu ambao tunajisikia na samaki. Kwa hivyo bwana Swazuri, nafikiri, wajua ninamastikiko wakati nakuja huko njiani wengine wana sema …….. ah Katiba imeisha nyinyi muanenda tu kuwekwa sawa isiwe hivi. Kitu ambacho naomba, Katiba na tunasema maneno yetu hapa, haya maneno yetu wakati Katiba ikikamilika tutumiwe. Very good. Tutumiwe hata kama ni vitabu tusome neno hili …… Mombagizo ulisema nini hapa eh …. Asanteni sana. (**clapping**).

**Nzeki:** Salaam aleikum. Mimi niko na maneno mawili tu. Kwa majina naitwa Peter Nzeki. Ni mkaazi wa hapa Diani, mzaliwa kutoka sehemu ya Nguluko center huko Shimba hills. Mimi niko na maneno mawili maanake mimi ni mkulima na unajua mkulima ako na mambo mengi sana. Tukiangali upande wa kilimo, kilimo chetu katika Kwale district hakijawekwa maanani kabisa tunalima korosho, kuna rangi, kuna nazi lakini hazitambulikani kama ziko. Na tukiangalia kitu kama bixa, hapa ndipo mahali tunatoka bixa peke yake. Ile ingine inatoka Brazil. Na biksa yetu ni nzuri kuliko ya Brazil, maanake ya Brazil inakuzwa na madawa. Lakini yetu inakuzwa naturally. Na hawa wakulima wa kulima bixa wakipeleka soko yao, bixa inanunuliwa kilo moja shilingi kumi na saba. Na hali hawa watu wananunua wakiuza hiyo biksa wanauza Ksh.10,000 per kg. in powder form. Na hiyo ni kitu nimechunguza nikajua na hata mahali wanauza. Sisi wakulima hatuweki katika Coast province hatujawekwa maanani kabisa. (interjection inaudible) Tupatiwe hata kama ni ile tunaeza kuuza huko ng’ambo, tupatiwe hizo soko tupatiwe wale watu wanaweza kuja kununua. Last time kulikuja watu ambao wanataka kununua hizo … hiyo rangi walikuwa mrikebu imekuja hapa, walinunua kila kilo at 120. Ikawa ukiuza kwa hiyo mbei unaambiwa utashikwa na area chief na wale watu wengine. Sasa hiyo nikuregeza maendeleo nyuma ama nikupeleka maendeleo mbele?

**Com. Baraza**: iko middle men?

**Nzeki**: There were some middle men.

**Com. Baraza**: And you don't directly go to the bixa factory?

**Nzeki:** tunaweza kwenda kwa bixa factory directly lakini pia wananunua pia na mbei yao hiyo ya shillingi kumi na saba au kumi na nane na kuna wale wanakuja kutoka nje wananunua kilo moja themanini ama shilling mia. Sasa hawataki twende tuwauzie hao directly.

**Com. Swazuri:** Wanawauzia musiwauzie wale wanaotoka ngambo?

**Nzeki:** Wale the leaders. Kama chiefs wanatuambia watu wasiuze direct kwa zile kampuni zinakuja, hata wanakutwa wanafukuzwa wanaambiwa msiende kununua kwa wakulima.

**Com. Njoroge:** Kama watu gani?

**Nzeki:** Unajua sasa sitaki kuanzakuonea habari ya watu hapa itakuwa ni ….

**Com. Njoroge**: Kwa sababu kama ni haki ya mtu. Ikiwa ni haki yako kuuza kwa shilingi mia moja kwa nini unauza kwa shilling kumi na saba?

**Nzeki:** Sasa wale wakija wanaambiwa musirudi kuonekana hapo wakionekana hata magarini wanaweza hata kuchomwa. Sasa si lazima waogope?

**Com. Baraza:** To liberalize the market …. If you want to take to the factory you can, if you want to take to somebody else

**Nzeki**: If you want to sell outside country then you can also sell outside the country. Sasa hiyo ni oni moja. Tuna madini ambayo iko katika Kwale district. Kuna huu mchanga ambao unapitishwa hapa kila siku wa Kenya Glass unapelekwa kwa akina J.S.S ina nani wanapeleka … wanapeleka mpaka Nairobi. Hilo lorry moja kupelekwa mpaka Nairobi…. It's a lot of money. Wale watu wananuna ile mchanga pale lorry moja ni kama shillingi mia moja ama mia mbili na huo mchanga dhamani

yake ni kubwa. Sisi imekuwa sasa ni kama tunalaliwa tu hakuna kitu tunaona. Sasa hiyo lazima pia sisi tuwe na wale leaders wetu lazima wawe pia wafunguke macho na waangalie mbele. Kuna huyu mradi mwingine ulikuwa wa Titanium mining in Kwale district. Hii titanium munaambiwa ya kuwa yule yuko na shamba hapa lakini sasa unaambiwa yako ni feet tatu. na tukijua kabisa hii sheria iliwekwa na mkoloni maanake mwafrika alikuwa hajui ni kitu gani iko chini. Alikuwa akijua akipanda mgomba wake hapa hiyo ndiyo Mwisho shamba lake lakini kilicho chini yake alikuwa hajui. Sasa ndiyo waliweka hiyo seheria ya kuwa mwafrika …….. tape stops here side A tape 3

Zinaweza kutu-govern mpaka chini mpaka foot zile ambazo zinawezekana. Wacha ni malize hii, ile kitu ningeguzia kidogo ni kama mambao ya bara bara, hospitali watu wote wapatiwe free medication, shule iwe free mambo mengine kama mishahara unakuta mtu mmoja anapata 120 million mshahara na maid anapatiwa 12 ama kama mia mbili hiyo unakuta maid pengine mtu anapatiwa shillingi mia mbili. Ukijaribu kufanya hiyo fraction hata hiyo hesabu haingiani. Kunatakiwa kuwe na kiwango ikiwa yule aliye juu atapata mshahara wa 1.5 million at least ikiwa masharaha ya basi wachini kabisa iwe ni Ksh.10,000. huyu ni yule mtu wa shamba ama pengine maid. Sasa iwe classified namna hiyo.

Kitu ingine mtu kama amestaafu asirudi tena rurundishwa kazini maanake kuna watu wengine wanataka kazi unakuta mtu amestaafishwa halafu anapatiwa tena Board of Governor ama Director wa kit ingine Fulani Asanteni sana (clapping)

Na majimbo hivyo mambo ikiwa tutakuwa katika jimbo lao hapa kwale tutakuwa na hiyo mambo yote ikifanyika maanake utakuwa na hiyo mambo yote ikifanyika maanake utakuwa uchumi wote wetu na tunaweza ku-control sisi wenyewe. Asante sana **(laughter & clapping)**

**Mohammed**: Salaam aleikum. Ndugu maCommissiners, jina langu naitwa Mohammed Yusuf Masengeza mkaaji wa hapa kilonde. Mimi nataka Serikali ya majimbo kwa maana hii mbili ama tatu. Ya kwanza wenzetu wanjue washapata majimbo yao sababu nikisema hivyo majimbo saba sasa tayari wameshapata kwa sababu wamemiliki vitu vyao vyote lakini wapwani hawajapata majimbo na isipokuwa wao ndio wanatumiwa vitu vyao wakilisha watu wa juu. Hiyo ndiyo imewafanya watu wa Pwani wakati huu wote wanataka majimbo kwa sababu ya kuwa wameiacha muda mrefu. Na kwanza tuna bahari ambayo

niyadhamani kubwa sana kwa watu wa Pwani. Lakini bahari hii haitusaidii sisi inasaidia watu wa juu.

Nikisema hivyo mfano watallii wanazulu bahari hizo kama kwa mfano Kisiti Island wanapelekwa kule lakini pesa zote zile zinakwenda juu. Watu wa Shimoni hakuna hata ndururu moja wanpata kwa hivyo inamaanisha kwamba kama wangekuwa majimbo lao ama kama ingekuwa mikononi mwao zile pesa zingewafaindisha wenyewe. Kwa hivyo ndiyo maana sisi twataka haya majimbo ili vitu vyote vya hapa Pwani tuwe tutavitumia sisi wenyewe.

Pili, kama National reserve hapa Shimba Hills. Hii nafikiri ni kama ile Maasai land ama Maasai National Reserve Wamaasai wakati huu wanachukuwa 20% ya pesa ambazo zinachukuliwa pale pesa zile zinatumika pale pale kwa wale wenyewe lakini hii ya hapa national reserve hii hakuna ndururu moja ambayo inatumika hapa Pwani isipokuwa zote hizo zinakwenda juu.

**Com. Swazuri**: Munataka ngapi?

**Mohammed:** Tunataka 25% zibaki hapa **(noise from the crowd)** Haya haidhuru. Kwa mfano ikiwa tuna jimbo tutakuwa sisi wenyewe tunajiwanya mali zetu. Kwa hivyo sasa ni hizo pesa tuzopate tujue tutafanya nini. Tugawanye sisi hapa Pwani. Nyingine kuna mali za asili kwa mfano kama hiyo Titanium hiyo tumezungumza ya Titanium hii, shamba kubwa lili limekuja likavamiwa na wenzetu wa mbala baada ya kujua kwamba kuna madini waliitana wavamie ile shamba. Ambako kuna karibu acre elfu mbili ambazo haina kila mtu lakini wale wamekuja pale kuvomia ili wakati ikipimwa wachukue wao. Kwa hivyo tunasema hiyo mali yote ni ya watu tote wa Pwani. (**clapping**). Wakati itagawanywa yawe watu wa Pwani.

Na tunasema mali hiyo hiyo sio kwamba ifanyiwe hesabu juu Nairobi, lakini wale wanaotaka kuchimba madini waje hapa wasikizane na wenyewe waafikiane ndio waweze kufanya kazi hiyo **(clapping).** Na kuna vingi ambazo zimeweza kujulikana kwamba kuna mali kama hizo,kwa mfano fafuta kumejulikana kama kuna mafuta huko ikapatikana kama kwa mfano sehemu za Kinondo. Lakini serikali tayari imetoa macho kwamba watakuja wachimbe mafuta yale na yawe. Kwa hivyo tunasema sisi tunataka majimbo mafuta yale tutumie sisi wenyewe ili tunufaike pia. (clapping)

**Com. Baraza:** Hiyo mambo ya titanium, hiyo ni mambo makumbwa na sidhani watu wa Coast wanajua mali ambayo iko hapo ndani. Na hiyo tumeambiwa, tumesikia tu mesoma tu hiyo ikichimbwa vizuri hii Kenya haitaona umaskini tena?

**Mohammed**: Haya Asante. Tunasema hivi ……

**Com. Baraza:** Hiyo mambo ni muhimu sana.

**Mohammed:** Tunakubali Madam. Lakini tunasema hivi kwa nini Wakenya wote wafaindika na mali ya hapa Pwani. Tunataka watu wa hapa wafaidike na mali ha hapa Pwani, (**clapping, cheers**) kwa hivyo ikiwa ni chache, ni nyingi watu wa Pwani peke yake wafaidike na hiyo mali si mtu mwingine pia (**clapping**). Nyingine kuna watalii wanakuja kuchukua zile assets za samani zile za wazee wetu ambazo zilikuwa zimewekwa kwa museum. Wakichukuwa hizo mali wakienda wakiuza kwao. Kwa hivyo tunasema kama vile vita zamani vihifadhiwe kama vilivyo pia. Asanteni. (**clapping**)

**Com. Swazuri:** Mabaru Juma, Idi Mwarobia, Omari Mwamarifa awe tayari.

**Mubaruk:** Arabic greeting. Mimi nitaanza momo kwa moja kuingia katika upande wa mapendekezo. Na kwanza nitaanza na utangulizi. Jina ninaitwa Idi Mubaruk Mwarobia lakini si Mubaruk yule aliyefukuzwa na Kubo. Nina ishi hapa Diani na ninatoka kikundi kinaitwa Similani Development Organization. Ninasema nitaanza na utangulizi maanake Katiba yetu ya sasa inakosa kipengere hiki cha utangulizi, ambayo hii ni muhimu sana katika Katiba, lazima iwekwe ndiyo mtu ambaye ako na haraka akisoma utangulizi atakuwa ametosehka kuna nini ndani ya Katiba hii. Kwa hivyo Katiba yetu iwe na utangulizi ambao utafafanua mabo yafutao:

- Kwanza Katiba ni ya wananchi wa Kenya walio katika taifa huru lililojumuisha makabila arobaine na mbili yalio na haki sawa.
- Pili, mamlaka ya juu ni ya wananchi na iwe itaelezea ya kwamba serikali ni ya kidemokrasia iliyo na mfumo wa majimbo.
- Tatu, Kenya iko na mfumo wa vyama vingi vya kisiasa na kati yao ni vyama vitatu pekee via kisiasa viwe vitasajiliwa kwa kugombea viti vya Bunge na Uraisi katika uchaguzi mkuu. Vyama vingine vinaweza kujiunga katika kugombea katika uchaguzi wa serikali za wilaya.

**Com. Swazuri:** … usiseme neno baada ya neno ukisema hii utangulizi tanjua….(inaudible).

**Mubaruk:** Sawa sawa. Pendekezo la pili ni aina ya serikali. Serikali iwwe ya majimbo yenye kuongozwa na Bunge. Majimbo yawe manane na yawe ya kiuchumi yaani kila jimbo liwe na mamlaka ya kupanga maendeleo na jinsi ya kutumia

rasilimali zao wao wenyewe. Twapendekeza nchi iwe ya vyama vitatu vikuu vya kisiasa na uhuru wa kueneza sera zao bila kuingiliwa kati na vyombo via dola ila tu vinapofunja sheria. Kuwe na uhuru wa utamaduni la kila kabira uhuru wa kuabudu na ndini zote ziwe na haki sawa.

Nyingine ni kuhuzu Mahakama. Muundo wa mahakama uweze kurekebishwa. Kwa mfano judge mkuu asiwe wakili na serikali. Wakili na majudge wakuu wasiwe makili wa serikali. Serikali iwe na wakiri wake maalum na wajudge wakuu wateuliwe na tume ya wana seheria itakayo undwa na bunge. Kesi zisichukue muda mrefu kuhukumiwa muda usiozidi miezi mitatu.

Mtu asiwekwe rumande kwa zaidi ya masaa arobaine na nane bila kufikishwa mahakamani. Ikiwa mtu atashikwa na asipatikane na makosa basi aliyesababisha kushikwa kwa mtu huyo au watu hao alipe gharama (clapping) Mahakama ya dini kama ya Kdhi mkuu iwe na koti ya juu na ya kukata rufani. Kadhi mkuu ni lazima achaguliwe na Waislam wenyewe kwa jia watakayo penda wenyewe. Serikali iweke mawakili katika mahakama zote ili wale ambao hawana uwezo wa kutetewa na mawakiri waki binafsi wawezi kutetewa pia na mawakili hao.

Serikali za wilaya Similani ya pendekeza kwamba serikali za wilaya zipatiwe mamlaka ya Kikatiba ya kumiliki uchumi na kuweka lami bara bara katika wilaya zao. Serikali za wiraya pia ziwe na uwezo wa kusimamia milandi ya maendeleo na kuwa na mapato na fedha zinazopatikana ziwe zikihifadhiwa katika wilaya kwa kupewa uhuru wa kuweza kukadiria mapato na matumizi ya sehemu zao, wakizingatia uchumi wa jamii zao, dini zao na tamaduni zao.

Asilimia kama ishirini na tano ya mapato yawe ya sehemu ya kupelekwa serkali kuu, na iwe na matumizi ya kitaifa na ya kimataifa. Hazina ya wilaya iwe chini ya mamlaka ya kabira lenye umarufu wa wenyeji wa wilaya hiyo, kwa mfano Kwale ni Wandigo na Waduruma. Mamlaka ya kiongozi wa (interjection inaudible) Jukumu la Katiba. Tunaona Katiba yetu tunapenda kuwe na kipengere katika chenye kutoa uwezo kwamba iwapo jimbo fulani limenuiya kujitenga kulingana na uwezo wake wa ustawi wa kiuchumi basi liruhusiwe kufanya hivyo.

Halafu chingine ni mahitaji ya kimsingi. Kuna mahitaji ya kimsingi ambayo binadamu analazimika kupata, kwa mfano maji, afya,

elimu eh…(interjection inaudible) tunataka kufanya hivi kwamba similani inapendekeza kwamba tume itilie umuhimu katika kuingiza mambo haya kwenye Katiba na ifafanue wazi wazi kwamba mambo haya yatatekelezwa na kupewa haki sawa na serikli za majimbo.

Kuishi kijamii. Katiba iruhusu watu kuishi kijamii machanganyiko wa makabira na wawe na uhuru wa kufurahia tamaduni zao. Katiba pia ifafanue ya kwamba katika kuishi kwa muchanganyiko kuwe na ….(interjection)

**Com. Swazuri:** Ndakika zako zimeishi …

**Mubaruk**: Ngoja nimalize. Jamii zingine zinazotoka nje ya wilaya ziwe zinaweza kuishi katika wilaya zingine baada ya kukubali na kufuata masharti ya kiuchumi, dini na mila za jamii wa sehemu hiyo. Mamlaka ya kukubali au kukataa yawe ni uamuzi kutoka kwa mwenyeji wa kijiji kile anachoishi.

**Com. Swazuri:** Asante Sana.

**Mubaruk**: Ngoja ni malize hii moja ya kupungaza umasikini. Asante sana.

**Hamisi**: Salaam aleikum: Mimi na shukuru tume hii ambayo imtufika kwa siku ya leo.

**Com. Swazuri**: Jina Lako?

**Hamisi:** Jina langu unalifahamu vizuri kama Amil Hamisi Banda mwenye kiti wa baraza la Maimam Pwani kusini. Memorandum yangu nisha iandika lakini naongezea. Kwanza, memorandum yangu imezungumzia juu ya elimu, habari ya uajiri, habari ya Rais, na habari ya Majudge, viapo vile vinavyofanywa kuhusiana na kupiga sijida katiba Mahakamani; Judge kuitwa Lord, hiyo yote imezunguzia. Sasa ninacho ongeza katika upande wa Uislam nimezungumzia pia kuhusiana na Chief Kadhi lakini na ongezea kwamba tantaka siku kuu za Idd-ul- Fitir na Idd-ul-Haj zifanywe za kitaifa (**clapping).** Siku ya ijumaa ifanyweya kitaifa kama vile ilivyo juma pili. Tatu sehemu zote zinazoishi Waislam kwa wingi wahukumiwe na kitabu chao ( **clapping**). Nne, Katiba tunayoitaka kuwe na kufungo, ambacho, kinashinda heshima yamavasi hususan kwa wanawake **(clapping**) katika Katiba ambayo tunatalajia kuipata kwanza twataka Katiba ya majimbo na majimbo tunayoyataka ni kuanzia

kutoka kijiji kiwe na uwezo, location au kata, Division mpaka District ama wilaya. Isiwe ni majimbo ya Coast province tu peke yake.

**Com. Baraza:** Hapo kijiji iwe ni kazi gani ambayo inafanyika hapo … governance…?

**Hamisi:** Yes, mzee kama wa kijiji awe na mamlaka ya kutosha ambayo anaweza kuidhinisha na akatakaza. Kama zamani tukikumbuka wakati wa ukoloni wale walikuwa wakiitwa Headmen walikuwa na uwezo. Katika katiba tunayoitarajia ni kwamba rasilimali zote ziwe zinakuwa katika hazina kama vile nilitangulia … wilaya na district zote. Ile sheria ya kumfanya mwananchi amiliki ardhi juu tu, lakini si chini, iondolewe ikiwa madini kama atapatikana kama ule Titanium yatapatikana hiyo iwe ni ya mwananchi. Ni mwananchi mwenye hiyo shamba ndiye atakaye kaa na ku-negotiate pamoja na serikali na yule developer. Ndiyo katiba tunayotaka. Kuanzia Province, DC, DO, hawa tunataka waondoke. PC aondoke, DC aondoke DO aondoke, Chief aondoke, halafu wakati shaa kubalika hivyo kuwe na kipengere ambacho kitaluhusu wananchi wa zile sehemu walizo wachague ambao wataweza kuwaongoza (**clapping**).

Nikimalizia naona unanipatia warning. Kuwe na sweeping court ya Ki-islam. Koti kuu, Chief Kadhi asiwe na uwezo wa kusemea waislam yeye ni judge. Chief Kadhi awe na malipo kama alivyo Justice yoyote katika Kenya. Hao unakuta Judge wa hizi secular courts anapata laki moja na elfu ishirini na tano, Judge anapata elfu Ishirini na moja huyu Chief Kadhi wetu, kwa nini? Twataka kuwe na equality ya kila kitu. Na sababu muda ni mwingi na mengi yako humo ndani, pia bado baraza la Maimam litawatumia memorandum nyingine kwa sababu mambo ni mengi. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Ali … inaudible)

**Ali**: kwa jina naitwa Ali Said Mwagoyo mzaliwa wa hapa Ukunda. Kitu cha kwanza ni majimbo. Tunataka majimbo hasaa hapa Coast kwa sababu mimi nimezaliwa 1947 na mpaka sasa sijajua maana ya uhuru, sijajua kabisa kwa hivyo kitu mimi nataka ni majimbo tujimiliki sisi wenyewe watu wa Pwani, hapa Coast.

Swala la pili, ni habari bahari huku. Vijana wananyanyaswa sana huko na ma polisi wa hapa Diani. Wanakamatwa ovyo anakamatwa na watu wa bara lakini wakifika hapo wanaowekwa ndani ni Wadigo Peke yake. Swala hili tunataka liondolewe

hili. Tatu, ni mambo ya ardhi. Mimi mwenyewe nimeanza kufieka ardhi kutoka mwaka wa sabini nafikiri mpaka sasa nina mimea ninakula matunda ambayo ukizaa maembe siyawezi, lakini sijamiliki hiyo ardhi hiyo hiyo shamba hiyo sijapata harti yake. Na ukisema kwa wakumbwa unaambiwa hayo ni mashamba ya watu hatujui hilo wanatoka wapi. Hilo swala la ardhi hapa nataka litatuliwe. Hasa kama sikombii.

**Com. Swazuri:** Sikmbii ni wapi?

**Ali:** Huko chini

**Com. Swazuri:** Diani …

**Ali**: Kwa hivyo mengi sina mimi yasha malizwa na wenzagu. Swala mbalo natagusia ni la kidini. Hili swala la dini, dini la Ki-islam twataka pia ipewe uwezo wake wajiamulie mambo yao wenyewe. Hata heshima ya mavasi, mavasi wenzetu wanaotoka huko juu washaa ambukiza wanawake wetu hapa kabisa. Kwa hivyo hatulitaki hilo tunataka wawe heshima, wavae nguo za heshima. Swala hilo mlichukulie maanani. Sina mengi mimi nishaa maliza.

**Com. Swazuri**: Pakia (inaudible)

**Pakia**: Salaam aleikum. Jina langu naitwa Mohammed Pakia na ningependa kuchangisha katika marekebisho ya katiba kama ifuatavyo. Kwanza, nafikiri katika serikali kuna kifungu kinachohusisha mashule na usomaji kwamba, shule nyingi zinachukuwa asilimia themanini ya wanafunzi wake katika sehemu ile. Halafu asilimia ishirini inatoka nje. Na ni jambo la kushangaza kwamba kama serikali imetilia maanani swala la masomo kwa upande huu lakini likaachia wazi katika swala la uwajiri, kwamba katika uajiri sheria hii haifuatiiri. Ni lazima sheria hii katika masomo iendelee mpaka ifike katika uwajili kwa hivyo ikiwa shule zetu sisi sio nzuri na kwa hivyo elimu yetu sio nzuri ni lazima bado vile viwanda na sehemu za kazi zinazo patikana sehemu yetu, asilimia themanini ya wale wanofanya kazi pale, wawe watu kutoka sehemu ile. Kwa sababu ukosefu wa elimu unatokana na sheria ile iliyopangwa na serikali yenyewe.

Chango la pili ni kwamba katika masomo, sisi imekuwa bahati mbaya kwamba tumeshikwa muguu mbaya serikali iliendeleza

shule za sehemu zingine na miaka inayoendelea shule zetu zimekuwa hazina usaidizi wowote ila kwa kutegemea BOG na PTA iwe ndizo inawaendeleza. Mambo haya tunatarajia kwamba bado zile zile shughuli za biashara zinazoendelea katika sehemu hii, zisaidie maendeleo ya elimu katika sehemu ile. Nina maanisha kwamba kuwe na kifungu ambacho kitaturuhusu kila aliye na biashara katika sehemu ile hasa biashara kubwa kubwa, kwa mfano zile hoteli utaona kwamba kuna pesa nyingi zinazopatikana pale lakini pesa zile hazitunufaihi sisi. Kwa hivyo tuweke kiwango cha asilimia thelathini ya zile revenue inazokusanywa. Sio kwamba iende tu kwa serikali mbali kuwe na committee ambayo itachukuwa pesa zile ziangalie maswala ya watu wanaoishi sehemu ile kuanzia elimu, 30%, maji masafi, umeme, barabara, afya vitu vyote hivi viangaliwe kutokamana na mapato yanayopatika katika sehemu ile.

Na pia tuwe na misitu inayaosajiliwa. Msitu hii husajiliwa halafu baada ya muda ikatokea wakubwa fulani ambao kwamba wao wanakuja kuvunja sajali ile. Kwa hivyo tungependa baada ya misitu kusajiliwa, ile iliyosajiliwa isiweze kuvunjwa tena katika hali ya kuhifadhi mazingira. Kwa hivyo misitu yote iliyosjiliwa ibakie hivyo hivyo na yawe manufaa ya uzingira yanawasaidia watu wenyewe.

Na jambo lingine pengine mwisho nitachangia kwamba serikali yetu, ama kifungu cha utawala kiwe cha majimbo ili uamuzi mwingi unaofanyika katika District level umetokana na District heads ambao kwamba sio watu wakaazi wa pale. Kwa hivyo tunaomba wale viongozi walioko katika district level wote wawe ni watu wa kutoka pale Kwa hivyo kwa ufupi tunasema tunahitaji kujitawala wenyewe na utawala ule umpe yule mzee wa ngazi za mashinani, nafasi ya kupinga jambo yaani uamushi uwanzinze mashinani kutoka village Chairman, mpaka kwa level za juu badala ya kuanzia juu ukija chini, uamuzi wa mambo yanaendelea katika sehemu yanzie chini. Asante.

**Com. Swazuri:** Juma Ali, Peter Macharia

**Macharia**: Asante sana. Mimi nitatumia dakika hizo kuzungumza haraka, na nita anza na Rais, President. Mimi nina maoni ya kwamba president ambaye tutakuwa naye kutoka hapa asiwe president ambaye ni ceremonial awe na mamlaka. Lakini mamlaka yale yasiwe kama ya wale wawili waliokuwa hapo mbeleni, yapunguzwe asiwe above the law. Akikosea ashtakiwe kama mtu mwingine.

Pili, akitengeneza commission ambaye inahusu wananchi, naifanye kazi, impe mapendekezo, atoe yale mapendekezo kwa

wananchi, asiyaweke. Tatu, sioni maana yake yeye kuwa Vice Chancellor wa chuo kikuu achie wale wataalamu wa huko. Asiwe na ruhusa ya kugawiya marafiki zake mali ya uma kama mashamba (**clapping**). Baada ya kuapishwa kama Rais wa nchi hapa aache kuwa Rais wa chama, awe Rais wa nchi sababu atakuwa Rais wa hata wale wasio wa chama chake. Baadaya kuapishwa kama Rais wa nchi asijigambe Rais wa chama chake, ni Rais wa watu wote wa Kenya hata wale wa vyama vingine. Vice President

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Macharia**: Awe Mbunge. Vice President napendekeza achaguliwe moja kwa moja na wananchi na ikiwezekana, wakati wa matokeo ya uchaguzi atakaye kuwa number mbili apatiwe kiti cha Vice President. Pili, huyu Vice President awe na uwezo kwa mfano Raisi akiwa nje ya nchi hii, ama akiwa mgonjwa atekeleze wajibu wa Rais kikamilifu na wote wawili wakiwa hawako kwa mfano mmoja yuko nje, Vice President ni mgonjwa speaker wa Bunge achukuwe mamlaka.

Member of Parliament. Akiwa amechaguliwa na haonekani na watu wake katika constituency yake, bungeni haendi, hata hasikiki na watu wake akisema lolote, labda anashughulikia biashara zake wananchi wale wawe na ruhusa ya kumuonda sababu hafai. Hata Councillor iwe namna hiyo hiyo. Huyu MP iwe ni lazima awe na ifisi katika Constituency yake afisi ya serikali (clapping) juzi tulisikia watakuwa na ma afisi Nairobi, lakini hatutaweza kuenda Nairobi wote, awe na afisi na ikiwezekana iwe katika makao makuu ya tarafa. Pale atapanga ni siku gani atonekana na watu wake. Three, huyu Mbunge akijiunga na chama kingine mbali na kile alichaguliwa na wananchi wake hii nikumanisha ya kwamba amewandanganya na amewasaliti ana amewauza (**clapping**) wawe na ruhusa ya kumfukuza.

**Com. Swazuri**: (inaudible)

**Macharia**: Kuwe na njia ya kumuondoa. Wananchi waliomchagua ndio amewaudhi wawe na uwezo wa kumondoa (clapping). Mbunge huyu katika mirandi ya Constituency yake, kama ni pesa za harambee ama grants zile anahusika nazo awe transparent na accountable na answerable kwa wale watu waliomchagua. Vyama vyia siasa. Napendekeza vyama via siasa katika nchi yetu ya Kenya visiwe saidi ya vitatu.

Elimu: elimu ya msingi iwe kutoka darasa la kwnza hadi ya saba iwe ya bure. Elimu irudi ile ya zamani ya miaka saba primary, miaka nne secondary, miaka miwili 'A' level na mitatu university na kuwe na commission permanent ya wataalam kushughulikia ubora wa elimu Kenya, na sio wanasiasa mtu akiingia analeta mabadiliko ya elimu. Serikali inunue vifaa vya elimu katika mashule yote. Kwa hivyo upande wa dini ningesema shida ya dini vile tunagongana mambo ya dini, shida hii inatokea kwa sababu ya Registrar anasajili kulingana na maombi ya watu wakitaka dini zao ziandikishwe. Napendekeza huyu Registrar atafutiwe wataalam watu wakutoka ndini zote tatu kubwa Kenya, dini ya Ki-islam, Protestants na Catholics. Wataalam hawa watachunguza maombi ya kusajili dini wa na kupendekeza kwa Registrar, ili asikosee kusajiliwa dini ya kuabudu shetani. Thank you.

**Com. Swazuri:** inaudible.

**Wachaunga:** Mimi naitwa Mwachaunga Wachaunga Mohammed. Mimi nilizaliwa 1940 nastaajabu mpaka saa hii sisi Wadigo wakati huo tulikuwa nikienda 1947 nilikuwa nikienda baharini siulizwi. Lakini saa hii naulizwa hata sielewi nitafanya nini na mimi ndio mwenyewe wa Pwani. Maanake mimi ni mtu wa Tigore ambaye mpaka sasa yuko picha yangu Zanzibar. Nikizungumza hivi na zungumza kikweli na ki-sure na jua mikataba ya Pwani iliofanywa, minne na naijua. Tunataka majimbo ama kama hakuna majimbo tunaenda kwa malikia sasa (**clapping**). Kwa sababu tumeteswa miaka sitini na Mwarabu, tumeteswa miaka sabini na mwingereza, tumeteswa miaka thelathini na serikali yetu ya Kiafrika kwa hivyo naomba sisi wansnchi wa Diani na wa Kwale jumla haswa wa Pwani mimi nimepewa memorandum hasa ya wazee wa Pwani. Wazee wa Pwani weameniambia wanataka majimbo na majimbo yao hawatamfukuza mtu yoyote.

Juzi nilikuwa Marafa kwa shirikizo Party of Kenya, na nilizungumza na wazee wa Marafa na tukaelewana hiyo kitu. Kwa hivyo nakuomba mama sisi hatuna mambo tunataka majimbo na majimbo ya anzie chini, mumesikia? Chini kwa wazee. Maanake wazee ndio wanajua historia ya Pwani. Hakuna mtu mwingine kwa hivyo nasema tafadhari; mambo yangu ni matano. Halafu upande wa kazi, mimi najua niliandikwa kazi na county council 1968 nilikuwa '66 nafundisha lakini nikiponda '68 nikaandikwa na city council lakini wakati huo ulikuwa wakati wa uhuru tulikua kazi tunapata tu, lakini surprisingly saa hii mamo yote huko sisi tuaandikwa kazi wapi. Secondly, nakwambia port inatoa 20 million a day niambie sisi wakati wa Sultan tulikuwa tukipata percentage ya watu wa Pwani na saa hii watu wa Pwani wanapata nini? (**clapping**). Halafu na kwambia kitu kimoja bwana

Commissioner kuna vifungu vipewa power commission…..

**Com. Baraza**: Unataka mapendekezo gani hii ya KPA

**Wachaunga:** KPA tunataka 80% ibaki hapa (**clapping**) tutakupa 20 sababu mwenzetu mumekula siku nyingi (**laughter**) halafu secondly na kwambia ni mambo mengine ya kustajabisha. Kifungu cha sheria mia mbili na themanini cha commission wa land kiondolewe. Hiki kifungu kimemupa commission power anaweza kutoa title deed.

**End of tape 3.**

Hata ikiwa Nairobi. Hiki kifungu ni lazima kiondolewe. Na kifungu hicho pia kina saidia kifungu mia mbili themanini na moja. (**Com. Baraza:** Munataka nani atoe?) Sisi wananchi tunataka hiyo section iyondolewe mnasikia?

**Com. Swazuri & Baraza:** Nani afanye hio kazi?

**Wachaunga:** Sisi wananchi tutafanya kazi hiyo maanake ndio we have local people, (**clapping**). La mwisho la sema hivi, serikali ya wazee ni ile ya zamani ya ngambi sasa kwa saa hii wazee wakifanya mkutanao wa "ngabi" wanaambiwa wanafanya kayambongo. Kwa hivyo tunataka serikali ile irudi kama vile zamani. (clapping) Ngoja kidogo tu kuhuzu elimu. Elimu Kenya ni ya huko bara hata mtu akipata upper one honours hapati kibarua, 100% na kwambia hata akipata upper one honours, upper two honours hapati kibarua mtu wa Pwani ambaye ni Mdigo, Mgiriama, Mchonyi, Mrabai kwa hivyo I am surprised kwa nini iwe hivyo….

**Com. Baraza:** Huyu na ako na job kubwa (inaudible)

**Wachaunga:** Sikiza mimi niko na ndugu yangu alifanya mtihani wa DO he is having upper one honours and he was failed alienda kwa teachers sasa ako private sector munaniambia nini Madam (**laughter**). Halafu watoto walisomea education na mpaka saa hii hawajapata nafasi za kuende kusomesha. For example wa wapa (**noise**/ **laughter**).

**Hassan:** Nashukuru ndugu muliohudhuria hapa saalam aleikum. Mimi ni Hassan Mwandarashi Jasho ni mwenye kiti wa Guard Welfare ama kundi la maendeleo la Gombato sub-location linaitwa Guard. Mimi kwa kweli sina maneno mengi sana nina maneno machache. Nipatie ruhusa ni vae miwani kidogo. Sisi watu wa Guard Pia tuliona kuna makosa mengi katika

Katiba hii ya sasa na tukaona lazima tuajibike tuzungumze.

Kwanza kabisa sisi tunataka majimbo, mufumo wa majimbo. Tumeona tujiunge na wenzetu tutake majimbo. Tulichunga kwa kikamilifu idara zinazotutumikia, na tukaona pia kuna hitilafu nyingi sana. Tumezungumza katika memorandum yetu habari ya lands kwa kirefu ama kifupi, tumezungumza roads kwa kifupi, tumezungumza health, education, agriculture. Tumezungumza utalii na pia tutazungumza kuhusu utawala, provincial administration, Judge na

**Com. Baraza**: Tupatie highlights.

Kwa kifupi mfano hii swala la ardhi ni nyeti sana. Licha ya kuwa kuna hali hizi ardhi tu. Private land owned by community na imefanywa scheme hapa kwetu. Hiyo Diani complex the famous Diani complex, that was private land owned by the community. Lakini imefanywa scheme. There is a two fifty hundred acres on the front row no land was given to a local resident. Hakuna mtu wa Pwani aliyepatiwa acre hizo the front low zote zilichukuliwa kama scheme ili ambiwa na serikali zote hizo acre mia mbili hamsini the front row beach, hakuna local resident alipata ardhi hizo.

**Com. Swazuri:** Tunataka proposal.

Hassan: Proposal nikuwa sisi ni mufumo wa majimbo, ambayo ni kila jimbo liweze kuwa na uwezo wa kumiliki mambo haya ya ardhi kuwe kuna land board kabisa inashugulika na swala la ardhi Pwani, si mambo mengine. Si Commissioner wa lands chochote no! Habari ya ardhi tuliona pia ni vile tunazo peleka watu kwenye mahoteli kubwa kwa vile vile.

Imechukua miaka ishirini kwa hospitali ya Msambweni kupata barabara ya lami na hiyo barabara ya Kwale nafikiri imechukuwa miaka ishirini, hiyo nyingine imepelekwa Lunga Lunga ilikuwa pale mangwenyenye, Kenatco walikuwa wakipeleka mali huko Tanzania ikalazimisha Tanzani kufunga mipaka yake. Kitu nyingine hizo sehemu kabisa hakuna barabara nzuri. Kwa hivyo ni utawala wa mkoa ue na maamuzi ya kuhusu swala la ardhi kwa jumla. Nenda hospitali ya Msambweni hii watu wengine husafiri kama garden ya kifo. Ukienda kule ukiwa wewe mgonjwa mahututi wewe huna usalama kuja mzima, wewe utakufa tu. Hiyo ni wazi kabisa. Nenda pale utaoa mambo mwenyewe.

Kuhusu swala kabisa la elimu, hili ni shikitisho kubwa, kwa kweli tumeanza elimu lakini tumekuwa nyuma kama mwenzangu amevyozungumza. Kwa kweli swala hili dawa yake ni utawala wa mkoa tu. Kwa sababu tumeachwa, na tumeachwa kuna wengine wamesema chuo ama waalimu wamesema kuwa chuo kinajengwa cha utalii hapa. Lakini kama vile vile tunaona ile chuo cha waalim pale, wanatoka huko kwenda kufundishwa pale. Kwa hivyo kitajaa watu wa huko wafundishwe na waje wajae hapa. Sisi tutakosa tuna nafasi hizo. Kwa hivyo dawa kubwa kabisa ni utawala wa majimbo ambayo mamlaka hayo yawe chini ya majimbo.

Kuhusu swali nzima kabisa la ardhi – agriculture. Agriculture kila kitu chetu kinakosa thamani kabisa na hii ni tatizo kubwa kwa sababu nchi yetu yategemea agriculture. Ikiwa swali hili tumeachwa nyuma hivyo hatuna la kuwa. Ni kama ule mfano unasema make them poor and you will get what you want. Hapa mtaa wa Pwani maskini, hakuna kila tunachotoka. Wametufanya maskini, vitu vyote havinunuliwi kokote kule ili waweze kunyakua zile ardhi zetu. Na wanafaulu kwa sababu hatuna kingine isipokuwa vile vipande vya ardhi. Kwa hivyo hili ni sikitisho kubwa. Kiwanda kile ambacho, kilikuwa kinatutumikia hapa cha Ramisi kimekufa, kwa hivyo shamba hazina thamani. Kwa hivyo swali kubwa sana hapa ni majimbo tuwe tunaweza kushughulikia swala la agriculture sisi wenyewe hapa.

Tourism hii, ninawaambia kwamba kile hoteli kue ukipata watu wa hapa wawili ama hata watatu utaona ni ajabu. Wengi ni mtu mmoja, wawili tu ama watatu. Wale ambao huandikwa kazi licha wakubwa ni wale wadogo tu. Mimi niko karibu pale na zile hoteli, niko karibu na Indian niko karibu na Southern Palm kule. Mtu kama hapo ambako naishi mimi hawazidi watu watatu wanaondikwa na Southern Palm, na tuko pale, watu wote ni beach boys, hakuna kabisa. Kwa hivyo hii ni tatizo kubwa. Kwa hivyo tukiweza kusimamia jimbo letu, nafikiri maswala haya yatakuwa chini ya majimbo. kwa hivyo tutayangalia vizuri.

Utawala lazima tuwe tuna-adopt hii parliamentary system. Hii ndio tunaona ni sawa na wataalamu najua wataka parliamentary system. Sitaki kuongeza mbele. Hii ni kugawanya mamlaka kuwe na kiongozi wa nchi na kiongozi wa serikali. Hii kiongozi wa nchi awe Rais na kiongozi wa serikali awe waziri mkuu. Kiongozi wa nchi awe kazi yake ni kutengeneza serikali na kuivunja. Halafu waziri mkuu aendeshe serikali, basi atoshe hiyo. Tuwe tuna executive powers ya mahakama, kuwe kuna executive kwa swala la ardhi, education ana kuwe kuna uhuru wa uwajiri wa Serikali, Public Service Commission; tuna uhuru wa polisi, ndio

tuwe na tume yetu hapa, kila jimbo litakuwa na tume yake, maswali ya hapa ya kunyanyaswa watoto yataangaliwa na jimbo hapa. Kwa hivyo itakuwa hakuna matatizo zaidi. Kwa sababu mashtaka kama tunavyosikia kuhusu beach hapa kama tungekuwa na commission yenyewe ambayo inaangalia maswali ya polisi, maswali haya nafikiri iyangekuwa sawa sawa kabisa. Nakushukuru asante.

**Com. Swazuri**: (inaudible) Husseing Uza, Juma Barua, halafu ………….

**Barua:** Asalaam aleikum……………. Ndugu Commissioner na Waislam wote mlio hapa salaam aleikum. Mimi kwa majina naitwa Juma Hamisi Barua mzaliwa wa Diani location. Kwanza mimi nataka Serikali ya majimbo. Kila jimbo litakuwa na bunge lake, kuwe na upper house na lower house. Jimbo ambalo litakuwa na uwezo wa utekelezaji kuhusu maswala kama ile ya ardhi, elimu, uchumi, afya. Rais awe ni Mbunge atakaye chaguliwa na wananchi, kuwe na waziri mkuu. Hawa wote wagawanye mamlaka.

Swala la afya, hili ni swala letu sana ingewaje wengi wamelihepa. Mimi naomba ninacho omba kwa serikali yetu ya majimbo itakayo kuja, iondoe kitu kinachoitwa ‘cost sharing’. Afya iwe bure kwa wote, mwenye uwezo mpaka yule hana uwezo. Mwambao wa Pwani. Tunahitaji mwambao wa Pwani kulingana na mikataba ya hapo awali. Na mimi nasema hivi ikiwa wakenya wenzetu hawatakuwa tayari kutupa support ya majimbo basi mkoa huu ujitenge kama vile wenzetu wa Zanzibar. Kuna majimbo mawili tu. **(clapping)** Kuwe na jimbo la bara na jimbo la Pwani (**clapping**). Kwa mfumo huo tunataka Rais baada ya kuunda serikali amuachie waziri mkuu awe ndiye mkuu wa serikali na Rais awe ni mkuu wa nchi peke yake. Na napendekeza Rais atawale kwa mifumo miwili ya mika mitano mitano. Na ikiwa amefanya ufisadi, asiwe juu ya sheria anangaliwe na sheria vile vile, kupatikane kifungu ambacho Rais anaweza kushtakiwa. Kuwekwe kifungu katita Katiba inayokuja, Rais afanyiwe tume ya mashtaka apelekwe kotini kama amefanya ufisadi dhili ya nchi. Wabunge tunao wachagua wakishatawala kwa miaka mitano ikiwa hawakutufanyia yale tunayotaka basi turuhusiwe ama tuwekewe kifungu tutoe ile kura ya kutokuwa imani na wao. I mean Mbunge akishachaguliwa, si atafanya kazi kwa miaka mitano…..

**Com.Swazuri**: Mmutoe kabla au baadaye?

**Barua**: Kabla ikiwa hakutufanuyia yale hatukuhitaji ikiwa ametundanganya kwa sababu wakati wa campaign hawa watu hutundanganya sana. Tutawaletea maji …… tutawafanyia hivi na hivi halafu wakishapata ile license ya kwenda bungeni ndio hawaoni mpaka miaka mitano ijayo. Kwa hivyo kwa maoni yangu mimi nasema, ikiwa hawatatufanyia yale ambayo wametuahidi, tupewe kipengele ambacho tutakuwa hatuna imani na wao.

**Com. Swazuri:** Ifanywe baada ya miaka mingapi?

**Barua:** Ikiwa ametuahidi na ….. at least miaka miwili ikiwa hakuonyesha ile maendeleo yake tumpigie vote of no confidence. Kwa hayo mengi na machache salaam aleikum. **(clapping**).

**Com. Swazuri:** Abdala Mwachambuli (voice: memorandum yake niko nayo hapa) Ya Mwachambuli. Haya tafadhali itoe kwa niaba yake. Ajali Muvua? Munyikai Mwanyaka. Haka karibu mzee. Atafuatiwa na Mohammed Mwacharo.

**Suleiman:** (Greetings in vernacular) Salaam aleikum. Mimi naitwa Munyikai Suleiman Mwamnyaka. Mzaliwa wa hapa Gombato, Diani. Maoni yangu mimi hasa naitaka majimbo kwa hiali hata kwa nguvu (cheers & clapping), nataka majimbo kwa hiari hata kwa nguvu (more cheers) niko tayari. Sitaogopa, hata kususi hasa nasikitika sana kwa sababu ya ardhi tu, peke yake. Wacha haya tote yamezungumzwa na wenzangu. Hassan ni kweli amezungumza na Rama Mwasina pia amezungumza haya maneno yote, mimi siko na ubaya. Lakini uchungu nilionao ni ardhi, wakati huu mimi sasa ni mgonjwa nitafanya wapi ikiwa mnazi yangu mimi nimepokonywa na miembe nimepokonywa kwa sababu ya usaliti. Kwa hivyo huu mwambao wa Pwani ulikuwa haukutawaliwa.

Hata nakataa Mwambao wa Pwani ulikuwa unajitawala mwenyewe kutoka hapo mwanzoni. Mwingereza hakutawala hapa mwingereza alikuwa ni jirani wetu, rafiki yetu ambaye alitudufuzia yule mwarabu. Sisi tulikuwa tunatawaliwa na Mreno. Na Mreno akafukuzwa na Mwarabu. Mwarabu tukaomba msaada kwa Mwingereza ndiye alitufukuzia yule mtu. Tukamwambia sasa wewe utakuwa hapa mwenzetu, jirani yetu mzuri natumeendelea naye. Hapa kwetu tulikuwa sio Kenya. Hapa ni Mwambao wa Pwani. Coast Province (**clapping**) Hapa ni mwamba wa Pwani tulikuwa hatukutawaliwa na mwingereza Kenya ni huko juu sehemu za jioni (**cheers and Clapping**). Kwa hivyo mimi matakwa yangu hasa hususi ni majimbo.

Nijitawale mwenyewe na nimalize mimi mwenyewe, mawaziri wangu niwaweke mimi mwenyewe, mawaziri wangu niwaweke mimi mwenyewe, matakwa yangu yote niyaweke mimi mwenyewe. Sitaki mtu kuniingilia kutoka sehemu za jioni (**laughter & clapping**). Na majimbo haya si kusema nitamfukuza mgeni hata. Nitakuwa nayeye kwa sababu wale watu wengi ndio wenye biashara. Lakini naomba katika tume hii iliyoingia hapa, mimi naomba sana majimbo. Majimbo kabisa na pia hapa ninayo makaratasi ile ya mwanzo tulyoweka sahihi Ngala na pamoja na Mr. Kenyatta. Hii ndio ambayo wewe itakupiga ni kiboko yake (laughter) salaam aleikuim. (talks in vernacular) Naitwa Mwinyika Suleiman Mwamnyaka. Long pause followed by the next speaker.

**Omari:** Arabic greeting. Ndugu zangu mimi kuchangia kwangu katika Katiba hii, mimi nasema kidogo tu, ila nanacho kikaratasi changu ambacho kwamba nimekisalimisha kutoka hapo, nitawapa hawa wanangu wakiongalie. Lakini ni kidogo mimi haja yangu ni majimbo **(clapping**). Hii serikali ya majimbo ina maana. Sisi tumenyanyaswa mpaka hivi sasa maukio yangu mimi pia nimetukanwa na mwanamke wa Kikikuyu ananiambia mimi ni serikali yako wacha viaka (**laughter**). Hiyo ni Kiswahili gani. Namwambia jambo ananiambia jambo ya nini. Je wakati huo roho yangu nimsikia aje? Je sasa hiyo ni serikali ama ni maonevu?

Sasa kwa hivi sasa ikiwa iko Katiba ambayo imekuja hii nzuri ambayo wananchi wanaitaka, mimi haja yangu ni majimbo. Haja yangu ni majimbo niipate na serikali yake na kirauni chake. Sio kuwa ati ni pewe majimbo kuna nusu hukoinaambiwa ati iko jioni. Hiyo kupatikana mambo ya jioni ni mengine yamekwisha. Yamepitwa nawakati hivi sasa sio hivyo. Hivyokuchangia kwangu mimi uchungu pia ninao tunaambiwa nyinyi watu wa Pwani mkae hivyo hivyo. Mlivyo kaeni hivyo hivyo. Hicho Kiswahili hicho ikiwa mtu anafikira zake anaweza kujiuliza nikae hivyo hivyo kivipi? Jamani, sasa mimi ikiwa nitakwambia sikukuambia jina langu ninaitwa Mohammed Omari Mwacharo kuzaliwa kwangu mimi nataka wale wasomaji wangu watoto wangu waniandike uelezwe kuwa mimi ni mtoto ama mimi ni kijana. 1983….. ngoja 1989. Hebu fanyeni hesabu makaburu (laughter) okey ikiwa nakosea sorry.

**Crowd:** 18 sio 19 …

**Omari:** Je, mimi ni mtoto mimi nanafuatanyote huyu baba aliye miwani … huyo nunda huyo nunda huyo mimi namzaa. Kutoka

siku hiyo niambie wana mzee ni serikali yako fanya heshima. Nimekasilika mpaka muda huu.

**Com. Swazuri:** Pole baba.

**Omari**: Pole heshima yangu mimi nataka majimbo sitaki serikali ingine. Hiyo majimbo tu ndiyo nataka. Majimbo! Majimbo! Majimbo

**Crowd**: Majimbo! Majimbo!

**Omari:** Tupate MajimboPwani. (interjection: Com. Baraza, inaudible) Hapi Hapa! Mama wakike ananiambia mimi ni serikali yako wewe uanfikiri nini kitu hicho? Hiyo ni utoto kabisa mwanamke.

**Ali:** Salaam aleikum. Kwa jina naitwa Swaleh Ali. Nafikiri mambo mengi yamezungumzwa hasa ya majimbo na mimi pia sitapinga nasema naungana na wenzangu walio tanguliwa kuhusu serikali ya majimbo ambayo itazingatia; uraia kwanza uwe unapewa mzaliwa wa hapa Pwani katika serikali ya majimbo. Uraia utakuwa ni mzaliwa wa hapa. Ama mtu wa kutoka jimbo jingine ataingaia jimbo hili na kibali maalum. Isije ikawa mtu amefanya madhambi kwao sasa anakuja kutafuta mahali pa kujificha. Kwa hivyo raia la nje wa jimbo hili atakaa kwa kibari maalum.

Kuhusu ardhi, ardhi lazima mwenye jimbo hili ndiye atakuwa na kibali cha kumiliki ardhi. Kuhusu shughuli zote za viongozi lazima lizingatie, mzaliwa wa hapa ndiye apewe madaraka fulani kuanzia, Chifu, DO,DC mpaka PC kusiwe mtu wowote wa bara. Halafu pili wakuu pengine wa Polisi kuanzia OCS mpaka wote lazima wawe wa hapa kwa sababu haya yote maliyoyasikia maonevu yanafanyika kwa sababu vituo vyote hivi havina mzaliwa wa hapa. Kuanzia ofisi hizi zote ninazosema mpaka kituo cha polisi. Ndio maana kunatendeka maonevu haya na mengineyo.

Mambo mengine, kwa sababu membi yamezungumzwa vyama vya kisiasa viwe vitatu tu. Zisiwe zaidi ya vitatu na yeyote yule kiongozi yeyote yule, awe ni mbunge au awe ni wa upande wa pengine DC, au nani, awe anawezekano wa kupingwa na raia na akaachishwa kazi sio kupewa transfer … ah …ah. Awe raia wana haki ya kumkataa na aachishwe kazi kabisa. Asifanye kazi mpaka Rais vile vile. Tukimkataa raia awe ni aende nymbani asiwe tena na uongozi wowote.

Katika mahakama ya Chief Kadhi lazima ihusione na kesi zote. Sio yaachiwe ndoa na talaka na urithi peke yake, bali iwe inahudumia kesi zote lakini ihukumu kiislam. Yule mstakiwa yule mwenye kustaki, mfano kama ni mimi mlalamishi nikimpeleka mtu kotini niwe nina uwezo wakuchagua huyu apelekwe koti ya upande wa kiislam. Ahukumiwe na upande huo kwa hiyo haki iwe kwangau mimi na nikimtoa mtu yule awe atashughulikiwa na ule upande ambao ninautaka mimi mwenyewe. Kwa hivyo ofisi ya Kadhi iwe inahusiana na kesi zote.

Pili, appeal isiwe inje ya na korti ya kiislamu. Appeal iwe ni katika hiyo hiyo ofisi ya upande wa kislamu. Ishalla kwa sababu mengi yamezungumzwa haya machache yametosha.

**Com. Swazuri**: not audible

**Kuliwa:** (Greetings in vernacular) Asanteni: Sasa nitazungumza Kiswahili. Majina yangu kamili naitwa Rashid Hamad Kuliwa kutoka Diani Mumombi kama Chairman wa village huko. Kitu cha kwanza tunalilia majimbo sote. Kuanzia sehemu zote za Pwani tunahitaji majimbo yapatikane, kwa sababu tumezidi sana kunyanyaswa na mpaka dakika hii hatuna uwezo wowote tunanyanganywa kila aina ya mambo ambayo angalao tungeyafanya na sisi tunashindwa. Nikisema ule ukweli kama ambaye nimekaa hapa kwa jukuwa hili, tuna mashamba ambayo tumenyanganywa kwa muda mrefu sana. Mashamba hayo kutoka mwaka tarehe moja mwezi wa kwanza 1914. Hizo shamba zimechukuliwa kwa lease na shamba zile zimekaliwa lease kabla haijaisha. Ina haki gani shamba hiyo kuuzwa ikiwa lease haijaisha. Si unyonge huo? Huo ni unyonge mkubwa sana. Ikiwa sisi hatuna uwezo je tufanye nini serikali ya KANU ndiyo inatuumiza sisi? Kwa hivyo tunataka majimbo na shamba zile ambazo zimechukuliwa. Kila mmoja apate hilo shamba kulingana na uwezo unavyotakikana kisheria ya mwananchi wa Pwani wapate shamba zao. Sababu mpaka dakika hii nahakikisha kwamba tuko na shamba ambazo ziko wazi kutoka Nairobi ukiangali kwa map. Lakini ukija hapa shamba zoate zime katwakatwa kila mahali, hakuna nafasi kabisa ya kuingia shamba hizo kutoka ukunda mpaka Diani complex shamba hizo zimechukuliwa. Ukiuliza ni nani amchukuwa shamba hajalikani ni nani. Unaona mtu anatoka huko na title deed yake mkononi shamba yenyewe hajui iko wapi anauliza Chifu akaonyeshwe shamba. Hilo jambo tunaliomba tafadhali liondoke. Tena, sisi village Chairmen tupate uwezo wa kuangalia mambo ya mashamba. Sio watu wengine waangalie mambo ya mashamba. Chief hajui mambo ya mashamba ni mimi ndio najua haki ya shamba iko wapi na ni nani na nani wamepakana. Leo mtu anakuja huko anasema shamba yake ni hii wewe ulipakana na nani? Hajui.Je, ni haki hiyo? Ni

sababu ya kunyanyaswa. Na tunayanyaswa na serikali ya KANU. Kwa hilo jambo tafadhali ninaliomba majimbo yaingie hapa ili makusudi ya kwamba tupate uwezo na utawala wa kujitawala wenyewe. Hatukati kunyanyaswa tena. Mambo ya kunyanyaswa yameisha. Haya shukurani. **(clapping**)

**Com. Swazuri**: Lithi Moge, hayuko? Mwanamisi Mwanaisha.

**Mwanaisha**: Jina langu kamili ni Mwanamisi H. Mwanaisha Hassan. Ni mwenyeji wa Diani Location karani wa vikundi vya akina mama tarafa ya Msambweni. Na ujumbe wangu ni kuwa nimetumwa na wanawake hawa wa tarafa kuwa umuhimu twataka majimbo. (**clapping**). Tunataka majimbo. Tunataka majimbo kwa sababu mambo mengi ambayo yamezungumzwa na wenzetu yamelenga kuwa hatujajitawala. Na kujitawala ni kupata nafasi za kimaisha kuyamudu. Hasa kwa akina mama wamesisitiza kupewa jimbo lao kwa sababu sisi nido wazazi, na tulionelea kuwa watoto wetu hawana ajira yoyote.

Tukilengania kuwa mfuo wa Pwani uliagizwa sisitizo tuuwache wazi ujengwe na wageni kwa sababu utufae kizazi chetu. Lakini kufikia sasa hakijafaa. Kazi ni kunyanyaswa. Serikali bado imetukodolea macho kufungashwa watoto wetu wakiletwa nyumbani bila ya umuhimu wowote tukiambiwa kukatwe vibali na ili hali wezetu wageni wana masanabu huko bila vibali **(clapping**)

Na upande wa ……….wakiwa tu tunawaleta upande wa driving tutaona magari mengi dereva akiwa Mdigo anaambiwa simama hapo. Yaangaliwa tairi yaangaliwa huku, ili gari nyingine ya mtu wa bara ipite hapo iende mara tano Msambweni ndio Mdigo aambiwe chunga huyo tairi. Sasa utakuta madawa ya kulevya na changaa imekaa huko ndani ya Nissan na watu wa bara amekaa hapo waendelea huko mashambani vichochoroni wakauzie watoto wetu, lakini askari yule ametega kikofia amwambia chunga tairi na tena ile speed upunguze saa hii. Sasa huo mnyanyaso huu twaona umetoka juu kuja chini. Kwa hivyo tunataka jimbo letu. Na wakina mama twasisitiza jimbo letu kwa sababu mnyanyaso wa akina mama haujatiliwa maanani. Kina baba wa Pwani mtake majimbo na akina mama wa pwani muwape heshima zao.

Tena tunataka kazi kama akina mama kulingana na ile elimu yetu ilipofikia. Kama tuko maJujdge tupewe U-Judge tusiambiewe ule ni mwanamke (**clapping**) Na kama tuko tuwe ma pilot wasiambiwe huyu ni mwanamke ataenda atoke nini aambiwa

atajipamba. Huo ubaguzi, huo mnyanyaso tunataka majimbo tuwe sawa kielimu bairi ya mume na mke. (**clapping**). Tumekataa kata kata kwa sababu licha twaijua na taabu za nyumbani tumeachiwa ndugu zetu waishia mafuoni na hawaji nyumbani wakiwa ndio mabwana zetu. Kwa hivyo wakihitaji majimbo ya kiislamu watulee kama waislamu wasituwachie tu uhuru kwa sababu tuko wanawake tukae hapo majumbani na mishahara hakuna, twaambiwa hakuna kitu mambo ni magumu. Kwa hivyo akina baba wa Pwani mtake majimbo na mtutilie maanani kama wazazi wenu. Na tukipewa vyeo sisi wanawake twaambiwa mara nyingi mwanamke ni mtu wa kujifunga funga. Hakuna kujifunga funga. Tumeona na tumeshuhudia, tunataka majimbo tuwe sawa na kiuchumi kama wanawake na kama binadamu asiyo na tofauti na mwingine. Majimbo yasibague hata mwanamke hata kiwete, hata kipofu, kulingana na juhudi zake na uwezo wake apewe ajira sawa na uhai wake. Kwa hayo machache asanteni. (**clapping**).

**Com. Swazuri**: Asha Ali.

**Asha:** Asalaam aleikum. Kwa jina naitwa Asha Mwakurauka Ali. Mimi ninataka majimbo. Kwa sababu tumeona sisi akina mama tunanyanyaswa hasa hususan akina mama wa Pwani tunanynyaswa. Na sisi tumekaa tumeona tunataka majimbo yetu. Tunataka majimbo yetu kwa sababu sisi tunapiga vifua tukisomesha watoto wetu. Tunataka jimbo letu na sisi tupate uwezo wa kufanya kazi tusomeshe watoto wetu. Asalam aleikum.

**Salim**: (Talks in Digo)

**Com. Swazuri:** Ongea na Kiswahili.

**Salim**: Haya nimekubali. Nimekuwa na furaha sana kwa sababu hapa nimekuwa nyumbani. Kwanza jina langu kama nilivyosema ni Salim Hassan Mwabashiri kutoka Kionondo location, villge yangu ni Kilole. Nazungumza haya niliyotumwa kwamba nenda ukawakilishe sisi tuliokutuma. Wajibu ni majimbo sote tunaakaa hapa fikira zetu ni majimbo. Ya nayo zungumzwa ni majimbo. Sasa yale maoni tuliofundishwa siku zile na mpaka sasa ni hivyo hivyo isipokuwa tumeyaandika tutayapeleka pale yaliyobakia ni kuongeza ongeza. Na yale nitakayoongeza ni yale yaliopitiwa na wale wenzagu. Sasa nami pia naongeza humo humo.

Kama nilivyozungumza kwamba mimi kule nili koni village Chairman. Lakini hata ukiniona njiani huwezi kujua yule ni nani. Kwa sababu gani? Sina kibali, sina badge, nina nguo, ni mtu tu wa kawaida. Hata matatizo yakitokea nyumbani nikisimama hapo mahali polisi akija ananiuliza "wewe ni nani" Ni nani vipi na mimindiye ninayejua matatizo yaliyotokea niko hapa karibu nawe, mimi nimefika hapa na kujua, mimi uniulize halafu nikuambie utariatibu ulivyo. Ukiniambia mimi ni nani toka huko mimi sijui habari yako.

**Com. Swazuri:** Ufanywe aje sasa?

**Salim:** Mimi nipate kibali.

**Com. Swazuri:** Halafu mshahara?

**Salim:** Mshahara ndio muhimu (laughter). Naam hapo ilikuwa ndiyo nia kwa sababu wenzangu wote waliozungumza wengine Chairman, lakini bado hawajagusa hapo na ninavyotaka ya muhimu ni hayo, na majimbo hivyo ninavyosema. Basi upande wa utamaduni pia. Utamaduni kuna mambo mengine hufanywa nyumbani kama kuaguana. Sasa mambo haya ya kuaguana wengine hutaka vibali kutoka kwa Chairmen au kulingana na chief huenda akapewa shilingi hamsini au mia moja ili waweze kuwakilisha. Lakini kwa sababu sisi tuko huru mwananchi afanye kazi yake tu peke yake bila kushangazwa na mtu yeyote. Anakwenda kufanya nini mzukani kule au mizimuni ameshika nini mkononi. Hebu simama mzee. Hiyo hakuna kwa hivyo nashukuru kwa hayo niliyonayo au niliyoyasema yatosha inshallah (**laughter).**

**Com. Swazuri:** (inaudible) Tuambie jina lako kamili.

**Juma:** Okey. Jina langu kamili naitwa Ramadhani Juma Dzitsai Sawa. Hilo ni jina la babu la kujikuza la mjua ni Mchawi. Sawa? Kwa ukweli kumezungumzwa mengi hapa ambayo tumeyasikia lakini huwezi kumpatia mtoto wako jina ikiwa wewe hukuzaa. Ni kweli ama uongo? Ni ukweli. Kwa hivyo nakuta yalivyozungumzwa hapa ni mengi sana. Lakini haitowezekani kwamba kwanza tupate majimbo ndiyo hii mikataba itakuwa. Na kama hatutapata majimbo itakuwa ni ovyo. (clapping) Kwa hivyo mimi naonelea kwanza kitu majimbo ni muhimu na hakuna ambalo litatendeka bila ya kupata majimbo. Itakuwa ni nyimbo. Tumeambiwa kutajengwa chuo kikuu hapo, hiyo ni nyimbo. Hilo litakuwa juu ya majimbo ya coast. Kwa hivyo napendelea kwamba, tunataka majimbo. Sio kuwa tutamfukuza mtu. No. Tunataka majimbo ili kujifanyia sisi wenyewe mapato yetu ya coast. Yamezungumza mengi na kama ninavyosema kwamba mtu yeyote ikiwa hajaoa hawezi kusema huyu ni baba wa fulani, mpaka uone. Kwa hivyo na sema hivi, kwanza majimbo halafu mikataba. Yote iliyozungumzwa hapa kabla ya majimbo hakuna chochote kitafanyika. Mimi nimeona watu wengi ambao tumezungumza. Kwa hivyo yote yaliyozungumzwa

lakini isiwe ni nyimbo kwanza majimbo halafu ndiyo mikataba, iliyozungumzwa ndiyo itatendeka. Sawa? Okey. **(Clapping**)

**Com. Swazuri**: Charo Ngumbao?

**Ngumbao:** Habari zenu. Mimi kwa jina naitwa Charo Ngumbao. Mimi natoka Kinango na nimekuja na ujumbe kutoka kwa watu wa Kinango. Wanasema wanataka majimbo. Federal system. Kwa sababu katika sera ya majimbo itawezesha asilimia tatu, ni ya total collection iwe itabaki katika jimbo – ¾. okey?

Halafu napendekeza katika tume hii kwamba Serikali ianzishe compulsory education system. That is kuanzia darasa la nursery mpaka standard seven iwe compulsory kwa sababu watu wengi wa hapa Pwani pia lazima tujilaumu. Tukitoka mambo mengine iendelee, elimu kwanza. Kwa hivyo kuwekwe sheria ya elimu iwe compulsory. Lazima.

Tatu, kuwekwe sheria ambayo viongozi wote wawe wako chini ya sheria. Hakuna above the law ati mimi ni above the law. No, no. Kuhusiana na land sheria za mashamba ziwe chini ya wenyenji individuals (clapping) Halafu tena pendekezo kuwa Chief Justice na Chairman of electoral commission awe anchaguliwa na committee ya bunge. Kwa sababu katika Katiba kuna sehemu fulani ambayo I cannot recall it lakini inasema kuwa Rais akidhibitishwa kuwa ni mgonjwa na daktari anatakikana ajiuzulu. Kwa hivyo katika Katiba ya sasa hawezi sababu Chief Justice anachaguliwa na Rais. Kwa vile amechaguliwa na Rais, yeye ni kama mtenja wake. Lakini kama amechaguliwa na watu vile wamechaguliwa atakuwa ni … kwa hivyo Chief Justice na Chairman of Electoral Commission wawe wanachaguliwa. **(end of side A**)

**Com. Swazuri**: (not clear)

**Juma:** Commissioners, waheshimiwa mabibi na mabwana. Mimi jina langu naitwa Juma Boga mzaliwa wa hapa Diani Location. Umri wangu ni miaka sitini na nane. Yu can imagine Bw. Commissioner sitine na minane. Na nikifanya hivyo nataka kusema kwamba mengi ambayo yamefanyika hapa Kenya nikiwa na umri huo wa miaka sitini na minane nimeona mengi yaliyofanyika hapa Kenya. Ndiyo sababu nimependelea kujitaja kwamba mimi nina miana sitini na minane ili kuonyesha kwamba mengi yaliyofanyika Kenya mimi nimeyashuhudia yakifanyika.N niko hapa kuwakilisha group yangu ambayo inaitwa

Dina. Dina si chakula. Dina ni kukazana maanake diyo neno hili DINA. Dina development welfare and advisory group. Dina maanake nasema si chakula cha jinoni. Mumeelewa eh? Asante (**laughter).**

Mimi nikiwakilisha group yangu ambayo ni sauti inayosimamia wazee, akina mama, vijana, wafanyanji biashara wakulima, wavuvi na kadhalika. Kwa hivyo memorandum hii ambayo niko nayo hapa imechukuwa maoni kutoka group hizo zote. Hawa wanasema kwamba wao wanataka mageuzo ya Katiba yawe yataleta mfumo wa serikali ya majimbo. Na wanataka hivyo kwa sababu hawatosheki, hawakutosheka kamwe na hii serikali ambayo sijui inaitwa ya pamoja. Serikali hii ya pamoja kwa muda huo wote iliyo utawala wao hawakufaidika nayao hata kidogo. Na wamegandamizwa, wamenyayaswa, wamefanyiwa kile jambo. Kwa hivyo wanasema seikali ambayo wanapendelea na wanaona kwamba itawafaidi ni ile serikali ya majimbo. Kisha weanasema kemaba ikiwa kwa bahati mbaya labda wezetu huko juu wanatosheka na serikali iliyoko, watu wangu wanasema wao wanataka jimbo lao. **(clapping)** Na katika serikali hii ya majimbo, wanasema jimbo likipatikaniwa liwe na serikali yake ambayo itakuwa inaongozwa na governor iwe na bunge lake la kutengeneza sheria, liwe na police force yake na kila kitu ambacho kinahusu serikali kuwa nacho. Hivyo ndiyo wanataka. Mapendekezo yao ni kamba sisi watu wa Dina tunataka utawala wa majimbo, na tunataka pia Kenya iendelee kufuata mfumo wa vyama vingi. Huo usife huo.

Com. Swazuri: Hawakusema ni ngapi?

**Juma:** aa aa wanataka vingi wao. Pia wanasema kwamba tunatambua kila jimbo liwe na serikali yake na katiba yake …..

**Com Swazuri**: Haya ushasema.

**Juma:** Nimeshasema ni vile macho yangu ni mzee na ngonjwa. Oke asante. Basi wanasema ardhi na kilimo, uchumi, elimu, utalii mali ya asili na afya na vyote hivyo viwe chini ya mamlaka ya majimbo. Hivyo nasema kwamba tukipata majimboule uwezo ambayo umerundikwa mahali pamoja kule juu, utatawanya kwa kila jimbo kuweza kujisimamia lenyewe. Nafikiri kwa hayo machache kwa sababu mengi yamesemwa na wenzangu laini sisitizo letu ni kwamba sisi tunataka utawala wa majimbo. Asante **(clapping)**

**Com. Swazuri:** Hayuko Salim Mwajora? Saumu Amani.

**Saumu:** Salaam aleikum. Mimi jina langu naitwa Saumu Hamisi Amani. Na lengo langu la kuja hapa nilikuwa nataka majimbo. Ndivyo nitakavyo na ni lazima iwe hivyo (clapping) kwa kusema hivyo mimi niko na uchungu sana. Mimi nilimaliza form 4, 1990 na mpaka dakia hii sijapata kazi. Na tukitembaea huko kwenye ma beach kwanza jambo la kwanza manager anakuuliza huyo aliyo hapa ni msichana ama ni bibi ya mtu.

Maswali ya kazi haijalishi kuwa ni msichana wala ni bibi ya mtu. Ukisema ni bibi ya mtu anakwambia mwambie aje siku nyingine. Ukimwambia ni msichana anakuambia wewe ni mwembaba ama ni munene. Maana ya umbo langu ismjalishe. Kwa sababu mimi nilisoma na stakabadhi zatu zinaruhuru kufanya hiyo kazi. Akiambiwa ni mwembamba unaambiwa ingia ndani ukiingia ndani anakuambia tukutanae Manor. Ofisi iko leisure lodge lakini anakuambia tukutane Manor hotel. Huo ni unyanyasaji ama ni nini?

Sisi wanawake ni lazima tupatiwe haki zetu na sisi tunataka kazi kufanya hatutaki mambo ya kukutana Manor. Tufanye nini huko? (**clapping)** Kama ingekuwa ni mjomba wangu huyo aliyekuwa hapo hotelini asingeniambia tukutane Manor, lakini kwa sababu ni mtu wa bara ni lazima aniambie tukutane Manor tufanye mambo mengine halafu ndipo ni kazi baadaya itawezekana aje? Pengine bwanangu hana kibarua na mimi sina kibarua mpaka dakika hii, nikipeleka application kwa nursing mimi na qualify, kuwa nurse wanaotoka pale ni language wanatoka B. Na language nilipita na mean grade pia nilipita. Lakini ukifika kwa interview ukiangalia katika ile orodha yote ya watu wa Kwale district pengine mtu mmoja ama wawili ama watatu ndiyo walienda college. The rest hakuna na tuna qualify. Why? (**clapping**) Hata sisi tunauchungu. Saa hii sina kazi na bwanangu hana kazi. Tutafanya nini. There is no need of learning for a girl. Haina haja ya wanawake kusoma kwa sababu tukisoma munaambiwa tukutane pahali pengine. Kama mimi mtoto wangu niliye naye ni msichana saa hii hakuna haja ya kumsomesha kwa sababu yeye atabaki nyumbani. Na uwezo mimi sina sababu sina kazi. Nitamsomesha na nini mtoto wangu ama babake atamsomesha na nini?

Na sisi tu wazaliwa hapa, beach ziko hapa tu chini ukifanya kosa kidogo mtu pengine amekosea ameogea choo ya mzungu. Mzungu si ni binadamu sasa kama umeshikwa na kosa kama hilo ni lazima upatiwe warning letter halafu arudishwe kazini. Kwa nini wanamfuta kabisa? Kama angekuwa ni mtu ambaye na mjua singemfuta. Lakini kwa vile hamjui ni mtu wa bara

anamwambia nenda kabisa. For what? Until when. Mambo kama hayo tumechoka sisi. Tunataka tuandikwe kazi. Hata mimi saa hii nataka niandikwe kazi sababu nina watoto wangu wanasoma. Nitawasomesha na nini? (**clapping**) (a lot of noise and discussions in the background).

**Com. Swazuri**: Mwanarusi?

**Mwanarusi:** Salaam aleikum. Niendelee ama bado muko na mazunguzo mazungumzo.

**Com. Baraza:** Hapana endelea mami. Sema jina lako halafu endelea.

**Mwanarusi:** Asanti. Jina langu mimi ni Mwanarusi Nliseso mzaliwa wa Diani Location. Mimi kama mwanamke mojawapo wa Kwale ama wa Pwani nilikuwa naomba tupatiwe serikali yetu ya majimbo kwa sababu zifuatazo. Laitani kama Katiba ilie iliyopata uhuru ambayo ilikuwa ni ya majimbo, kama ingekuwa hiyo hiyo mpaka dakika hii sisi watu wa Pwani hapa tungekuwa watu wengine. Lakini ilifinywa finywa hapo ikafutwa futwa ikatengenezwa kivingine sisi wanyonge tukawa tunagandamizwa. Tumegandamizwa sana mpaka dakika hii tunaumia mbavu, maana tumefinywa sana. Kwa hivyo tunaomba tupewe uwezekano wa majimbo ili tuwe na uwezo wetu katika jimbo. Tuwe na mamlaka yetu tuwe na mashauri yetu pia. Wakati nchi za ng'ambo zikitoa kama ni msaada, msaada ule ugawanywe kwa kila jimbo, kila jimbo likafanye mambo yake. Tumefinywa sana kwa sababu kama tungekuwa tunasaidika na hiyo Katiba ama huwo ungozi wa Katiba hio ambayo bado iko, mwaka huu ni wa thelathini na tisa Pwani hii yetu hakuna hata chuo kikuu kimoja kilichojengewa kwa watoto wetu ama kwa sisi wenyewe ( **clapping).**

Tukiingilia mambo ya utalii, utalii mwingi uko hapa Pwani, mahoteli mengi yamejengwa zaidi ya mia moja, lakini college yake iko bara. Sasa sisi wa Pwani nikuwa tutowe ardhi ijengwe mahoteli halafu wanaochukua ujuzi ni watu wa bara waje kuandikwa kazi huku? (**clapping)** Tukiangalia mambo ya ardhi, jimbo likipatikana ardhi zitakuwa mikononi mwetu tutakuwa tunasawazishana sisi wenyewe kwa wenyewe. Yule aliyepokonya mwenziwe atajulikana na mambo yatasuruhishwa.

**Com. Baraza:** Mambo ya mashamba, unataka uwezo uendee nani hata ukiuchukuwa kwa jimbo uwe kwa mikono ya nani?

**Mwanarusi:** Mikono ya wazee kwanza. Halafu ipande juu pole pole kama mambo yamekuwa magumu. Kwa hivyo sisi watu wa Pwani ama sisi wanawake tumechoka na ugawaji wa ardhi kwenye meza umekuwa hapo miaka nenda miaka rundi unangusha nazi, lakini kutakuja mtu kutoka bara na karatasi yake aseme hii shamba ni yangu angalia title deed. Tafadhali ugawaji wa shamba mezani uishe. **(clapping)**

Mengi yamezungumzwa nitazungumzia kidogo na kutilia mkazo. Nikuzungumza kuhusu huu ubakaji wa watoto. Watoto wanaonajisiwa. Sheria imetoa kifungu maalum cha kuwa mtu atakaye najisi mtoto mdogo vifungo vinatolewa kila kukicha. Na kila kukicha watoto wananajisiwa. Kwa hivyo tunataka sisi wanawake hasa wa Kwale ama wa Pwani, tukishapewa jimbo letu, uwezo utakuwa umewezekana kutoa amri. Ama basi kama ni hiyo serikali ya pamoja lakini hiki kifungu kiwekwe mkazo hapo kiwe kimefungwa sawa sawa ili hao wanaume wapendao kutafuta watoto wadogo,

**Com. Swazuri**: Ungependa wafanywe nini?

**Mwanarusi**: Mimi ningependa kuwe na adhabu mbili mojawapo apewe huyo aliyefanya hivyo. Huyo aliyembaka mtoto. Ya kwanza afungwe maisha. Kama haikuwezekana basi imekuwa too much kwake maana wengine huwa wanaendelea hata kesi zimekuwa tatu tatu, inne, tafadhali hizo sehemu zake za siri zikatwe. (**laughter, clapping**)

Nikimalizia ni kuhusu mambo ya kazi. Kazi zipewe uwajiri watu wote. Wake kwa waume, hata walemavu tunaona lakini wamebaguliwa ati kuna kazi zingine hawaziwezi. Kwa hivyo nasema asante kwa hayo machache.

**Com. Baraza:** Kasunge Hassan. Hayuko? Asman Mwayuyu? Musa Mwarayulo. You highlight your memorandum.

**Makoroma:** Okey, Kwanza kabisa mimi ni Makoroma na moja kwa moja nitaenda kwa point direct. Kwanza serikali ya majimbo ndiyo kitu naunga mkono na majimbo ambayo nayataka mimi ni haya. Majimbo tisa katika Kenya nzima; haya yaliyoko yatabakia vile vile lakini kama Rift Valley kwa sababu ni kubwa itakuwa na North Rift na South Rift. Halafu majimbo haya hayatakuwa na Governors; lakini kutakuwa na Chief Minister. Huyu Chief Minister atachaguliwa na raia direct na wananchi wa ile jimbo. Na kila jimbo litakuwa na bunge lake na bunge litakuwa lina idhini la futa kazi mtu ambaye atakuwa ameajiriwa kama civil servant ama muajiriwa wa serikali. Halafu bunge lile la jimbo litachagua makamu wa Rais ambaye

atakuwa vice Chief Minister katika hizi district ambazo ziko sasa hivi hazitakuwa na ma DC, wala ma DO.

Katika ile serikali napendekeza mimi, hawa wataondolewa halafu district itakuwa inawakilishwa na Chairman ambaye atakuwa nachaguliwa na Rais wa jimbo halafu it should be approved by the parliament. Lile bunge pale lihakikishe ule mtu amechaguliwa sails through, na lazima awe ametoka sehemu ile. Halafu ma-councillors. Macouncillors watachaguliwa direct na wananchi. Kila wilaya itakuwa na Mayor wake na atachaguliwa direct na watu lakini si ma Councillors, kwa hivyo kila mahali kuwe na mayor. Kuhusu Central Government kutakuwa na Rais ambaye atachaguliwa na raia direct halafu na Prime Minister.

Prime Minister atachaguliwa within the parliament na atakuwa yeye ndiye mtu ambaye anauwezo wa kushika jeshi na atakuwaa nahusika na mambo ya fedha. Iwapo nchi iko katika vita huyu Prime Minister atatangaza vita lakini vile vita lazima amwambie Rais kabla ya masaa arobaini na nane na lazima pia azungumze na bunge la central kabla siku nne (4 days).

Jambo lingine ni kuhusu wafungwa. Wafungwa ni lazima wawekwe katika hali ya kibinadamu ni lazima wawe na vitanda ni lazima wapate postal address, kwamba lazima wawe na access ya kuzungumza na watu wao na ni lazima waruhusiwe kuangalia televisheni na kusikiliza maradio.

Jambo lingine ni kuhusu habari ya Police harassment. Police harassment ni lazima ihakikishwe kwamba kutakuwa na Police force ambayo sasa itakuwa inaangalia mambo ya harassment, ya kunyanyasa watu, yaani a special unit. Halafu kwa special unit kutakuwa na ofisi ya Ombudsman. Ombudsman atakuwa na ofisi yake katika kila district kuangalia hali ya violations ama vile haki za kibanaduam zinavyokuwa violated.

Jambo lingine ni kuhusu habari ya education. Elimu iwe free from nursery mpaka form 6 na system ile ya zamani kuanzia nursery upto class 7, form, one upto form 6. Halafu kuanzia hapo sasa ni university sasa elimu ya university ni lazima iwe affordable kila mtu aweze kusoma.

Jambo lingine ni habari ya Waislamu. Waislamu baraza la Imam ikuwe chombo cha kudumu na kitambulike na Serikali. Wachague Kadhi wao wenyewe, baraza la Maimam. Halafu na Kadhi wadogo wadogo pia watakuwa wanachaguliwa na baraza la Maimam la taifa nzima. Na kuhusu Waislam ni lazima ihakikishwe kwamba waalimu ama maustadhi wanapelekwa

kule mashuleni. Wawe payroll ya TSC kwamba watakuwa wanasomesha masoma yote ya Kiislam. Iwe ni fiki Arabic, kila kitu. Na watakuwa wanalipwa sawa sawa (clapping).

Na issue lingine ama swala lingine ni kuhusu habari ya Ramadhani, mwezi wa Ramadhani. Unapofika kama vile watu wahakikishe katika shemu za Kiislam, madanguro yote, mukahawa yote ifungwe. Hakuna kula mchana. Ukishikwa unakuwa sentenced ama unafungwa mwaka mmoja. Wakati unakula mchana mwezi na Ramadhani.

Issue nyingine, Rais anapochauliwa na Prime Minister wake ni lazima wawe baina ya miaka 40 upto 65 years. Hiyo ndiyo age ambayo tunataka. Swala lingine ni Rais kuwa na excessive powers ama nguvu zaidi ni lazima ziwe cut off ili to have checks and balances.

Swala la Mwisho ambalo nataka kumaliza kabisa ni kuhusu habari ya beach. Mambo ya beach hapa ni matumaini yangu kuwa watu wamekuea harassed mara kwa mara. Na ningeomba badala ya kuweka askari kule, sungu sungu lazima wawe kule chini na ni lazima walipwe na serikali. Nasema homeguards, unaona? Lazima wawe kule chini na pia huku manyumbani sungu sungu lazima waihidhirishwe, sio mambo ya Mungiki ndio waleta shida halafu inaonekana it has become a collective fault. Kwa hivyo homeguard lazima wafanye kazi na wawe payroll ya serikali. I hope its clear.

Cha Mwisho tafadhali kuna hawa village Chairmen, kwa sababu ile serikali mimi nafikiri ni kwamba hawa ma DO lazima waondolewe hawana kazi. Chief atakuwa answerable kwa yule Chairman (si DC tena) ni yule Chairman atakayechaguliwa na Rais wa jimbo halafu atakuwa approved na bunge la jimbo sasa yule Chairman ndiye atazungumza direct na Chief lakini yule Chairman hataitwa Chairman huku ataiwa mwakirishi sasa atakuwa pale analipwa atakuwa anaonge ana Chief halafu anaongea na Chairman ambaye sasa hivi ni DC.

**Com Baraza:** Na huyo chief awe elected?

**Makoroma:** Chief anakuwa elected na watu direct nakuwe na kamati wakati Chief yeye hatimizi kazi yake uzuri then ile kamati iitishe uchaguzi, anaa ireport kwa makao makuu halafu kuna kuwa na uchaguzi mpya then he is thrown out. Thank you very much (**clapping**)

**Com. Baraza**: Hilda Nzambia? Salim Bakari Mwachata.

**Mwachara**: Salaam aleikum. Mimi kwa jina langu naitwa Salim Bakari Mwachala. Kwanza swala langu la kwanza ningetaka majimbo. Majimbo ndio yatakoyoleta yale tunayotaka sisi. Kama mzee wangu amezungumza hapa, amesema kwamba majimbo twataka kwa hiari kwa nguvu kwa sababu tumechoka. Kwa sababu majimbo ya kija ndiyo yataondoa mambo mengi kama ukimwi, ukimi umezagaa hapa kwetu kwa sababu ya serikali ya mseto. Wakina wamama wetu zamani walikuwa wakivaa mavasi mazuri na ilikuwa uzinifu kwao si jambo rahisi, lakini sasa hawa wanawake wamekuja kutoka bara wanatembea uchi ndiyo wame sababisha ukahaba umekuwa mwingi hapa kwetu Pwani (**clapping**) .

**Com. Baraza**: Hao mama wakutoka bara watarudi kule?

**Mwachara**: Kile watakaa hapa watapata umri za hapa za kuvaa mavasi yakueleweka, hivyo ndivyo tunavyotaka (clapping). Kwa sababu mwanamke ukitembea uchi ndio unasababisha wanaume kukutamani lakini ukijivaza hakuna problem.

Kitu chingine ambach nazungumzia ni kwa upande wa elimu, nitaunga mkono mwenzangu kwamba watu washomeshwe bure kwanzia class ya kwanza mpaka form 4. Kwa sababu sisi huu umasikini umsababishwa na watu wa bara kwa sababu hawa watu wa bara ndiyo wametukalia muda mrefu. Sisi si maskini umasikini ni watu binafsi kwa sababu rasilimali tunazo hapa kwetu Pwani ni za asiri zio kwamba niza kupita kwa sababu bahari huwezi kuitembeza wala, huwezi kuihamisha.

Kilindini vile vile hivi viwanda vyote vina uwawa ilituwe masikini. Watu wote wa hapa hakuna hata mtu aliye kuja na gari sote tumekuja na miguu. Tumefanyishwa tuwe hivi sio kwamba sio sisi…….. tumefanyishwa. Kwa hivyo tumechoka kunyanyashwa tunataka majimbo kivyo vyote Salaam aleikum (**clapping).**

**Com. Baraza:** Bw. Ramadhani Zani, Salima Omar.

**Salima:** Jina langu naitwa Salima Omar kutoka Diani, mim maoni yangu ni ya majimbo. Sisi tumezaliwa hapa Coast. Wazi wetu wote wamehudumia mambo ya beach, kina babu zetu, hata sisi wenyewe twa hudumia mambo ya beach lakini sasa mtoto akienda beach yeye mwenye anaenda kuuza sanamu zake mbili polisi wa Diani akimuona kijana yule, atasimamisha amwambie

"wewe leta kitambulisho, na wewe hebu leta kitu kidogo". Sasa saa ile akimpatia kitu kidogo ambacho ame patiwa na yule mzungu ameuza sanamu atakuwa amefanyia yule Polisi na yule Polisi yeye fuko na mshahara wake ama itakuwa amejifanyia mwenyewe?

Sasa mimi naomba Polisi wa Diani wapewe maonyo kuhusu watoto kule beach. Waachiwe waendelee na biashara zao kulingana nao na uchumi, wao kila mmoja yuataka maendeleo. Coast hii ina maendeleo makubwa lakini kulingana na wale wenzetu wageni ambao wamekuja hapa huwa wao wanataka sisi tukae chini wao wake juu kama kwamba wao ndio wazaliwa wa hapa. Wazaliwa wa hapa wawe hawana nafasi yoyote. Sasa mimi nataka kuanzia hiki chama chetu watoto wetu wawe na maendeleo kama ni mahotelini, kama ni beach boys, kama ni akina mama wakiuza maleso yao, sio ma Polisi saa yote wasimamie akina mama ati wewe nipe kitu kidogo. Hiyo hakuna kila mmoja yuatafuta uchumi. Na sisi tunataka majimbo. Na kulingana kutaka majimbo sisi ni wale wenzetu wanataka kujifnaya wao ndiyo wenyewe sisi sio wenyewe. Kwa hivyo nimemaliza sina mengi. (**clapping**)

**Com. Baraza**: Salim Muindi, Salim hayuko? Rajib Nassir.

**Nassir:** Salaam aleikum. Mimi kwa jina ni Rajib Nassir Bodo kutoka Diani Mwaroni. Sitaki kupoteza muda kwa sababu mengi yamezungumzwa. Sasa kama nitatia yangu sitaona jambo la maana. Shida yangu ama pendekezo mahitaji yangu ni majimbo. Majimbo ninayo hitaji kwa kwaida ni rasilimali zote za hapa ziwe zitapitia mikononi mwetu. Sio kama hivyo wakati huu ninavyoona tumkuwa kama ngazi za kupandia watu juu. Sisi tukanyangwe watu waende juu.

**Com. Baraza**: Zikipitia mikononi mwenu, mubakie na ngapi na sisi wa juu tubaki na ngapi?

**Nassir:** Ninavyoona mapendekezo yangu kwa sababu tumechokeshwa ni zote zimbaki hapa (clapping) Umeona mama? (interjection Com. Baraza) Mushakula kutoka kitambo bwana. Tumechoka mpaka mambega yao chungu sasa. Kule kuwabeba mpaka dakika hii hatuwezi kuwabeba tena. Kwa hivyo hatuwezi kuwabeba tena. Andika hiyo mama. Si uandike, watu wa Pwani wamechoka kuwambemba watu wa bara.

**Com. Baraza:** Nimeandika.

**Nassir:** **A**ndika mama ni maoni yangu. Na kwa kifupi sitakuwa na muda mrefu sana sababu yote yamekanyagwa kanyagwa na wenzangu. Nina mengi lakini hapa leo nitakuwa mnyonge. Lakini tumechoka.

**Com. Baraza:** Haya haya

**Nassir:** Andika tumechoka mama, ndilo langu la Mwisho **(laughter**)

**Com. Baraza:** I know how to do my work. Nenda hapo using, Hamisi Rasa

**Raso:** Asalaam alaikruim…… Na wale ambo si Waislam, amani ya Bwani iwe nanyi. Kwa jina mimi naitwa Hamisi Juma Raso, na mimi ni mzaliwa wa hapa Diani location, Ukunda sublocation. Kwa kuchangia mambo ya Katiba, Kwanza mimi nataka majimbo mwaandika ama mwazungumza? Kwa sababu haya maneno sisi wenzenu hata mukituona twatetemeka kwa ule uchungu.

**Com. Baraza:** Wewe endelea.

**Raso:** Twataka majimbo, hiyo iandikwe. Halafu kwa nini watu wote wakija hapa wanasema wataka majimbo? Ni kwa sababu serikali iliopo hatuoni ina faida yoyote. Na majimbo kuyataka sio kwamba twazua bali huu ni mkataba uliowekwa huko Lanchaster House in 1962. Wengine wanasema in 1963. Yaani mwaka wa elfu moja tisa mia sitini na mbili. Hapa kuna confusion kidogo wengine wanasema mwaka wa elfu moja tisa mia sitini na tatu. Lakini point ni kwamba kwa huo mkataba wa majimbo uliyowekwa Lanchaster house sio jambo la kubuni. Watu wakija wakisema majimbo … majimbo hiki ni kitu kilikuwapo. Kwa sababu gani tunataka majimbo? ni kwa sababu ule unyonge twauona hapa tumezingatia ama tukifikiria kwamba, mambo yote yataondoka. Kwa sababu ya elimu, tumeachwa nyuma mfumo uliopo haujatusaidia sisi.

**Com. Baraza**: Sasa usema point zako. Tumeelewa mambo ya majimbo. Hiyo ya elimu unataka nini?

**Raso:** Elimu twataka vyuo kama hizi university zijengwe hapa. Kutokea uhuru ni jambo la kutukana mpaka dakika hii hakuna university. Hata chuo hiki cha Waalimu kidogo tu kilicho shanza hapa, kimeanzishwa kingine huko Taita, kime kufa kimfifia

kwa hivyo elimu tunataka vitu kama hizo viwepo.

Kwa upande wa security. Security, serikali iliopo vifungu vilivyopo pengine vipo ambavyo vina ruhusu kuwe na homeguards, yaani sungu sungu. Lakini pengine vile vifungu vipo vimekuwa weak. Kwa hivyo twataka ile serikali itakuja ya majimbo vifungu kama hivyo za security, wenyenji wenyewe wawe na jeshi maalum la homeguards ambalo litachaguliwa. **(clapping**) Na ninasema hivyo kwa sababu mimi nikiwa na ujuzi ama experience ya hiyo, nimefanya hiyo kazi mimi Tumechaguliwa na nikafanya hiyo nikaona mafanikio ya kuwa wenyenji wa hapa lazima wawe wenyewe kipawa mbele kwa upande wa security.

**Com. Baraza**: ok next point.

**Raso:** Next point, upande wa kazi. Mimi nafanya upande wa private sector lakini utapata uhuru ama siku ya labour day vifungu vilivyopo ama mfano wa serikali iliopo, ni kwamba utaona maneno yote ya maana ama nyongeza zozote ambazo zinafanywa pale huwa zinalenga tu upande wa civil servants, ambayo hii si sawa. Kwa hivyo serikali ambayo itakuwepo lazima ilenge upande wa private sector na civil servanta wote wawe wanapata nyongeza. Nikiongezea hapo hapo mwanadamu kufanya kazi ni lazima kuwa off situ moja haitoshi, mfanyi kazi yeyote awe atakuwa off. Off day ziwe ni two days instead of one day. Utapata hawa wenzetu jumamosi na jumapili huwa ni siku za off, lakini sisi hata ambao tuko upande kama wa private sector hasa kama nitakuwa off jumatano halafu next day ni Thursday niwe off hivyo hivyo. Yaani kuwe na kufungu fulani ambacho mtu hapa Kenya awe ataruhusiwa kwenda off siku mbili. One day is note enough.

**Com.Baraza**: ok. That’s enough.

Kumalizia, swala nyeti kabisa la ardhi. Sasa hii majimbo inapiginiwa halafu hizi system zimetumika huko nyuma ziwe basi katika hii mambo ya Katiba ambayo imelekebishwa hapa. Swala la ardhi zote zilizo nyakuliwa ziwe zitakuwa revoked. Hii ndiyo faida. Hakuna maana ya kuwa mimi nije niongee hapa mamo ya ardhi, tunanyanyaswa, halafu majimbo ya kija iwe itaendelea hivyo hivyo. No. hiyo system yote yakufinya iwe ardhi ambazo zimechukuliwa kiholela ovyo ovyo ziwe zitakuwa revoked.

**Com. Baraza:** Sawa, endelea.

**Raso:** Next namaliza.

**Com. Baraza:** oh time is up, tuna watu wengi ambao wanataka kuongea.

**Raso**: Its up, ok thank you so mu lakini naomba mwenyezi Mungu maneno haya yawe yatafuatiliwa. Majimbo twataka kwa nguvu, kwa pole pole jamani. Asalaam alaikrum.

**Com Baraza**: Bakari Ali Manjeni, Huyo Bakari yuko?Lela Kassim, yuko? Atafuatiwa na Rashid Mtama. Dakika tano.

**Lela:** Salaam aleikum ndugu Waislam. Na ndugu zangu msiokuwa Waislamu mumeshinda aje? Nina shukurani kubwa sana kwanza kupata fursa hii ya kupata siku hii ya tamasha ya kuchangia mkataba mpya wa majimbo wa Katiba. Pendekezo langu mimi kupitia akina mama wa Diani location ni kwamba sisi akina mama ndai letu la kanaza tunadai mwamba wetu wa Pwani tuwe nao mkononi ili tuweze kufaidinda nao. Kwa sababu tofauti tofauti. Mwambao huu wa Pwani ni Mwambao mzuri sana uliopambwa kwa ajili ya mwenyezi Mungu. Lakini ni mwambao usiotunufaisha kwa lolote wala usiyotufaidisha kwa lolote. Kwa hivyo twaomba mwamba huu uwe mikononi mwetu, ili tuweze kumiliki mwenyewe na tuweze kufaidika vilivyo tujue faida ya mwamba wetu.

La pili, sisi akina mama wa Diani tumekaa na tukachungulia kirefu na vilivyo, tukaona ipo haja ya serikali ya mseto ikiwezekana tuiondolee mbali na tuwe na serikali ya majimbo(clapping) kwa sambau ambazo zinafautia: Serikali ya majimbo itamfanya mama ya Pwani afaidike vilivyo.

**Com. Baraza:** Hiyo ni sawa tumelewa … ziko point?…

**Lela:** Point ziko Madam. Kwa hivyo tafadhali naomba unipe time kwa sababu situmii kitu kingine natumia ile hewa ya mwenyezi Mungu.

**Com. Baraza**: Sawa lakini ni time …. Umesema majimbo tumeelewa go to the other points.

**Lela**: Ndiyo hivyo naja. Kwa hivyo taratibu wajua uki ni harass nitashindwa vile nataongea pia.

**Com. Baraza**: I'm not harassing you I am directing you.

**Lela:** Sasa nitarundi pale kwa majimbo. Majimbo yetu yale tunayoataka sisi tunataka Mbunge wa Pwani awe ana bunge lake na anaweza kuhamasisha wambunge wote na kuzungumza wakiwa na ofisi zao badala ya kuwa viruka njia kila kukikucha sisi twawahitaji na wamekwenda city. Huku tumeachwa na city yetu ambayo haina faida kwa wabunge wetu (clapping)

Majimbo yale tunayoitaka la pili, tunataka hata wale ma askari kupita askari tawala, mapolisi na ma PC, DO. Pia tuwe na uwezo wa kuwa jimbo hili linajimiliki viwavyo, kulingana na sector hizo zote.

Jambo la tatu, akina mama wa Pwani tunaona kuna jambo ambalo ni lazima tuwe nalo lakini sijui hawamini tunanyimwa haki hizo. Unafurahi wewe ni mama umetoka bara na unafanya kazi ambayo kwamba huenda ikawa umeifanyia kutoka huko, sio geni kwako. Kwa akina mama wa Pwani mameomba nafasi za viti arobaini kwenye bunge. **(clapping**) La pili akina mama wameomba katika council waachiwe viti kumi na vitano **(clapping**)

**Com. Baraza**: (inaudible) … endelea.

Akina mama wa Pwani kuna unyanyasaji wa uwajiri kupitia akina mama wa kawaida mpaka walemavu. Kwa hivyo narudi kwa walemavu. Mama akiwa mlemavu, tunaiomba serikali imushughulikie kupitia kwanzia kwa watoto wake iweze kuelimisha watoto wa walemavr. Na mama akiwa mlemavu anayo haki kuajiriwa vilivyo. Kwa sababu kile ni kiumbe kilochoumbwa na Mwenyezi Mungu na kiko timamu. Isipokuwa ulemavu ni rehema yake Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo tunaomba akina mama walemavu watiliwe maanani na waajiriwe vilivyo na akiwa Mwalimu, na akiwa anonekana ana haki ya kuwa officer kwa ofisi awekwe ofisini wala asiwekwe kama mtu asiyekuwa na maana **(clapping**). (Com. Baraza: dakika moja) Jingine ni swala la ardhi.

**End of Tape 4.**

**Tape 5** (has started before speakers name)

**Speaker:** Nasema hali ya security Askali wetu wafanywe waweze kuheshimu raia. Ma wabunge na machief wachaguliwe kwa mlolongo ili waweze kuheshimu wale wanaowachagua . Kwa hayo machache naona nisije (inaudible) nanyi asanteni.

**Com. Baraza**: Tuachie memorandum tutasoma. Sign pale.

**Speaker:** I will give it to you later on this is a rough one.

**Baraza:** Said Ali. Dakika tano.

**Ali:** Salaam aleikum. Nashukuru wakubwa wa hii Katiba. Langu muhimu la kusema hapa mbele yenu ni majimbo. Majimbo ndiyo yana niumiza mimi roho yangu sana. Kulingana na hali ilivyo nimefika hapa hasa kuja kuzungumza majimbo. Maneno yote hayo ambayo yamezungumzwa hapa mbele na wakumbwa na wandogo na wasichana na akina mama hayawezi kupatikana mpaka majimbo kwanza. Lakini unaona wengine wanaanza kupanga serikali zao hapa, kupanga sheria za nini hapa hizo zote ni uongo. Mpaka ipatikane majimbo kwanza ndipo mutaweza kupanga maneno yoyote hayo **(clapping)**

**Com. Baraza**: Tuanelewa lakini wapange na hiyo Katiba tuliotengeneza tunapanga malipo na hizo vitu vingine. Wasiachilie kwa sababu tunapanga?

**Ali:** Kwani, hapa ndipo pana akili zao ama wakifuata majimbo akili zitakuwa zimekufa.

**Com. Baraza**: Tutatengeneza Katiba na tutwapatia hiyo majimbo na lazima iwe na hizo vitu zingine.

**Com. Njoroge:** Na pia binadamu aliyekuwa akifanya (inaudible)

**Ali:** Nimesikia mtoto umuleavyo ndivyo akuavyo wakati ambao watu waliishi hapa wameona haya yote. Hawawezi kusema mengine ama kapanga mambo mengine. Lazima watapanga vile wanavyoona.

**Com. Njoroge:** Sasa wewe unasaidiwa … sasa wewe tunakuambia serikali ni ya majimbo ndiyo. Lakini zisopeowekwa sheria zote kabla ya hiyo serikali kuanza wale waliyo juu, yale yale madhara …. Hata huku unaona wengine ….

**Ali:** Haya nimesikia kwa sababu mgaa gaa na upwa hali wali mtupu. (laughter) kuendelea mimi hasa kusitiza ni majimbo. haya yote ya ardhi, ya kazi ya nini, hiyo tunaweza kupanga kulingana na kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho ni cha Koran pekee. Koran ina mambo yote ya sheria, zote hizo ambazo zimezungumzwa hapa. Ka hiyo majimbo kwanza ya pili yanayofuatia mimi ambayo naisisitiza na niko na uchungu sana ni kitabu cha mwenyezi Mungu ambacho ni Korani ndicho majimbo yakipatikana kitumike kama sheria. Asante.

**Com. Baraza:** Saidi Mwalalo?

**Saidi:** Arabic greetings. Ama kwa ufupi mimi nataka majimbo ama sisi zote tumezungumzia majimbo. Na kwa kweli hili jambo la majimbo kwa jumla laonekana hata hii serikali ilivyo sasa yazungumzia majimbo, ki hivi: makabila ni arobaini na mbili katika Kenya lakini vyama ni arobaini na sita. Yaonekana wazi kila mmoja ataka kujimiliki ama kila sehemu yataka kujimiliki kwa hivyo inonekana hii katiba ya majimbo ikipitishwa, nafikiri hili zogo litakuwa limeondoka. Kwa mfano waliotawala wa kwanza, ukienda huko Gatundu, utafikiri ni uraya. Halaru ukienda mkoa a Rifit valley…..

**Com Swazuri:** Hapo nitakupinga.

**Saidi:** Utanipinga eh? Haya basi tuachilie hapo hapo. Haya nikisema majimbo nafikiri nimetilia maanani kwamba ukiangalia wote walio bunge wana (interjection inudible) Haya niko na wewe.

**Com. Njoroge:** Kidogo tu, wacha nikutatize ukienda Gatundu, hakuna umasikini ulioko ma Gatundu kwa sababu tulienda kusaidia wale walio karibu na yeye na jamaa yake. Na hukondiko kuna maskini zaidi.

**Saidi:** Haya basi haya yote nafikiri kwa kukusaidia ni kwamba kila kabila lataka kujitawala kimajimbo. Mfumo huu wa majimbo kiufupi kwa sababu wengi wamezungumza kuhusu majimbo. Pia naonelea majimbo haya mgeni aidha atoke mbla atoka uraya lakini ameingia ki majimbo kwa sehemu ile za majimbo pronvinces nane zimekatiwa kimajimbo awe anatoa ushuru. Ili kufaidi yule mkaazi wa pale. Kwa mfano itakua kuna harambee, yeye badala ya kutoa harambee ya hapa atapeleka kule

alikozaliwa, sasa si ni majimbo tayari?

Sasa naonelea kwamba yeyote atakayeingia hapa ikiwa sasa serikali ya majimbo imekumbaliwa sasa tunamkata ushuru. Either 20% ama 40% itategemea wakaazi wenyewe kwamba mgeni huyu akatwe pesa ngapi.

**Com. Baraza:** Na huyu mgeni anakuja ku…..

**Saidi:** Either atoke mbla ama ataka uraya lakini ameingia kwa kimajimbo laima tumkate ushuru 20%.

**Com. Baraza:** Hata nikija kulipa hapo kwa hoteli yenu ya jimbo lenu munanikata ushuru?

**Saidi**: Sasa mkaazi umekuja hapo, na hata wabiashara bado naja. Hata biashara za utalii ikiwa sio ya mwenyenji wa hapa lazima sasa hiyo ikatwe imiliki wenyenji walio pale.

**Com. Baraza:** Na mgeni ambaye anafanya biashara ….

**Saidi:** Naam. Naja. Nakusaidia wewe. Na mkaazi wa hapa hapa mwenyewe ikiwa yeye ameajiliwa lazima akatwe ushuru kumsaidia yule ambaye hana kazi. 20% hivyo hivyo. kwa sababu ya nini? Mimi nitakuwa sina kazi ninataka kumlea mtoto na mwenzangu pengine ana kazi pengine ya kimagendo, am amehonga, sasa na yeye lazima akatwe 20% ili kumsaidia yule ambaye hana kazi yoyote. Hiyo nafikiri itaweza kutusaidia.

Na tukiangalia mambo mengine nai upande wa ma DC, ma chief, DO. Hawa naona pia waondolewa maanake, tukichunguza sana hakuna kazi yoyote wanatufanyia bali ni village Chairman ndiyo anakusanya na kujua shida za mitaaa yake taabu ….. ushaona? Halafu yeye ndipo apatiwe uwezo pia msharara mkuba apewe yeye. Badala ya kuweka DO sasa angoja nini ikiwa Chairman wa village aweza kumaliza maneno.

Kwa hivyo mimi naona hii serikali ya majimbo ile katka mfumo ipelekwe kwenye vijiji badala ya kwenda kwa Chief ama kwa DO. Kwa sababu aliye na watu ni village chairmen. Kwa hivyo mfumo wangu mimi nasema majimbo haya yaanzie kwenye mashinani unaona?

**Com. Baraza**: Dakika moja.

**Saidi:** Halafu pia basi nikisema majimbo nafikiri kuna misaada mingi ya kuletwa lakini kwa mfano mimi sio mkaazi wa sehemu hiyo pengine mimi natoka shemu ya Nyandarua na nimekwenda kubeba msaada ule watoka Canada umeambiwa uletwe Kenya niaatangalia kule nyumbani kwanza. Kwanza mtoto wangu, bibi yangu, ndugu yangu kijiji, haya pesa hizo zote zinakuwa ufisadi katika mtaa wangu. Na balance pia tena badala ya kuwa kwa sababu nin wasi wasi napeleka kule kule nikafungue account. Basi inaonekana kwamba ufisadi unaletwa kwa sababu hatuna serikali ya kimajimbo. Nafikiri kwa yayo machache kuna wengi ningependa wapate nafasi ndogo ndogo wachangie haya mambo. Kwa hayo machache Salaam aleikum (Arabic).

**Com. Baraza**: Juma Ali?

**Juma:** Kwa jina kamili Juma Ali Guha. Kwa jina la maarufu Juma Acha. Nashukuru sana kufika mahali kama hapa nikiwa na machungu sana, ikiwa sisi hatutapata majimbo. kwa hivyo kitu cha maana tunataka majimbo. Natoa points mbili. Ya mwanzo, sisi tuna posta hapa tunalipa ushuru kila mwaka elfu moja mia mbili. Ajabu iko hapa. Ukienda posta kuchukua barua kuna kitu kimeibwa. Unapata parcel , Parcel zingine unapata zingine hakuna. Kwa hivyo hatufurahii jambo kama hilo. (interjection inaudible) Na wezi hao. Kwa hivyo tunaomba serikali ya majimbo irekebishe mambo hayo.

**Com. Baraza:** Mwizi hata kwa majimbo atakuwa anaiba.

**Juma:** Lakini angalia hiyo sasa. Halafu point ya pili. Sisi tuko na shinda sana hapa kwa hii mazingira. Tumekabiliwa na ukimwi. Kama akina mama na akina baba. Mtu akizunguka anaambiwa ni Malaya, mwenyewe ameamua kufanya biashara ndogo ndogo hizi kama kuuza tomato, analazimika anunu license. Ambayo license anatoa elfu moja mia nane, ambayo yeye mwenyewe ana elfu moja. Sasa inakuwa tatizo sana mama kama huyu, pesa ni ndogo, license ni pesa nyingi, sasa kitu kama hiki kinatutatisha sana sisi. Kwa hivyo tunataka serikali ya majimbo kwa hayo machache Asanteni sana.

**Com. Baraza:** Itamaliza ukimwi?

**Juma:** Ndio kwa sababu mama yule afanya biashara atasomesha watoto wake na itakuwa mengine yameondoka.

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Juma:** Ndio lakini unakuta kitu kimoja mwenye duka na biashara ndogo ndogo, sasa license ni ile ile akitoa elfu moja na mia nane.

**Com. Swazuri:** License iwe kwa wote?

**Juma:** No, ile license iwe ni wale akina duka pake yake lakini hawa akina mama wenye biashara ndogo ndogo wasiwe na license.

**Com. Njoroge:** Sasa kama jimbo litahitaji pesa za kuliongoza kwa sababu litakuwa na wafanyi kazi munataka elimu ya bure, hospitali iwe ya bure na humutaki license munafikiri hiyo itawezekana?

**Juma:** Hatukatai lakini shida iko hapa kidogo

**Com. Njoroge:** Nyinyi ni lazima muwe serious.

**Juma:** Kuna biashara kubwa…..

**Com. Njoroge:** License ….. atoe nini.. asidie kama ni ushuru watu wato ushuru wasaidiane.

**Juma:** Nimekubali.

**Com. Njoroge:** Kuwe na elimu ya bure na hospitali ya bure ……………….

**Juma:** lakini ni ……………. (noise)

**Kiio:** Commissioners mlio hapa na wananchi wa Diani hamjambo? Kwa jina naitwa Thomas Kiio. Mimi ni mkufunzi wa chuo ch ufundi cha Ukunda. Yangu ni machache tu maoni. Oni la kwanza ni kuhusu elimu. System ya elimu ambayo tuko nayo ambayo sasa iko Kenya, napendekeza kama ingerudi ile ya zamani ambayo ni kutoka class ya kwanza mpaka ya samba halafu inaenda form 4 mpaka form 6. Halafu unaenda university 3 years. Tukiwa katika elimu hiyo hiyo mimi kama technician. Technical education hasa katika Youth polytechnics, imesahaulika sana katika nchi yetu ya Kenya. Tuna vyuo mia sita na

themanini ambavyo viko mikononi mwa serikali. Lakini utakuta vyuo hivyo vyote havisaidhivi kama vile inavyostahili, vyuo hivyo vyote zimeachiwa wanakamati, vimeachiwa villagers ambapo hawawezi kusaidia na hawawezi kuendesha hicho chuo kulingana na standard inayohitajika. Kwa hivyo naomba jambo hilo la elimu la ki-technical, ili tufike kile kiwango kinahitajika cha viwanda mwaka wa elfu mbili na ishirini tuwe na technician wa kutosha. Hii elimu ya education katika technical iwe inadhaminiwa kikamilivu na serikali. (interjection inaudible) Kwa hivyo pendekezo langu ni kwamba serikali (interjection in audible, noise) okey nyamazini nitoe maoni yangu. Asante Bw. Com. narudia hapo hapo kwa technical. Nasema ya kwamba maoni yangu natoa Kenya tuko na vyuo mia sita na themanini ambazo ziko katika ministry of labour. Na vikiwa katika Ministry of Labour ni jina tu. Waziri yuko pale na vocational training lakini ni jina. Vyuo hizi zote zimeachiwa wanakamati. Wanakamati ndio wanashughulika na kuendesha vyuo hivyo.

Sasa tunaomba serikali ichukue jukumu ya kuelimisha mwananchi bila kubagua ati acadamic ndio inapewa bursaries na katika Youth Polytechnics kuna wanafunzi hawajiwezi na hawawezi kupata bursaries. Tunahijaji bursaries katika kila eneo ili maskini yule ambaye hawezi kumufadhili mtoto katika chuo cha ufundi awe anaweza kupata bursary na afundishe mtoto. Tuna jua katika maumbile ya binadamu kuna talents. Kila mtu ana kipawa chake na hatuwezi kuwa wote ma-pilots. Kila mtu anakipawa. Vipawa zote tuzikuze katika nchi yetu ili tupate taifa ambalo lina stahili, ili tufikie kiwango kile kinstahili cha viwanda mwaka wa elfu mbili na ishirini.

Upande wa agriculture. Sisi ni wakulima wa Kwale, tunakuza mimia mingi tukianza na bixa, korosho, nazi, maembe na machungwa. Lakini vitu hivyo yote vinaozea mashambani kwa kukosa soko. Sisi ni wananchi tunalimia tu yaani kutupa. Utakuta embe moja hapa tunanunuliwa kwa shilingi moja nikiwa mkulima. Lakini ukifika mahali una kuta ni shilingi ishirini. Sasa unakuta mwananchi hakulima hapati faida. Tunaomba jambo lili liangaliwe na soko zitafutwe.

**Speaker**: ………………………. Na chochote. Ili ku-discourage maonevu ya ukabila na mambo mengineyo. Halafu pia akiwa yeye anawachini wake pengine, tunasema awe na vice president ama, tunaisema nini ile tunaitaka? Aha Prime Minister awe mwanamke. Akiwa Rais ni mwanume Prime awe Mwanamke akiwa Rais ni Mwanamke Prime awe mwanaume. Ili twende bega kwa bega na nyinyi.

Halafu sisi tunataka wanawake wanaoolewa na kufiwa na mabwana zao waachiwe ule urithi wa bwanake, ili awalee wale watoto aliochwa nao, asifukuze (clapping). Hatutaki sisi. Tunataka awekwe pale ili alinde ule mji pamoja na watoto wake. Halafu kitu kingine tunasema, ile haki iliyoko pale iwe inaongozwa na mama sio watoto.

Haya mashamba, pia kama title deed inatolewa mzee amenunua shamba na ile mali tumechuma pamoja iandikwe bibi na bwana, ili ku-discourage uuzaji ovyo ovyo. Mahakama, tunasema mahakama dhuluma dhidi ya wanawake kuna wazee wengine wanatembea na watoto wao kwa nguvu. Kesi hizi ziachiwe zinfanyiwe akina mama, ndiyo ambao watahukumu hizo kesi. Tusiwape wanaume, maana wana huruma maana yale mambo ni yao.

Halafu tunataka university ziwe Pwani, utalii aiudi Pwani maana utalii woate uko huku. Msajili wa pesa yule wa national asisajili tu mara moja kwa mwaka kama vile ilivyo kwenye hii Katiba ya sasa. Awe anasajili hizo pesa akitoa report. Tena report iwe inaweza kusomwa na hata yule mama wa grassroot kwenye nation. Aeleza matumizi na mapato ya pesa za nation.

Haya, tunaendelea kwa utamaduni, hii niya Mwisho. **(Com. Baraza: inadible)** Huu utamaduni tunataka wale wanozuza wanaoagua kinyumbani wasikate karatasi ya kufanya hii kazi. Ikiwezekana wakitaka tu kufanya mambo yao waweze kufanya bora isiwe ni ya madhara tu. Kwa hayo machache, hii memorandum itaeleza mambo mengineyo Asante.

**Com. Baraza**: Juma Amri yuko?

**Amri:** Salaam aleikum. Mimi sitaongea mengi sana kwa sababu haja hasa ni majimbo. Na haya majimbo tunayotaka kwa njia mbili tuyapate kwa njia mbili. Tuyapate kwa hiali au tuyapate kwa nguvu. Kwa sababu tumechoka na kunyanyaswa. Kutoka Kenya hii ipate uhuru, mtu wa Pwani hana haki. Hata wasomi wetu, wako wasomi wa Pwani lakini hawajulikani kamwe. Ukimwambia huyu ndiye msomi kwa mtu wa bara ni vituko. Kwa hali hii ndiyo sisi tumekata shauri kutaka majimbo kwa hayo machache Salaam aleikum.

**Com. Swazuri:** Daktari Mwaramundu?

**Daktari:** Tume ya katiba, wananchi watukufu, mabibi na mabwana, hamjambo? Mimi katika kuchangia kwangu katiba hii

nasema hivi. Mimi nimechoshwa na serikali hii ya KANU. Sitaki kusikia serikali ya KANU kabisa. Kwa sababu hii serikali kwanza ilileta ufisadi pili haitambui mtu yeyote hapa Kenya. Mpaka sasa kitu cha pili ni kwamba watu wanakufa hospitalini na serikali iko. Ka hivyo mimi nasema serikali hii imenichosha. Afadhali watu wa Coast tupate serikali yetu tujiamulie sisi wenyewe mambo yetu. Kama ni beach hizo beach ni zetu, kama ni ndovu, ndovu ni wetu, kama ni kodi ya serkali iwe yetu, kama ni Port ni yetu kama ni kila kitu kiwe chetu. Kwa hivyo mimi sitaki watu wapate serikali ya majimbo nataka watu wa Pwani wapate serikali yao. Kama vile watu wa mbala walivyona serikali yao, Central government na sisi pia tupate Central government yetu. (clapping)

Kitu chingine sababu ya kusema watu wa Pwani wapate Central government yao ni kwamba kutoka 1963 utakuta hiyo DDC ya Kwale hakuna hata Mduruma mmoja anyeamulia mambo ya DDC hakuna Mdigo anayeamua mambo ya DDC. Kwa hivyo nina maana kwamba, nataka tuwe na serikali yetu kwa sababu Kwale DDC tujiamulie wenyewe, Mombasa DDC tujiamulie wenyewe, Lamu DDC tujiamulie wenyewe, Tana River DDc tujimulie wenyewe, Taita huko DDC tujiamlie wenyewe, hatutaki kuamuliwa na watu wa bara kabisa, kabisa nakataa. (clapping)

Kitu cha tatu nasema hivi sisi tumewaliwa na mtu anayeitwa Mreno. Tumetawaliwa hali ya kutawaliwa na kutawaliwa mpaka tukamalizwa kabisa. Hatujapumzika, tukatawaliwa na Mwarabu mpaka tukachoka, hatujampumzika utawala na Mwarabu tukatawaliwa na Kenyatta mpaka Kenyata akaja hapa hapa Mswambweni. Sasa tunatawaliwa na Moi … Kwa hivyo nasema hatutaki tena utawala huo wa Dictator. Ku- dictatiwa hii ni wazi. Lazima niweke wazi. Hatutaki. Tunataka serikai yetu kama serikali ijayo itavunywa. Lazima Katiba itungwe kwamba watu wa Pwani wapate serikali yao. Wajiamlie wenyewe. Kitu cha mwisho nasema hivi Wapwani wote wamekuwa maskini na sababu ni kuwa serikali sio yao, ni serikali ya watu wa bara. Ndiyo sababu ukaona hapa hakuna gari hata moja. Kama ni bara ingekuwa hapa kwenye Katiba kuna magari kama ishirini ama thelathini. Kwa hivyo tumekuwa maskini kwa sababu serikali si yetu.

Tunataka serikali yetu, sisi watu wa Pwani, nasi tujimulie wenyewe. Hatutaki kuamuliwa … Hatutaki kugawiwe … sijui 75% sijui nini … upuzi mtupu. Kila kitu kiwe hapa.

**Com. Swazuri**: (inaudible)

**Daktari:** Kila kitu kama ni kazi hapa, ndovu hapa, ni utalii hapa everything. Sitaki kitu kingine kiende mbala wala kiende Zanzibar kibaki hapa hapa. Kwa nini vitu vyetu viende huko. Twataka kila kitu hapa. Serikali ikivunjwa kule Nairobi bunge likuvunjwa basi sisi hapa tuwe na bunge letu, tuwe na wajumbe wetu, tuwe na ma councilor wetu tuwe na kila kitu chetu. Tumechoka kabisa kunyanyaswa. Saa zote twaenda Nairobi sijui Swazuri yawaenda wapi … sijui … upuzi mtupu. Kwa hivyo twataka serikali yetu. Salaam aleikum (clapping)

**Com. Swazuri**: Mwandarashi Jasho yuko hapa? Haraka baraka mzee. Endelea.

**Jasho:** Salaam aleikum. Mimi kwa jina ni Mwandarashi Jasho na kwa kweli serikali ambayo naitaka, ama tunaitaka wa Pwani ni serikali ya majimbo. Kwa kweli kutoka tupate uhuru tumepata taabu za kutosha sana. Hata kwa kweli ule uhuru vile tulivyoendelea kutoka wakati wa mkoloni ndivyo wakati huu tulivyo hivyo hivyo. Kwa hivyo tulikuwa tunasema hivi hii serikali inaonekana hii serikali ya Kenya sio ya watu wa Pwani.

Kwa sababu zile shida tulizo nazo sisi zinashinda hata wakati wa uhuru. Maanake uhuru ni ardhi ndiyo bendera. Lakini zilikuja zikauzwa na watu wa bara, inaonekana wao haja yao ni kuwa watutawale halafu wauze Pwani watufanye maskini. Kwa hivyo tunaona kwa kweli katika hali hiyo inaonekana kwamba hii Kenya na Coast imekuwa sio kitu kimoja ni vitu mbali mbali. Kwa vile katika historia yetu tunanjua ya Kwamba kuna Zanzibar ya Sultan iliyokuwa imevuka mwambao mpaka Mombasa Pwani. Kwa hivyo inaonekana hajo ya watu wa bara walikuwa wana haja yakuuza Pwani watufanye maskini kweli. Hata tukiangalia kila njia ambayo tumeifuata tumepata hasara. Tunaona watoto wetu tuliowasomesha hawana kazi, na sisi wenyewe pia maisha duni. Kusomesha mtoto ni taabu. Na ukimsomesha hapati kazi, kwa hivyo kwa kweli tungeomba wazi kuwa hatuwezi kupata jimbo letu la Pwani sio lazima bara, kama wabara wanaweza kukaa kwa umoja. Lakini wa Pwani wanahitaji jimbo ama uhuru. Jimbo likikosekana uhuru upatikane wa watu wa Pwani waweke bendera yao wafanye mambo yao. Maanake tunaona miaka arobaini ya utawala wa nchi hii tuna taabu tupu. Ma-beach yote yameenda Diani Complex imeuzwa. Ati imechukuliwa na serikali kujenga hoteli. Kwa hivyo huu mwambao katika hizi district saba tupatiwe uhuru wetu ikiwa hatuwezi kukubaliwa nchi hii ya Pwani kuwa na jimbo. Maanake tunaona wazi katika Pwani wabara wote wako Pwani lakini wa Pwani hawako bara pahali kwingine hawajulikani. Kwa sababu hiyo tunaomba katika hii tume ifikirie watu wa Pwani kuwapatia mamlaka katika

nchi yao kwa kila kitu.

**Com. Swazuri:** Kuna mengine wataka kuongeza mashamba nini jimbo na utawala tusha ongea.

**Jasho:** Lakini ni mara mbili. Jimbo tupatiwe ama tupatiwe free country. Wenyewe tupatiwe independea yetu tuweke bendera maanake tunaumia na serikali hii.

**Com. Baraza:** Tunaelewa hii mambo yeu sana na tunona iko shida. Ndiyo tunafanya hii kazi. Lakini kile ningewaomba ni kwamba, kama serikali imekuwa mbaya, imekuwa mbaya. Na sote kama wana Kenya tumeona serikali tangu 1963 imekuwa mbaya. Na musifikirie hapa tu ndiyo nyinyi ni maskini. Ni watu tu watu kumi ambao wanakula hii nchi. Ni watu kumi hata sio village yao. Hata ukienda huko Baringo mzee watu hawana chakula, hawana mavazi, kule bara yangu natoka kule western hatuna university hakuna bara bara hakuna chochote. Mumeelewa eh at maseno? Maseno iko Nyanza, Kisumu. Western ni kama hapa hapa tu. Na ukienda huko watu wantembea bila viatu. Mimi nianoa nyinyi muko na viatu na sandals zenu (noise) sikizeni mimi nafanya kazi yangu. Hata kama majimbo inakuja kile mimi naomba ni kwamba musiwe na roho kama hiyo. Tuangalie vile tutatatua matatizo yetu. Kama ni majimbo itakuja. Lakini hii mambo ya kufikiria kila mtu anakula hakuna watu kumi tu wanakula. Sababu musifikirie kila mtu huko bara ako na pesa tukae kama wa Kenya tutatue matatizo namna gani nini. Umasikini, mashamba muko ma-squatter mimi nimeona mwenyewe. Hatukujua. Lkini nani amefanya?

Hiyo ni serikali ikiwa mbaya ni mbaya na imkuwa mbaya kwa kila mtu. Musiwe na roho kama hiyo. Kama huyu mzee ameongea nikaona unaweza kuanguka na high blood pressure (laughter) Ni uchungu lakini, ni serikali. Na tutatatua hii tatizo namna gani? Hilo ndilo swali na msifikirie watu wa bara wemkula. Hawana hata kiatu, hawana hata baiskeli. Hakuna.

**Jasho:** Maombi tu naomba basi nilikuwa naomba katika swali kumbwa kama la ardhi ambazao zimenyakuliwa ziregezewe wananchi wenyewe ambazo ardhi zao zimenyakuliwa na sasa wamekuwa masquatter kwa ardhi hizo. Zimechukuliwa mkopo zimeuzwa na mwenyewe yuko hapo hapo anaambiwa wewe huna haki. Kwa hivyo ardhi hizo ziregeshwe zote katika Diani na Kwale nzima na Pwani nzima (clapping)

**Com. Swazuri**: Peter Ahenga? Dakika tano.

**Ahenga**: Asanti. Hamjambo wazee na vijana? Kwanza nasikitika sana kuhusu haya mambo ya majimbo, tuna shida. Kila

anayeongea asema sisi Pwani tunataka majimbo tunataka tujitawale wenyewe. Vile com. Nancy Baraza amewaambia kamba hata kule bara mimi ninatoka Nyanza (noise) sikiza, tuelewane pole pole. Hata sisi tunaziona huko huko mbala. Ukitofauatisha Rift Valley ukiingia Nyanza hizi taabu unaweza tofautisha. Hapa ukiingiia Nyanza hizi taabu unaweza tofautisha. Hapa kuna utawala hapa hakuna utawala kwa hivyo hii ni taabu ya kila mahali. Nikiachilia hayo kuna mambo ya haki za kibinadamu, kuna mambo ya health care. Maoni yangu kuhusu health care, nikamwamba yoyote ambaye ni maskini ama tajiri hospitali yoyote iliyoko karibu naye iwe ni private, iwe ni ya serikali iwe anaweza kuingia atibiwe bila malipo yoyote. Na yule mwenye ile hospitali serikali iweke namna either ana insure wananchi wake ili serikali iweze kulipa yale malipo. Sio, maanake uzima ni kitu muhimu iwe ni kwa tajiri iwe ni kwa maskini. Katika nchi yetu ya Kenya utakuta kwamba maskini anakufa zaidi kwa sababu sio kwamba ugonjwa wake hauwezi tibika, bali ni kwa sababu hana ule uwezo.

Halafu kuna mambo ya vitambulisho. Haya mambo ya vitambulisho polisi wamekuwa wakiangaisha raia sababu ya vitambulisho utakuta kwamba labda mtu amesahau kitambulisho chake nyumbani, ni saa mbili saa tatu, saa inne, usiku. Maoni yangu ni kwamba huyu bwana asishikwe. Either polisi amu-surmon kesho abebe kitambulisho chake akipeleke police station kudhibitisha kwamba alikuwa na kitambulisho alifanya kuisahau. Ama kama huyu polisi ana tashwishi zaidi ampeleke huyo bwana mpaka pale aliposema kwamba alipoacha kile kitambulisho amuonyeshe mimi naishi hapa na kitambulisho changu nilikuwa nimekisahau ni hiki hapa aachiliwe. Mambo ya kupelekwa cell au kortini sababu ya kitambulisho yaishe.

Kuna mambo ya polisi kuhangaisha raia. Maoni yangu na kulingana na research ambayo ilifanywa kuna wale polisi ambao hawana vyeo. Wanaoitwa ma-constables hawa polisi wasipatiwe haki ya kushika kuhoji mushukiwa ama mtu yeyote. Yeyote atakaye fanya kosa ahojiwe na polisi ambao ana cheo cha juu kidogo. Kwa sababu hao angalau wamesomea mambo ya public relation na mambo mengineyo. Lakini wale ma-constables anataka kuweka kifua mble maanake anaonelea labda unamdharau kwa vile yeye hana cheo ama mambo kama hayo. Atachunguza kesi akupeleke mahakamani bila kuchunguza ile kesi sawa sawa.

**Com. Swazuri**: inaudible

Ya mwisho, kuna Provincial administration, chief Do na kuendelea. Hawa mabwana lazima waelewe kabisa kabisa kwamba hawa ni wafanyi kazi wa raia. Haya mambo ya kuambiwa ufike kwa chief saa tatu, na yeye mwenyewe anaingia saa tano.

Tunataka raia awe na haki ya kumuuliza huyu Chifu kwanini amechelewa. (**clapping)**

Kulingana na structure ya government, haya mambo ya prime minister kwa maoni yangu mambo ya prime minister na two deputies na president na deputies mimi naona haifai. Maoni yangu ni tuwe na present system ya president lakini power zake ziwe devolved zirundi chini. Hizi decision making zingine zifanywe hapa hapa nchini. Sio lazima aone kuna shamba nyingine. Kinondo aandike barua mwenyewe hajaiona, iwe imepitshwa. Shamba imepewa councilor Mabavu ama impewe mtu mwingine. Sisemi Councillor amepewa, (**laughter**) in mfano tu.

**Eunice:** Asante Mwenye Kiti wa Katiba pamoja na wenzako na wananchi mliofika hamjambo? Mimi niko hapa kuzungumza na represent kikundi cha wakulima kutoka Nguluku Centre Msambweni Division. Mnanisikia vizuri. Jina langu naitwa Eunice Buko na mimi ni mkulima wa sehemu hiyo. Kwa niamba ya wenzangu tunasisitiza Serikali ya Majimbo, kulingana na Katiba ya 1962 huko Lancaster House.

Kuhusu elimu tunaomba Katiba ishughulikie swala la kuptisha kuwa elimu iwe ni bure kote nchini kwa sababu kuna wengine ambo hawana uwezo wa kusomesha watoto na watoto wengi sasa imekuwa wanakaa nje bila kusoma. Kwa hivyo elimu iwe bure kuanzia primary mpaka Form 4.

Halafu Uajiri. Kusiwe na ubaguzi wa vyeo au kielimu. Watu waajiriwe kulingana na elimu walio nayo katika wilaya zao au katika jimbo lao. Mishahara iwe ya juu isiwe ya chini ya elfu kumi kwa mwajiri yeyote. Malipo ya nyumba yazingatiwe kwa wale walio chini ya elfu tatu na hata kwa matibabu pia.

Biashara zimekuwa zikitatiza kwa sababu mambo mengi yamekuwa yakipandishwa, bei zinapandishwa hata kama ni madukani ama ni kwenye viosk zinapanda, tunasahau yule mwananchi wa chini ambaye pengine hata hana uwezo wa kupata zile pesa. Kwa hivyo kuwe na sheria ya kuangalia bei hizo za biashara.

**Com. Swazuri:** Price control.

**Eunice:** Mutanirekebisha kwa sababu….Haki za watoto. Watoto wapewe elimu na pia malezi bora na mavasi. Wazazi

wanaoachana wanaotengana wamesababisha familia nyingi kuwa na maisha yasiofaa. Kwa hivyo ikiwa ni mume ameamua kumuacha yule mke baada ya miaka tano kuwe na sheria ………. **(End of side 5A)**

**Eunice: (cont..)** Nina zungumzia swala hilo kwa sababu mimi mzaliwa wa mahali pengine lakini nimeishi sana hapa na nimeona shida zinazotokea hapa. Mwanamke anakaa na familia, anazaa watoto saba, mwanamke anakuja kufukuzwa hana chochote. Mme akifaa anafukuzwa. Hapewi chochote. Si mnaona hiyo ni shida?

Haya swala la ardhi. Mwananchi awe na mamlaka ya kumuliki ardhi yake maana ardhi ndiyo urithi wa kutoka babu zetu wa kiafrica. Na ukubwa wa ardhi, wa mtu binafsi usiwe chini ya akari hamsini. Isiwe chini ya akari hamsini (interjection not clear) eeh kwa mtu binafsi. Halafu uchimbaji madini (interjection not clear) ni kulingana na vile watu wamekaa wakazungumza.

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Eunice**: Haya basi nimsema mahali kuna makosa mtanirekebisha lakini ni kulingana na vile wameketi wakazungumza.

**Com. Swazuri:** Inaudible

**Eunice:** Halafu uchibanji wa madini (bona mwaniharakisha sana). Uchimbaji wa madini. Iwapo shamba ya mkulima itapatikana na madini, mkulima anapaswa kushilikishawa na mipango yoyote inayohusu eneo na pia eneo la kilometer kumi na tano kutoka sehemu ile ya madini. Wakulima wanaoishi pale wanaweza kuadhiliwa hewa ya sumu kwa hivyo pia walipwe na kuhamishwa.

Uridhi: Watoto warithi kutoka kwa wazazi wao na pia wanawake warithi kutoka kwa wazazi wao na pia bwana zao. Ningezungumza mengi lakini wakati una harakiswa harakiswa sana kwa hivyo mtanisamehe.

**Com. Swazuri:** Asante toa memorandum zako pale. Haya, Hamisi Ramisi.

**Hamisi:** Mabibi na mabwana saalam aleikum. Mimi nashukuru sana ya kwamba karibu yale yote ambayo yameandikwa katika memorandum hii ya shirikisho yote yamezungumzwa na nimefurahia ya kwamba vile ndivyo tunahitaji. Commissioners ningependa kusema to highlight this things ningependa kiusema ya kwamba aina ya serikali ambayo tunahitaji si nyingi ila ya majimbo. Iwe na president, ambaye ndiye atakaye chagua Prime Minister. Prime Minister ambaye ndiye atakuwa Head of

Government.

Kitu kingine tunamtaka rais awe tu ceremonial President. Pia parliamentary federal government iwe itakuwa na uwezo ya kumuimpich President mala tu atakaye kosea. Kitu chininge tulizunguzia habari ya judiciary pia tuakasema ya kwamba tunahitaji kuwe na supreme court. Supreme court iwe ndiyo itakuwa above.

Pia, katika sheria tulionayo ama katiba tuliyonayo, imeandikwa ya kwamba Constitution uhuru wa kuabudu uko katika Kenya hii. Lakini maajabu yaliyoko ni kwamba uhuru wa kuabudu ule ule umetengwa kwa mambo matatu tu. Katika Kenya hii kinyume na sheria za ulimwengu au za dini kwa sababu kuabundu sio ndoa, taraka na urafi pekee yake au kujenga misikiti tunaenda kusali huko, si kuabundu peke yake. Karibu kila kitu kimeandikwa katika Koran kule ni kuabundu kwa Muislam. Kwa hivyo kumfanya Muislam hawezi kumuabundu Mungu wake sawa sawa na kwavile inahitajika iwe hivyo katika katiba yetu tulionayo. Sasa na ndiyo tunataka iwe katika katiba hii basi kumsaidia Muislam aweze kuabundu Mungu wake sawa sawa ama kama vile inahitajika ni lazima ahukumiwe kulingana na sheria ya Kiislam ambayo ni Kora (clapping) na huko ndiko kuabundu ukimpa kinyume cha hapo au uchache wa hapo huo basi ni unafiki au Muislam hakupewa haki za kuabundu hata kidogo.

Upande wa ardhi yote yalizungumzwa ya kwamba ni lazima ardhi zile zote ambazo zilitolewa kiholera ziwe crapped na zirundishwe kwa wenyewe na uzuri ni kwamba kila regional state ambayo itakuwa inajua, wenyewe wananchi wanajua, mpaka ya wengine kila moja ardhi iko mahali gani na wanajua. Kama vile kulivyokuwa tukiishi zamani. Hakuna hata mmoja wakati title deed zilizokuwa hazijapatikana ambaye hakujua shamba yake iko wapi. Kila moja alikuwa akijua shamba yake. Kwa hivyo kurekebisha mambo vile ilikuwavyo kwa vile leo kuna wengine wako na acre zaidi elfu kumi, elfu thelathini katika Kenya hii hii, wengine hawana ni squatters. Kwa hivyo ili kurekebisha swala hilo ni lazima title deeds zote ziwe scrapped na ardhi zirundiswe kwa regional government. (Clapping).

Tunasema ya kwamba Head of government ambaye atakuwa Prime Minister yeye ni lazima awe Kenyan Citizen, ni lazima awe na university degree au equivalent au kingine kinacho fanana na hiyo. Pia tungemtaka awe na umri wa kati wa miaka 35 to 65, asiwe na criminal recored na awe ni mtu na integrity na character yake ni mtu wa kisawa sawa. Asante.

**Com. Baraza:** Awe ameoa?

**Hamisi:** Ni lazima hiyo. Moja kwa moja. Hata waziri tunataka awe ameoa. Ni lazima awe ako nominated na political party ambayo imeshida na ile sheria ya 25% ya kuwa lazima mtu awe ameshida 25% katika provinces tano iwe ni lazima. Kwa vile mengi yamezungumzwa mimi nilikuwa nataka kuzungumza yale ambayo mengi hayakuzungumzwa vizuri na nitaweka hii memorandum iweze kusomwa vizuri. Asante.

**Hassan:** (doesn't say his name at the beginning) Kwa kuonyesha vile nataka nitaanza kuwa slamia ki ile hali ninavyotaka. (greetings in vernacular). Hiyo ni kuonyesha tuko majimbo na ndiyo tunataka ndiyo tunasalimiana kimajimbo. Asante sana. Na kwa kusema kweli tunataka hiyo serikali ya majimbo kwa sababu zifuatazo. Kwanza, viwada ambavyo vimekufa. Nikichukulia mfano kiwada cha Ramisi na nikichukulia mfano kiwada cha Mhoroni huko, kiwada cha Ramisi kilikuwa na miwa ambayo haitaji kuchomwa. Inafunwa inapelekwa kwa machine sukari inatoka safi nyeupe ukiangalia viwada viko mhoroni na sehemu zingine lazima miwa ichomwe ndiyo impelekwe ikasigwe ndiyo itoke miwa. Kwa hivyo naonelea hapa tumedhurumiwa (laughter).

Pili, tukienda cashewnuts hazikufanyiwa utafiti kwa sababu serikali imetosheka huko ikasahau pia huku tunataka utajili mikorosho kwa nini hazizai, na kama hazizai watu wa agriculture wanafanya kazi gani? Naona tukipatiwa serikali ya jimbo mamo hayo tutafanya. Tukija upande wa hizi Iddi days wakati wa siku kuu ya Waislam natumai hii imeleta matatizo. Mara nyingi watu wanasema mwezi umetoka tisa wengine wanasema mwesi umetoka thelathini. Twataka hizi siku kuu za siku kuu ziwe mbili kama vile kuna Chrismas iko na Boxing day tenda kwa na nini basi twataka hii ya tisa iwe siku kuu na hii ya thelathini siju kuu itoe hii matatizo.

Tatu, tukirudi upande wa tendering, narudi upande wa serikali tenders nyingi tangu tupate uhuru hazikufaidisha watu wa Pwani. Tenders zote zimechukuliwa na watu wa kutoka sehemu a mbali kama Western, Nyanza maana tunasema ukweli maana unauma kidogo. Ukweli lazima usemwe. Unaenda kwa ile board ku-supply tu. Nyama kwa hospitali hapa imechukua miaka

hiyo tender imekuwa na Wakikuyu hapa hapa. Sasa imekuwa ni vita mpaka watu kama sisi kuja kupata vitu kama hivyo. Tukirudi hapa hata kuangalia mabara bara hizi za ndani ndani hizo tender zote hakuna mwananchi wa hapa amepewa hizo tender ingekuwa miaka kabisa. Kwa hivyo Serikali ya National imetunyanyasa sana. Vitu kama hizi tumezikosa. Na tunataka hata ku-supply madawa huku tenders ziwe departments – kwa nini wananchi hapa izidumishwe wananchi wapewe nafasi waka-supply vitu kama hivyo?

**Com. Baraza:** Wao wana apply?

**Hassan:** Sana sana tena. Na ukifika kule unaona forms zimetupwa huko kwanza uki-apply ukipita ukifika hospitali unapata huyo mkubwa wa store ametoka Kitui anataka pia ule mwenzake apate hiyo order wewe wa hapa pia inakuwa ni tabu utasupply namna gani hapo? Mambo kama hayo twataka iyangaliwe sana hayo (clapping)

Naona ningezungumza zidi tuingile upande wa mishahara ama twende upande wa masomo. Tukiangalia ukweli upande wa masomo watu wanasema watu wa Pwani hawakusoma. Watu wa Pwani wanataka kusoma na wangi wao ambao hawakusoma wamekosa wale watu wa kuwasukuma. Tukienda na ndugu yangu mabaye alikuw ani student Kenyatta wakati huo, anasema wakati Moi alichukua Serikali ilibidi achukue Wanandi wake awalete pale kwa institution, watu watafutiwe madeski yaani qualifications haziruhusu anaambiwa Head of Department chukua huyo sasa yule Head of Department anasema bona qualifications haziruhusu hizi mpaka hyuo mtu anaingia mpaka huko darasani hakuna madeski hakuna blackboard ama ni chalk. Si ulichukua watu? Sasa ukiangalia jambo kama hilo inaonyeshana watu wamesukumana na sisi tunakaachwa hivi hivi mtu amepata ka D+ ambaye at least akisukumwa pengine amefail kwa bahati baya anaweza kuendelea mpaka akawa Doctor mzuri. Na wako ambao watu madaktari ambo walifail kidogo lakini walipo sukumwawalipoenda India wakaja na qualifications nzuri sana. Kwa hivyo hii madharau ya kuwa watu hawakusoma mimi nakataa kusukumanwa ndiyo hakuna. Na hatuna ule mtu wa kusukumana. Ni hayo machache asant. Mimi jina ni Hassan Yusuf Mwasio.

**Com. Swazuri:** inaudible

**Speaker:** Commissioners wazee salaam aleikum. Mimi sitazungumza mengi lakini yangu ni yale yale ambayo twakaka majimbo tumechoka. Kutoka enzi na enzi tumeumizwa na sababu kubwa na kuzungumza hivyo pia ni kwamba hii system ililetwa na 8-4-4 inasema ni zero system haileti kitu, turudishe ile ya std.7, Form 4, Form 6 na university. Kwa sababu (inaudible) masomo mengi wanafanya watoto wetu nafail na university ziko kule kwao hapa hakuna university afadhali mtu afike Form 6 tutakuwa na wa Form 6s lakini kwa vile universities ziko kule watu wanakosa nafasi za kuenda university. Kama alivyozungumza mzee akasema wanasukumana kule. Kwa hivyo afadhali tuanguke Form 6 kwa maana hakuna university hapa kwetu.

Nyingine nazungumzia ni kwamba hawa police officers wasichukue mtu mbila usaidi ile habari ya suspect iyondoke mtu akishikwa awe ameshikwa na kupelekwa kortini na polisi yuko pale anatoa usahidi na kazi maimi ndiyo natoa usahidi na ule mtu. (clapping)

Nyingine nazungumzia la Mwisho kwmaba yawe chini yetu. Uajiri. Fedha inapatikana hapa Pwani ibaki Pwani. Kila kitu kibaki hapa tujiamlie wenyewe mambo yetu tutengeneze bara bara, madawa, mahospitali kila kitu. Kwa hayo machache asanteni.

**Com. Swazuri:** Salim Mwasema. Ufanye haraka dakika tano.

**Salim:** Commissioners na wahesimiwa nyote mabibi na mabwana salaam aleikum. Mimi nitazungumzia Kenya, nazungumzia Kenya kwamba serikali iliyoko ni baya kwa Kenya nzima. Kwa hivyo tunahitaji majimbo katika wakenya kila watu wajisimamie kwa sababu ya uchoyo wa yule aliye jikoni. Maana usimlilie mwanaye na mwana wa mwenzio pia amuangalie sisi tunasema kwamba tulipigania uhuru ili watu wafaidike hatukupigania uhuru wa mtu mmoja.

Hii above iyondoke maswala yote ya kiutawala kila watu wapewe mamlaka yao kwa sababu nyumba ni kubwa, baba ni mmoja anapewa mamlaka yao kwa sababu nyumba ni kubwa baba ni mmoja, amepewa nyama atawapawatoto wawili. Lakini wengine wankosa. Kwa hivyo tunasema Kenya hii, ni Kenya lakini ni nyumba kila mtu awe na chumba chake na afagie

mwenyewe yule anayekosa kufagia chumba chake huyo ni shauri yake tunataka katiba irekebishwe kwamba Kenya iwe na serikali ya majimbo. Kenya nzima kila watu wajisimamie yule asiyeweza kujisimamia atasaidiwa na jirani yake. Si kwa sababu yeye awe na uwezo vile tunaomba miswaada kutoka nje naye taomba katika jimbo jingine kwa sababu sisi ni ndugu.

Elimu: Elimu watu wa Pwani ilishuka hapa, elimu kutoka mwaka wa 1928 akajengwa shule ya kwanza lakini kwa sababu watu wengine wakikaa kufikiria ya kwamba watu wa Pwani wana vitu vingi. Mwarabu alifikiria hicho kitu akamwabia mzungu si wasomeshe hawa? Akasema hii ni halamu hii. Hii ndiyo tulinyanyaswa hii na leo kumekuja mtindo mwingine kwamba watu wa Pwani hawajui kusoma kwa sababu ya umasikini tulionao. Viwada tunavyo hakuna.

Bamburi ilikuwa yataka kunjengwa Shimoni imeplekwa kwingine, je tutafaidika vipi sisi wananchi? Kwa hivyo jimbo si hilo la kufukuza mtu,si hilo la kusema kibinafsi hata wa Pwani wako bara. Lakini tunasema mwenye chake apewe uwezo yule mtu wa bara aliyeko hapa awe yeye ni mtu wa Pwani amekaa miaka ishirini hapa. Atakuwa kwenye jimbo kwa sababu hata sasa manufaa yake yako kwenye jimbo hili. Kwa hivyo naye awe na uwezo wa kusimamia pamoja na sisi. Ukikataa utakwenda (clapping). Maana Wahindi waliokataa kutawaliwa na Wafrika waliondoka.

Aficanization ilipoingia watu walichaguana. Kenyatta alichukua watu wake wote akawaweka kwenye duka maalum. Sehemu inaitwa Nyeri hata si mtu wa Nyanza alichukua watu wa Gatundu na sisi ndio tulipigania Kenyatta atoke. Muingeleza akasema huyu ni kiongozi wa kisa na vifo. Tukasema la. Huyu ni muarisilishi kwa hivyo lazima apewe power. Lancaster house ilipokwenda watu walizungumza kwamba kuwe na Serikali ya muafrika ambaye atakuwa na uwezo. Hao mimi kuna muafrika fulani kama mtu mwingine alivyosema kwamba Kenya nzima kuna watu themanini na mbili ndiyometajiri hao. Wamewekwa mfukoni na mtu.

Ufisadi unafanya mtu anachukuliwa hapa kiwada hiki amekiharibu anapelekwa chingine. Kwa sababu ya above. Ni utawala wa mtu mmoja. Tunaseme kwamba Kenya ni nchi moja lakini kila mtu ana nyumba yake, kila mtu anamazingira yake kila mtu ana mipango yake sisi watu wa Pwani na hao watu wa Nyanza watu wa Central watakuwa na madirifu yao. Akiharibu ataabiwa wewe unaharibu nyumba yako.

Leo kuna sehemu nyingine ukienda mtoto mtihani anfanya anaonyeshwa makaratasi. Je sisi huku tuaonyeshwa na nani? (clapping) Kwa hivyo Commission tunaiyomba serikali iwe ya majimbo na majimbo haya si ya Pwani pekee yake tuwe Kenya nzima lakini kila mtu awe na nyumba yeke. Hivi ndiyo serikali tunaitaka kuwe na President ambaye hatakuwa above. Na chifu aah . Huyu ni ukoloni na pia tunasema bunge pia lizungumze Kiswahili. Sisi lugha ya taifa ni Kiswahili, bona twazunguma kiingereza nday ya bunge, je sisi Waingereza? Waitaliani waliwatawala Wangereza miaka mia tatu, je wanazungumza Kiitalinai katika bunge lao? Kwa nini sisi tuzungumze kiingereza nyinyi watumwa sisi? Kwa hivyo tunataka katibayasasa uwezekano hata mtu akisoma afike binguni lakini tunasema akifika kwenye bunge na katiba iyandikwe kifasaha Kiswahili kila mtu atakifungu asome. (clapping) (discussions in the background).

**Com. Swazuri:** Juma Mwandarasha.

**Juma:** Commissioners na wenzangu wote nafikiri hamjambo. Kwa kweli haya yote inyozungumzwa wengi wetu ndio tuliya-plan tuzungume hayo mambo ya ardhi mambo ya kazi, lakini sote lazima tutoe mambo yetu. Mimi nimetumwa na wazee fulani huko kijijini kuwa ukifika huko sisi hatutaweza kufika huko Ukunda ukawambie huko kwetu majimbo. Na leo majimbo yatashida?

Tulisho mwambao wameniambia hivyo na pia wenzetu hapo ikiwa majimbo haya ina watu wote Kenya imeshida tuliyoahindi kule tulikotoka tuwe na mwambao wa pwani halafu hii katiba iliyoko – mimi sana hali ya elimu ndiyo imenifanya niungane mkono na wale wazee wamenituma. Kwani hali ya elimu kule kwetu imezorota kimakusudi yaani angalia shule ya kitaifa tunapelekwa huko. Huku kwetu hakuna, university hakuna, unajua university za kujengwa kwa mfano Ukunda hata kma husomi lakini mzee akipata kibarua pale mtoto wake atasoma. Maanake iko around. Ile shule ya taifa hata kama mtoto wake hatasoma lakini yeye mwenyewe akiwa amepata kibarua ple mtoto wake atafika bali sana. Kwa sisi hivyo vitu vyote huku, wale wazee nimeunga mkono hali ya elimu iko baya.

Na pia, ningeunga mkono wanzangu ziiwe ya bule kwani elimu ya primary imekuwa ya bule hasa. Hii mchango mchango wa wazazi iwe ni harambee badala ya kuwa watu fulani wanchauliwa chairman halafu wanakata shauri kwua kila mmoja shilling mia

tatu tatu. Nimegundua hii kitu. Mimi mwalimu nimegundua hii kitu wazazi wenye watoto werefu sana wamebaki nyumbani kwa sababu ameabiwa shule yetu ya hapo Ukunda kwa mfano, mtoto kuiingiza mtoto wake ni elfu moja mia nne hana. Na kuna watu hawajapata elfu moja mwaka mzima papa moja hajaipata anaambiwa apeleke mtoto. Sasa kwa hivyo nina omba kama tungeipata ile mambo yetu tuinjenge kwa harambee. Na kufundishana na harambee kama zile za kuenda kwa secondary uongo mpaka uwe na umarufu mtoto wako ndipo asomeshwe. Na watu wa watoto werefu ndiyo maskini na ni wengi ni harambee kila moja anataka kuenda naye atafanya harambe.

Halafu pia kuna kama Starehe Boys. Hakuna mzazi hapa anajua mambo ya Starehe Boys na ni shule ya masikini. Je tunaijua sisi? Imesidikwa huko Nairobi sisi hatujui. Ni wale ambao ni masikini wanapelekwa Starehe Boys watu wanasoma huko mpango wake hata hatujui, wanaosma wale wale matajiri. Nafasi Starehe Boys pengine ni watu mia tano wataenda kama watoto wa masikini tena wamechukuliwa na watu watutu tu ama mia moja tu hakuna hata wazazi hawajasikia hilo neno.

Ni ardhi tafadhali nimezungumza mambo mengi yamegusiwa. Hii ardhi imetolewa sana. Kwa mfano sehemu zingine huko wamelazimishwa wazazi kama watu wenye maardhi iwe ni lazima wakiambiwa na watu wakumbwa wakubwa, pia nao ni wenzetu ukifanywa hoteli hapa, watoto wataandikwa ni wenzetu tumewachagua wengine, wengine ni chifu, wengine ni wakina nani, halafu ikinjegwa hapo huna lolote hapo. Mtoto wako hakanyangi. Kwa mfano kuna hoteli ya Southern tuko karibu, mimi niko, kuna pale hakuna hata mtoto mmoja anatoka hapo village anafanya kazi hapo. (interjection not clear) Hizo ardhi nataka zirundishiwe wenyewe kwanza zimechukuliwa kwa kiholera sana. (clapping)

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Juma:** Ndizo hizo basi. Hizo zirundishwe na tena pia, huku Pwani, mimi hufikiria kama Lord Delemere alikuwa na mashamba sidhani kuwa yuko ama mtoto wake anayo. Bona huku kwetu shamba zile bado zina wale wale ama zimechukuliwa watu wengine wakutoka bali? Kwa mfano Thomas yuko pale pale, Waitiki haijulikani kazi lake? Haijuliknai na nyingi kwenda sijui huko lakini hizo mimi naona Lord Delemere (interjection not clear) huko shamba zote ziko vile vile lakini zetu kunazo ziko vile vile. Kwa hivyo Lord Delemere yuko pale pale baado analima wingi hapo.

**Com. Baraza:** eeh na wanyama wake?

**Juma:** Nasikia huko kuna watu maana wamepewa. Shamba zimegawanywa.

**Com. Swazuri:** Je wewe wataka aje?

**Juma:** Nataka shamba turudishiwe. Kwa hivyo hizo twataka turudishiwe halafu kama mistu hii, kama walivyo zungumza watu wengine hivi watu vyo asili ambavyo tunavyo karibu karibu navyo vikichukuliwa na watu fulani mpaka nao wazee wa mji wasiopungua mia moja wauhusiswe ama wanaenda vipi. Sio kuwa mtu mmoja halafu akipata kitu kidogo inakwisha mala msitu unachukuliwa ama sehemu ya bahari imefungwa fungwa ni mtu mmoja ametia sign. Kwa hayo machache nafikiri nitatoa memorandum yangu ndiyo ina mengi. (clapping)

**Com. Swazuri:** Asante sana. Maiyoyo? (not clear)

**Maiyoyo**: Kwanza ni serikali ya jimbo ndiyo tunataka sisi. Kuna watu wamesema wengi wengi kuwa sisi tunataka mashamba … oh mashamba yaliharibiwa na watu wa bara. Ni warongo (laughter) singekuambia ni warongo mzee watu wa bara nakupa kiti wewe endelea na wenzio pale. Lakini wale wale ambao wameopewa ukubwa wale ndio wanonyanyasa watu. Ukisema ni mtu wa bara wajisemia kama hauoni. Lakini kila mtu ameletewa mtu machoni mwake. Wewe Councillor chunga nchi yako, Chifu chunga nchi yako. Wewe ukisema unaonewa na watu wa bara lakini wajionea wewe mwenyewe nyinyi wenyewe Wadigo kwanza hampendani. Hampendani. Hawa wanandanganya …. Oh watu wa mbala oh ulongo hapendani. Chifu hapendi raia, Councillor hapendi raia wake, yule ambaye ni aitwa aje? Mbunge hapendi watu wake. Atapitishwa ile siku ya kupitishwa anapotea. Hawezi kukarimbia tena watu wake. Kweli watu wataweza kusikia maneno ya nchi inavyoendelea? Hawezi kusikia na Councillor anakuona njiani lakini ile shamba yako ndiyo anataka uchukue. Hapana sema watu wa bara munawalaumu nini? Mtu wa bara hana ubaya lakini wa baya ni nyinyi wenyewe Wadigo. Ingekuwa mko watu wazuri tungona watu wa bara wakitusifu yakuwa Wadigo wanapendana.

Haya utasema baharini …. Oh … huko kuna hoteli sisi hatuchukuliwi. Nanyi nyinyi nao wasomi na Wabunge wako hapa kwa nini huwezi kuchukua mzungu wewe mtu msomi ukashikana naye nchini yako ukabebana naye mpaka ukapata hiyo njia? Lakini wewe utashutumu mtu wa bara, lakini mtu wa bara hana ubaya ameshikana na mzungu anamwita mzungu hapa, anaweka hoteli lakini yeye akifika Councillor hatetei watu wake hata (**laughter).**

Kwa hivyo sisi tunataka Councilor kama hasikii wananchi apewe retire aondoke. Chifu hivyo hivyo. Ikiwa hataki kuwalea watu wake kwa nini tukae naye? Mtu namna hiyo? Watu wa bara saa ayote watu wa bara ….. ah ah. Ni mambo mumeletewa. Semeni ule ukweli wenu. Wasema watu wa mbla wenzetu wafanywa nini ….. university … kwani nyinyi university mlitaka mkakataliwa? Si leo mutake university mletewe? Watu wapeleke**. (noise**).

Haya nimesikia uchungu kidogo nina uchungu na hii nchi. Mna uchungu na watu wa bara…. Watu wa bara… lakini wanaumiza na wenyewe.

Kwa hivyo tunataka majimbo ya kupendana, hatutaki majimbo ya vita sisi tunataka majimbo ya kupendana. Hiyo ndiyo njia ya uchumi sio tulete majimbo ambayo haina uchumi.

**Com. Swazuri:** Haukusema jika lako mzee. Mzee ……….? Haya Dzombo yuko (noise)

Speaker: Liangaliwe na soko zitafutwe ili wananchi wote wapate haki yao. Uchumi tuukuze. Hatutafufua uchumi ikiwa tunatupa mali yetu. Ni tuwe na mali inayoleta pesa ili utfufue uchimi na mwananchi ajitosheleze. Mwisho kabisa na malizia na wale ambao wamekuwa matajiri zaidi. Wanachijua pesa hizo wanaenda wanaweka nchi za nje. Unakuta mtu ameweka pesa katika bank ya Swiss. Na hali hapa kuna mwananchi hata posta yenyewe kuweka pesa katika posta hana. Kwa nini pesa hizo kama ana pesa nyingi asikweke katika banki za Kenya zi-circulate katika nchi yetu, ili ule ushuru ufaidi na ujenge na uwe uanaleta maendeleo katika nchi yetu. Sasa tunaenda kuweka pesa nchi za nje huko. Unakuta mwananchi wa huko anafaidi maana nchi yao ina pesa nyinyi watu wamekuja kuweka. Na sisi tunaendelea kuwa maskini. Jambo hilo liangaliwe.

Mwisho kabisa, ni pesa zile mtu akienda bunge. Aeleze utajiri wake ili miaka mitano ikifika asiseme ana billion ishirini amezita

wapi na halipwe billion moja kila mwezi. Tujue mahali hizi pesa zimezotoka. Kwa hayo machache nasema asanteni (clapping)

**Com. Swazuri:** Wamunga?

**Wamunga**: Macommissioners na wenyenji wa Ukunda, mimi kwa majina naitwa Jave Wamunga Wabechirobasi. Ni nazo sababu tano zilizonifanya nikae hapa. Ya mwanzo ni kuhusu federal government. Sisi ukweli kabisa twakata federal government, majimbo. sababu ambazo zimefanya watu apige meza hapa ni kwamba wamechoka. Na kama Watu wanasema wataka majimboi mwaka huu twataka majimbo, mwaka mwingine twataka majimbo, twataka nini zaidi. Ndiyo maana yule kijana mmoja Amir amesimama hapa akasema kuna siku atataka majimbo kwa lazima. Je, sasa kama sisi tunangojea mpaka situ ile hao watu wanaotaka majimbo kwa lazima wataka majimbo yao kwa kazima itakuwa ni Kenya ipi hii twataka? Kwa hivyo serikali itoe fund ambayo itaeleza wananchi wa kawaida pesa fulani ambayo itazunguka Kenya nzima kueleza majimbo ni nini. Kwa sababu watu wengi hawajaelewa kwamba hawa wanataka majibo aina gani.

Kwa hivyo mtu wa bara akisikia mtu wa Pwani anazungumzia swala la majimbo, anamchukia kwa sababu anaona hapana pale Kilindini kuna watu elfu kumi na inne, elfu inne ndiyo watu wa Pwani, elfu kumi, ni watu wa bara sasa wanona kwamba nafasi ile itakuwa vice versa. Kwa hivyo wanachukia swala hili. Kwa hivyo itoe pesa, itenge, iweze kuelimisha watu wa Kenya nzima kuhusu federal government. Na kama itapita watu wapewe federal government. Sisi tupewe majimbo, wakamba wapewe majimbo yao na nini tuwe tuna central government.

Pili, Harambee. Hizi harambee Kenya kutoka uhuru zimedanganya watuwengi sana. Mtu atachuma kama alivyoongea huyu mwalimu aliyekuwa hapa billioni mbili na billion mbili hizi atazitumia kwa njia ya harambee ili aweze kundanganya uma. Aweze kundanganya uma ili aonekane kiongozi ili aweze kupata ile, power ili aweze kuumiza zaidi. Hapa hatuwezi kumtaja mtu. (interjection. Com. Swazuri: inadible) Lakini hii mambo ya harambee kama ikiwa mimi ni mfanya kazi na mimi nalipa kodi. Halafu kodi ile ile inaingia kwa serikali. Pili jioni naletewa resiti natakikana skuli nikatoe elfu moja ya mwanafunzi kisha siku ya harambee nipelike pesa ingine. Hii kodi ni ipi na hii harambee ninayotoa mimi ni ipi kwa hivyo harambee haifai. Serikali itoe kodi na kila kitu iendelee.

Ya tatu, ni kuhusu mipango ya utawala. Utakuta kwa mfano Pwani pale kwa PC ni Mnandi, DC pia ni Mnandi katika constituency ishirini na moja tuna ma DO sitini na tatu na katika sitini na tatu watu wa Pwani ni Saba. Hii sidhani kama ni sawa. Kwa hivyo ikiwa pale juu yuko Zecharia Cheruiyot, hapa chini pia awe niwa Pwani na anapanga latiba kwamba je, nimechukua watu saba kule wetu, kule kwenye provinces zingine, tupeni watu saba hapa. Hawa wengine hamsini na sita watakuwa wetu ili jambo likizungumza na PC na lipishwa na DC lipitishwe na Do wakulaumu sisi tutakuwa hatuna, tutajilaumu wenyewe.

Nne, sisi tuna madini hapa Msambweni, tuna madini vipingo, tuna madini Magarini, tuna madini Voi, kwa hiyo madini haya kama ni kuchimbwa haya madini yanayozozaniwa na kampuni ya Canada, sisi tupewe mamlaka hapa kuna wasomi wa kutosha, Kwale kuna Kwale Proffessionals halafu kule Kilifi kuna wasomi sana. Kwa hivyo (interjection,Com. Swazuri inaudible) Ndio lazima mahali ukienda huwezi kutia moto, lazima ukate kate mwanzo.

Sasa hao wasomi wakae chini watoe repoti ambayo pia najua washafanya. Wakishamaliza hivyo hiki. Kiwanda ama hivi wiwanda vipewe nafasi ya kuchimba, ili ziweze kunufaisha mtu wa hapa watalipa kodi kwa serikali. Mfano, Japan, wakati walipopigwa bomb na America wao waliumia na wao sasa hivi wana lead kwa sababu pesa ambazo walilipwa na commonwealth ndiyo zimeweza kuwanufaisha wale. Sasa sisi tunalilia hoteli, lau kama madini inachimbwa hawa watalii watasema Kenya hakuna usalama kwa sababu kuna radioactivity series katika maji, katika samaki katika vyakula. Kwa hivyo tutakosa madini na tukose wageni. Kwa hivyo hotel industry pia itakufa. Kwa hivyo ikiwa itadufa na sisi tukose ma kazi basi tuwe tumepata huku. Sio tukose hoteli, kisha tukose madini. Kwa hivyo madini kwa mukhtasari yapewe watu wa Pwani wachimbe na walipe kodi.

Ya Mwisho, ni kwamba napongeza tu mwalimu hapa aliyeondoka, amezungumza swala la agriculture sasa sisi hungonja mpaka mambo yakaharibika wakati fulani nyuma kidogo kulikuwa kuna maembe haya ambayo yanayouzwa hizo shillingi mbili yale amezungumza. Ilikuwa kuna fruit fly, maembe haya ilikuwa inapelekwa Saudia kukatokea kwamba kuna fruit fly, kutoka siku hizo mpaka leo fruit fly yule yuko na wizara haijachukua hatua na maembe yaendelea kuzaliwa vile vile. Kwa hivyo ningeomba, wizara zinazoangalia mambo kwa hivyo ningeomba, wizara zinazoangalia mambo ya agriculture isikae tu ofisini watoke nje katika research wafanye research na watu wetu wako hapa wasomi. Asanteni.

**Com. Baraza:** Mzee uko cooperative ya hii matunda kwa sababu huko kwenu hakuna maembe na yanozea hapa na watu hawanunui - kuko ka cooperative?

**Wamunga:** Ngoja sasa nirudi mahali umeniuliza cooperative ziko kwa sababu tukizungumza cooperatives kuna vikundi hapa vya akina mama halafu kuna watu huungana watatu wanne wakaenda bara. Mimi nisha wahi kwenda mpaka Kibuye Market. Ukifika Kibaye market na wakute kwamba unaitwa Bakari, unaitwa Charo, unaitwa Chengo ukipeleka maembe hivi sasa unaulizwa hiyoembe unaulza aje mzee? Unamwambia hiyo embe ni shilingi kumi kwa sababu umechukua bei ya mkulima na pia usafiri lakini wanakataa kununua direct kutoka kwako. Wanataka nunue direct kwa yule mtu ambaye wanazungumza lugha moja. Hii ndiyo tatizo. Na si hiyo hata ya nazi. Huwezi kuchukua nazi hapa ukapeleke mbea. Ukifika kule wanataka mtu wao anunue nazi hapa apeleke kule. Kwa hivyo pia katika hiyo biashara ina ukabila. Hata hayo maembe tunayozungumza kwamba yalikataliwa Saudi Arabia kwa sababu ya fruit fly ni sababu yalikuwa yanapelekwa na watu wa hapa. Na kule Malindi yalikuwa yanapelekwa na hawa watu wa Malindi bus kwa hivyo ikatiwa hiyo doa la fruit fly. Na wamenunua maembe yenye fruit fly kwa miaka kumi ama ishirini.

**Com. Swazuri**: Stephen Mchenga.

**Mchenga**: Commissioners, mabibi na mabwana hamjambo? Mimi nina sababu nne ambazo zimenifanzya nifike hapa kuongea kuhusu mamo ya katiba. Kwanza ni elimu. Na zungumza sana kuhusu vijana kwa sababu mimi niko katika sehemu hiyo. Serikali inayokuja, tunataka iangalie kwanza mambo ya majimbo. Tukiangali mkoa Pwani colleges au vyuo vya elimu ni kidogo ama hakuna. Inayo julikana ni Shanzu tu peke yake na sio kuwa hakuna watu waliosoma kuliko waalimu. Lakini kutoka Witu mpaka Lunga Lunga nafikiri college ya waalimu ni moja. Kwa hivyo ninaomba serikali inayokuja iangalie colleges halafu baada ya hivyo kuwe na quarter system. Yaani robo tatu ikiwa ni hapa Diani Secondary imefanywa college robo tatu wawe ni wenyeji wa hapa. Sababu hiyo ni kwamba vijana wa Pwani tunakosa ma kazi kwa sababu hatuna soko. Hatuwezi kupigania na vijana wa kwingine kwa sababu walisoma kwa sababu yuko karibu na Mang'u, yuko karibu na wapi lakini vijana wa Pwani wakimaliza Form 4 hawana pa kuenda.

Hata kuwa beach watchman ni shida kwa sababu hawakuenda college yoyote na ni sababu ya kuwa mzazi wake hana pesa ya

kumfikisha Nairobi au hata hajui au vile alivyochaguliwa hata haijulikani. Kwa hivyo tungeomba colleges ziwe nyingi hapa ili tuwe na soko kama vile vijana kutoka Kitui kutoka wapi…. Pia sehemu hiyo ya elimu bursary pia ziongezwe mpaka college level. Maanake kwa college unasukumwa na yule mtu wa Form 4 umeisha lakini siku hizi lazima uwe na certificate ya college. Pia vile vile serikali iangalie scholarship za kwenda ulaya. Mwanafunzi wetu wa Kigiriama wa Kidigo akimaliza kwenda uraya ni shida maanake kwenda India mpaka mamillioni. Hapa kwenu hakuna pesa utaenda India kusomea nini? Kwa hivyo serikali iangalie hiyo.

Kilimo. Sehemu ya kilimo imeachwa sana Reseach centers Pwani hakuka. Kuna mnazi kuna mikorosho kila mmoja anaongea lakini jinsi kwa nini hizi vitu haziendelei ni kwa sababu research centers Pwani zimeachwa.

**Com. Swazuri:** Lakini kuna ya Malindi Pale, matunda …

**Mchenga**: Kilifi institute …. Ndio sio hakuna kabisa lakini hata ukiangalia wale wasomi wa pale ni mtu hajui faida ya mnazi ni mtu hajui maana ya maembe kwa hivyo tuangalie research centre kwa local areas. Mtu ukimwambia mnazi aelewe ni nini.

**Com Swazuri:** You need experts?

**Mchenga**: Yes. Coast experts wamekosekana. Maanake hata mtu wa kusomea mnazi anakua anaenda kangundo hakuna mnazi hataona maana. Kwa hivyo huu mnazi unakosa market kwa sababu hakuna mtu ana ushughulikia.

Ingine mambo ya title deeds. Inakuwa ni shinda kwa watu wa Pwani kuwa na title deeds kwa sababu ziko juu. Kwa hivyo serikali inayo kuja tungeomba mtu awe anapewa tu haki yake. Wazee wa mitaa, Chifu na akina nani wewe wakijua huyu alizaliwa hapa kwa hivyo anastahili kuishi watu wengi wamenyang'anywa mashamba yao ama anauza tu acre moja lakini acre moja itapata title deed within mwezi mmoja. Mwenye shamba yote hana title deed maisha yake yote. Sasa hii pesa inalipwa inalipwa wapi? Inalipiwa nini? Title deed hiyo ina umuhimu kwa mtu wa kawaida kwenda hata kuomba mkopo kwa bank ama wapi. Lakini mtu wa hapa hatakuwa na maanake yeye tayari hana pesa za kulipia kupata hiyo.

Kitu inginge form of government, majimbo ingefaa. President awe mmoja lakini watu wa Pwani wawe wana mambo yao na

yeye President anakuja kuapisha watu kama vile President awe ceremonial. Halafu wakati wa majimbo tuangalie campaign. Hii serikali inayokuja tungeomba ilazimishe campaign ziwe bure. Mara nyingi tunachagua Wabunge wasiyofaa kwa sababu ya pesa. Yeye awekwa Manager wa Port akija hapa ananunua watu. Mnamchagua anaenda miaka tanao hatakuja kabisa. Kwa hivyo amekuja tu kuwanunua pesa lakini iwe bure. Sasa mtu anaweza kuwa ni mwalimu hata wa nursery. Ana mawazo mazuri lakini hawezi akamwambia mtu yeyote anaenda bunge kwa sababu mpaka uwe na kitu ya kutoa kweli ama urongo?

Pia vile vile ningeomba ma Chief na ma Sub-chief wawe wanafanyiwa campaign after five years, wanatolewa, sio mtu anagandamia pale miaka yake yote anapendeza, hapendezi yeye yuko pale pale. Tungeomba mpango wanganliwe Asanteni.

**Com. Swazuri:** Haya wananchi wa Mswabweni nawa Ukuna tumeshukuru sana kwa vile mumekuja kwa wingi nafikiri katika kusikiliza wananchi hii imekuwa na record kwa sisi hatujawahi kupata watu wengi kama siku yaleo. Na tunawashukuru sana muwe na imani kwamba yale mliyoyasema tutayazingatia na baada ya kuandika report kama nilivyoema tutarudi hapa tena, tuje tukae na nyinyi kama hivi tuchambue sasa kila tuliloandika, halafu tutakuwa na nafasi tena ya kujadili na kusema hiyo ni sawa, hiyo si sawa na kadhalika. Kwa hivyo tunawashukuru sana na mzee mmoja atufunge kwa dua maana Mungu ametujalia tumefanya kwa usalama kwa hivyo ni lazima tushukuru. Haya ni nani?

**Maombi**

**Speaker:** Chigomba Baba tusema tusikiane kwa hivyo asante sana Bwana. Twamwomba Mwenyezi Mungu atupe amani iliyotufikia hapa kutoka asubuhi mpaka wakati huu pakwa pako kimya. Twamuomba Mwenyezi Mungu katika haya mambo yaliyosemwa hapa yawe ma elfu na maelfu yatufae katika dunia na akhera.

Twamwomba Mwenyezi Mungu katika hawa waandishi wetu waliokuja wawe na imani katika yale mambo yaliyosemwa ikiwa lilikoseka walielekeze. Twamuomba Mwenyezi Mungu tukiitwa tena tuje mara kumi zaidi ya hivi. Twamuomba Mwenyezi Mungu kule ambapo ni panyonge Mwenyezi Mungu ukupandishe juu pawe na nguvu.(rest in Arabic)

Tukisema … awe Mola tupe mambo mazuri katika dunia. Na utupe mambo mazuri katika ahera. Kwa hivyo twamuomba Mwenyezi Mungu zaidi ya zaidi pia umaskini utuondolee. (Arabic) Pia twawaombea wazee wetu waliyotuachia hii nchi

Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema kule waliko. Kwa sababu wametuachia miembe na minazi mpaka sasa twafaidika. Basi Mwenyezi Mungu naye awafaindishe huko waliko na sisi nasi tupate vizazi vizuri ambavyotwaweza kuwaacha wakatufuatia halafu nasi wakatumbea Mungu.

Meeting ended at 6.00 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**